# MOTIFU ZA YATIMA KATIKA HADITHI TEULE ZA WATOTO

NA

SUDI EUNICE NJOKI

C50/24715/2011

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

NOVEMBA, 2018

## UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

**MTAFITI**
SUDI EUNICE NJOKI
C50/24715/2011

______________________ 1/11/2018
SAHIHI TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

PROF. CATHERINE NDUNGO
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

______________________ 12/11/2018
SAHIHI TAREHE

DKT. PAMELA NGUGI
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

______________________ 12/11/2018
SAHIHI TAREHE

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Wycliffe Kisiang'ani aliyenifaa kwa hali na mali. Kwa wanangu Dennis Simiyu na Sandy Khakasa kwa kunihimiza na kunipa motisha kuifanya kazi hii.

# SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Maulana aliyenipa uwezo na kunijalia nguvu za kufanya kazi hii. Neema na rehema zake zimeifanya kazi hii kukamilika.

Nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu, Prof. Catherine Ndungo na Dkt. Pamela Ngugi kwa kunitia hamasa ya kutia bidii ili kufanikisha kazi hii. Ushauri wenu, maoni, fikra, mapendekezo na mwongozo katika kila hatua niliyopiga, ulinisaidia hadi kufika kiwango hiki. Asanteni sana na Mungu mwenye neema awabariki.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunitia shime katika masomo yangu. Shukran za kipekee zimwendee Dkt. Richard Wafula, aliyeniangazia kuhusu nadharia za vikale na uhalisia na kunitia moyo wakati wa utafiti.
Aidha, siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioshirikiana nao katika masomo na mijadala. Hawa ni pamoja na Inviolata, Pius, Teresa, Alice na Gladys. Nawashukuru nyote kwa kurahisisha safari yangu ya kiusomi na kunifaa kwa njia moja au nyingine. Rabuka awabariki kwa wema wenu.

Nachukua fursa hii pia kumshukuru mhazili wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika Bi. Anne Wairimu kwa msaada wake. Mungu akumiminie baraka zake kuu.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

MOTIFU:

Suala, dhana kuu au elementi iliyo na kisa chenye kutokea mara kwa mara au kujirudiarudia na ambayo inatumika katika kukuza na kuendeleza kazi ya kifasihi au sanaa.

KIKALE:

Taswira kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi. Aidha kikale kinaweza kuwa mhusika, motifu, ishara au taashira ambayo imekuwepo tangu zamani na inajitokeza mara nyingi katika fasihi.

YATIMA:

Mtoto aliyetengwa na jamii kwa sababu ya kufiwa kwa aidha baba, mama au wazazi wote wawili.

FASIHI YA WATOTO:

Fasihi inayowalenga, kuwavutia na kuwapa watoto burudani katika usomaji wao. Ni fasihi inayojumlisha fasihi andishi na simulizi.

MTOTO:

Binadamu ambaye hajakomaa kimwili na kiakili anayetegemea wazazi, walezi kwa mahitaji ya kila siku. Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya, mtoto ni yule aliye chini

ya umri wa miaka kumi na nane. Mtoto katika muktadha wa utafiti huu ni wa kiwango cha umri kati ya miaka tisa hadi kumi na tatu.

UHALISIA:

Kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa kuwa. Ni usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Ni ukweli kama ulivyo katika mazingira.

NADHARIA YA MSETO:

Hii ni nadharia inayohusisha sifa na mihimili ya nadharia tofauti tofauti ili ifanye kazi pamoja.

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Dkt. | - | Daktari |
| Prof. | - | Profesa |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa kinga mwilini |

# IKISIRI

Utafiti huu umechanganua motifu za yatima katika fasihi andishi ya watoto ukitumia hadithi teule za watoto. Utafiti unalenga kubainisha hali zinazochangia watoto kuwa yatima katika hadithi teule za fasihi ya watoto. Pia, utafiti umewezesha kuelewa changamoto zinazowakumba watoto yatima katika jamii. Vilevile utafiti umenuia kuonyesha jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba. Nadharia changamano ya vikale iliyoasisiwa na Northrop Frye (1950-1954) na Nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa na Georg Hegel na kuendelezwa na Lukacs (1972) na Larkin (1977) imetumika katika utafiti huu. Mihimili yake imetumika kama dira ya kuongoza utafiti huu katika kuyaafiki malengo yake. Utafiti unakusudia kuhusisha vitabu teule vilivyoandikwa na waandishi tofauti tofauti. Vitabu ambavyo vimerejelewa ni pamoja na: *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), *Yatima* (Wamitila, 2006) na *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006). Vitabu hivi vimeteuliwa kwa kutumia mbinu kusudio. Pia, vimeshughulikia mhusika yatima kama kikale na mbinu ya kuwasilisha ujumbe katika fasihi ya watoto. Utafiti umejikita maktabani ambamo vitabu, majarida, magazeti, machapisho na tasnifu mbalimbali zimesomwa ili kuupa msingi utafiti. Data iliyopatikana imechanganuliwa na matokeo yakawasilishwa kwa njia ya maelezo na mifano kutolewa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Muhtasari umefanywa baadaye na kutolewa kimaelezo. Utafiti huu umebaini kuwa yatima hupitia maisha yaliyo na matatizo mengi na ya aina mbalimbali. Hata hivyo, utafiti huu pia umebaini kuwa watoto yatima huweza kujiopoa kutokana na matatizo haya kupitia kwa juhudi zao za kibinafsi kama vile kuiombea hali yao, kukumbana na matatizo haya kwa ujasiri wao na hata kufanya bidii ili kujiopoa na hali hizi ngumu wanazokumbana nazo. Kwenye ngazi ya kijamii, watoto yatima huweza kuopolewa na jamaa na hata marafiki. Hali hizi za maisha pamoja na njia wanazotumia kujiopoa yatima hawa zinaambatana na hali ya maisha kwa mtazamo wa nadharia zilizoongoza utafiti huu. Kutokana na haya yote, utafiti huu umependekeza utafiti zaidi juu ya masuala ya maisha ya watoto yatima kwa kuzingatia aina nyingine za fasihi kama vile ushairi, tamthilia na hata hadithi fupi. Pia, imependekezwa kuwa utafiti zaidi uweze kufanywa kule nyanjani kando na huu uliozingatia utafiti wa maktabani.

## ABSTRACT

This research aimed to investigate the motif of orphans in children's written literature using selected Kiswahili Children stories. The study aimed at analyzing the situations in the portrayal of orphans in selected works of children's literature. In addition, this research has made it possible to understand challenges that orphans face in the society. Moreover, the research aimed at elaborating how orphans liberate themselves from the challenges facing them in the society. This research was based on the tenets of the Archetype theory by Northrop Frye (1950-1954) and Realism theory by Georg Hegel which was later developed by Lukacs (1972) and Larkin (1977) as a guide to achieving the research's objectives. This research used selected children stories written by different authors, thus; *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), *Yatima* (Wamitila, 2006) and *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006). These books were selected purposively. In addition, the orphan character was used as an archetype and a mouthpiece in children's literature. This research was conducted in the library and involved the reading of books, journals, newspapers and a variety of theses so as to give the research a basis. The data collected was analyzed and the findings were presented alongside befitting examples following the objectives of the study. The study established that orphans go through a lot of difficulties in life. However, the study also established that the orphans save themselves from such suffering in two main ways. Firstly, through personal initiative and effort by way of, for instance, courageously facing the situation with a view to overcoming it or by determination and hard work as they work their way out of their predicament. Secondly, it could be at the societal level where a member of the society such as a neighbour or a well-wisher would be the one to save them. These circumstances together with the ways out of such circumstances are consistent with the theories that guided this investigation. The study recommends that more studies be carried out on the plight of orphaned children as depicted in other art forms such as poetry, plays and short stories. Beyond this, the study recommends that more studies to be done in the field besides this particular study that was essentially done in the library.

## YALIYOMO

Mada …………………………………………………………………….. i

Ungamo ……………………………………………………………….. ii

Tabaruku ……………………………………………………………. iii

Shukrani …………………………………………………………….. iv

Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu ……………………………………… v

Vifupisho ……………………………………………………………. vii

Ikisiri …………………………………………………………………. viii

Abstract ……………………………………………………………… ix

Yaliyomo …………………………………………………………….. x

**SURA YA KWANZA ……………………………………………… 1**

1.0 Usuli wa Utafiti ……………………………………………… 1

1.1 Suala la Utafiti ……………………………………………. 6

1.2 Maswali ya Utafiti ………………………………………… 7

1.3 Malengo ya Utafiti ………………………………………… 7

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ……………………………….. 8

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ……………………………….. 9

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ……………………………. 10

1.7 Misingi ya Nadharia ……………………………………… 16

1.7.1 Nadharia ya Vikale ……………………………………….. 16

1.7.2 Nadharia ya Uhalisia ……………………………………… 22

1.8 Mbinu za Utafiti ………………………………………….. 26

1.8.1 Muundo wa Utafiti ……………………………………….. 26

1.8.2 Mahali pa Utafiti ………………………………………………………. 26
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli ……………………………………………............ 27
1.8.4 Ukusanyaji wa Data …………………………………………………… 27
1.8.5 Uchanganuzi wa Data …………………………………………………. 28
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ……………………………………………… 28

**SURA YA PILI: HALI ZINAZOCHANGIA WATOTO KUWA YATIMA 29**

2.1 Utangulizi …………………………………………………………….. 29
2.2 Muhtasari wa Hadithi Teule …………………………………………. 30
2.2.1 Mama wa Kambo (Kisovi, 2005) ……………………………………. 30
2.2.2 Yatima (Wamitila, 2006) ……………………………………………. 32
2.2.3 Mateso ya Johari (Ng'ang'a, 2006) ………………………………….. 34
2.3 Hali Zinazochangia Watoto kuwa Yatima …………………………... 37
2.3.1 Mizozo Katika Familia ………………………………………………. 38
2.3.2 Tabia za Wivu, Chuki na Tamaa …………………………………….. 44
2.3.3 Magonjwa ……………………………………………………………. 48
2.3.4 Mikasa ……………………………………………………………….. 50
2.4 Hitimisho …………………………………………………………….. 52

**SURA YA TATU: CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA WATOTO YATIMA ……………………………………………… 53**

3.1 Utangulizi …………………………………………………………… 53
3.1.1 Dhana ya Haki za Watoto …………………………………………… 53
3.2 Kufanyishwa Kazi Nyingi na Ngumu ………………………………. 55

3.3 Kunyimwa Haki ya Elimu ………………………………………………… 59

3.4 Mtoto Yatima Kukosa Mahitaji ya Kimsingi ……………………….. 62

3.5 Yatima Kutengwa, Kubaguliwa na Kutelekezwa na Jamii …………. 63

3.6 Kutumiwa kwa Mtoto Yatima kama Kitega Uchumi ……………..... 69

3.7 Mtoto Yatima Kuishi katika Mazingira Magumu ………………….. 71

3.8 Hitimisho …………………………………………………………… 81

**SURA YA NNE: KUJIOPOA KWA MTOTO YATIMA KUTOKANA NA CHANGAMOTO ZINAZOMKUMBA ………………. 82**

4.1 Utangulizi …………………………………………………………… 82

4.2 Kujiopoa Kutokana na Kazi Nyingi na Ngumu …………………….. 84

4.3 Kujiopoa Kutokana na Kunyimwa Haki na Uhuru …………………. 88

4.4 Kujiopoa Kutokana na Kutengwa na Kubaguliwa …………………. 96

4.5 Kujiopoa Kutokana na Kutumiwa kama Kitega Uchumi ………….. 102

4.6 Hitimisho …………………………………………………………… 105

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO … 106**

5.1 Muhtasari ……………………………………………………………. 106

5.2 Hitimisho ……………………………………………………………. 109

5.3 Mapendekezo ……………………………………………………….. 110

**MAREJELEO ……………………………………………………………….. 112**

**VIAMBATISHO……………………………………………………………..** **118**

Kiambatisho 1 ………………………………………………………. 118

Kiambatisho 2 ………………………………………………………. 119

Kiambatisho 3 ……………………………………………………. 120

Kiambatisho 4 …………………………………………………… 121

Kiambatisho 5 …………………………………………………… 122

Kiambatisho 6 …………………………………………………… 123

Kiambatisho 7 …………………………………………………… 124

Kiambatisho 8 …………………………………………………… 125

Kiambatisho 9 …………………………………………………… 126

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Usuli wa Utafiti

Utafiti huu umeanza kwa kuangalia dhana ya yatima kiulimwengu. Kulingana na SOS Children's Villages (2016) kuna takriban milioni 140 ya yatima kiulimwengu. Kati ya idadi hii milioni 120 hawaendi shuleni. Hii ni kwa sababu ya changamoto nyingi zinazowakumba watoto yatima. Baadhi ya changamoto hizi ni ukosefu wa rasilimali na ufadhili wa elimu yao. Wengi wao hupatwa na shida ya utapia mlo na hili huongeza idadi ya watoto yatima wanaoaga dunia.

Munawar (2015) anadokeza kuwa baadhi ya nchi ambazo zina idadi kubwa ya mayatima ulimwenguni ni pamoja na Afghanistan, Sudan, Somalia, Iraq, Haiti, Lebanon na Palestine. Baadhi ya nchi hizi zina uzoefu wa vurugu za uraia na kisiasa ambao umeongeza kiwango cha vifo ambavyo vinazidisha idadi ya mayatima.

Suala jingine ambalo limeshughulikiwa katka fasihi kuhusu yatima kiulimwengu ni kiwango cha kuasili mayatima katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Voight & Brown (2013) wanajadili kuwa kiwango cha kimataifa cha kuasili kimepunguka huku idadi ya mayatima ikiongezeka katika sehemu mbalimbali ulimwenguni.

Suala kuu ambalo limeshughulikiwa kuhusu mayatima katika bara la Afrika ni kuwa lina idadi kubwa ya mayatima. Kulingana na Nsagha, et al; (2012) chanzo kikuu cha mayatima katika bara la Afrika ni ukosefu wa kinga mwilini (UKIMWI). Ugonjwa huu

umefanya idadi ya mayatima kuongezeka. Inakisiwa kuwa idadi hii itazidi kuongezeka kama ugonjwa huu hautadhibitiwa.

Changamoto mbalimbali ambazo watoto yatima hukumbana nazo katika bara la Afrika ni pamoja na: kutojua kusoma na kuandika, viwango vya juu zaidi vya umaskini na njaa. Changamoto hizi zimeongeza kiwango cha vifo miongoni mwa mayatima. Masusala haya yamelengwa na waandishi mbalimbali wa Fasihi. Miradi mbalimbali imeanzishwa na watu kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu ili kusaidia mtoto yatima kujiopoa kutokana na changamoto anazokumbana nazo. Aidha mashirika mbalimbali yakiwemo ya kiserikali na kibinafsi yamehusika katika kumwopoa mtoto yatima.

Kulingana na Raptim Humanitarian Travel (2016) kuna mashirika ambayo yako katika mstari wa mbele kuhakikisha kwamba mtoto yatima anapata mahitaji yake ya kimsingi yakiwemo chakula, hifadhi na mavazi. Hii ni kwa sababu watoto yatima mara nyingi hukumbwa na njaa, ukosefu wa mavazi na hifadhi ambavyo huathiri uwezo wao wa kupata elimu na siha njema. Makao ya watoto yatima yamefunguliwa ili yawalinde na kuwatunza yatima. Hata hivyo, makao haya mara nyingi hukosa fedha za kuyaendeleza na hata wafanyakazi.

Fasihi ya Kiswahili imelenga changamoto ambazo watoto yatima hukumbana nazo katika maisha yao. Changamoto hizi ni: ukosefu wa mapenzi, ulinzi, shida za kiuchumi, kuachishwa shule kwa sababu ya ukosefu wa karo, mfadhaiko wa kisaikolojia na ukosefu

wa urithi. Aidha mtoto yatima hujipata katika hatari ya kufa katika ujana wake kwa sababu ya magonjwa na utapia mlo.

Akitafiti kuhusu yatima katika fasihi ya Kiswahili, Wamitila (2008) amezungumzia kuhusu kutengwa kwa yatima. Katika utafiti wake ameeleza kuwa kutengwa humlazimisha mtoto yatima kufanya kila juhudi ili ajiokoe kutokana na hali ngumu au madhila anayopitia. Wakati mwingine huishia kuokolewa na viumbe kama majitu.

Katika utafiti wake kumhusu yatima, Ayieko (1997) ameeleza kwamba watoto yatima huwa na shida mbalimbali kama vile, kutoangaliwa ipasavyo, kutotunzwa na kutopata nasaha waliokuwa wakipewa na wazazi wao. Aidha anaeleza kuwa watoto yatima hujipata na changamoto ya kutopata elimu, lishe bora na afya bora.

Judy (1999) ameelezea kuhusu yatima, jinsi ambavyo huwa na hamu ya kurudi katika hali yake ya hapo awali. Kwa sababu hii anakuwa na msukumo wa kumhimiza kuondoka bila kujali vizuizi ili apate kile ambacho kitamridhisha na kumfanya kuwa mkamilifu. Kulingana na Lukens (1990) na Nikolajeva (2002) wahusika ndio nguzo muhimu katika kuonyesha maana ya hadithi na dhamira ya mwandishi. Wahusika katika fasihi ya watoto hujengwa kwa njia tofauti hivi kwamba inakuwa rahisi kuelewa wahusika kuliko kuelewa binadamu halisi. Wanaendelea kusema kuwa wahusika katika fasihi ya watoto husawiriwa kwa njia ambayo watoto wanaweza kujitambulisha nao na kuwaiga. Katika hadithi nyingi wahusika huwa washindi jambo ambalo humfanya mtoto kujifananisha

nao. Nikolajeva akimnukuu Forstez, anamweleza mhusika bapa kama mhusika ambaye mara nyingi anapewa jina la majazi na mwandishi. Nao wahusika wa kinjozi huwa hawana sifa za kibinadamu wa kawaida, mazingaombwe huchukua nafasi kubwa. Ulimwengu wao unahusisha sifa zinazohusishwa na njozi, nguvu za ajabu zisizo za kawaida na matendo ya kiajabuajabu ambayo ni kinyume na binadamu wa kawaida.

Kwa mujibu wa Mpesha (1995) watoto wana uwezo wa kujinasibisha na wahusika ambao ni watoto na wanaopitia tajriba mbalimbali za maisha kama vile furaha, huzuni, mateso na hata mafanikio. Sutherland (1972) wanasema kuwa wahusika wanafaa kuwa na msimamo thabiti katika fasihi ya watoto na wawe wa kuaminika. Watoto hufurahia wahusika walio na majina wanayoyaelewa na kuyafahamu moja kwa moja, haya ni kulingana na Tucker (1976) anaeleza kuwa, usawiri wa wahusika basi hauna budi kuonyesha sifa zinazohusishwa na umri wa watoto ili kuendeleza wazo kuu ambalo mtoto anaweza kulitambua.

Yatima kulingana na Wamitila (2008) ni mtoto aliyetengwa na jamii kwa sababu ya kufiwa na baba, mama au wazazi wote wawili. Kutengwa huku humlazimisha kufanya kila juhudi kujiokoa yeye mwenyewe katika hali ngumu au huishia kuokolewa na viumbe kama majitu. Kuna aina mbali mbali ya mayatima; waliofiwa na baba, mama au wote wawili. Wale waliofiwa na wazazi wote huitwa yatima kamilifu. Wale waliofiwa na mzazi mmoja ni yatima nusu. Yatima aliyefiwa na mama vile vile huchukuliwa kama yatima kamilifu. Katika jamii asili za kiafrika, mayatima walikuwa wanashughulikiwa na

jamii lakini siku hizi wanatengwa kwa ajili ya mfumo wa ukabaila/ubinafsi na kusambaratika kwa asasi za kijamii. Aidha kuna watoto ambao wana wazazi wote wawili ama mmoja lakini hawawajali. Hata hivyo, kuna chokoraa pia ambao pia waweza kuchukuliwa kama mayatima. Msingi wa kuwa na yatima ni kule kuadilisha umuhimu wa kukuza ujasiri na akili ya kuweza kujinasua kutoka mtego fulani.

Wahusika ni nyenzo kuu ya fasihi kwa sababu wao ndio jira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu (Wamitila, 2008). Uhusika ni kipengele muhimu katika fasihi kwani kufanikiwa ama kupungukiwa kwa lengo la mwandishi hutumia mbinu mbalimbali za uhusika katika kusawiri wahusika katika kazi yake.

Ni kupitia kwa uhusika huu ambapo motifu za yatima katika fasihi ya watoto zitachanganuliwa. Motifu ni dhana au elementi katika fasihi iliyo na kisa kinachotokea mara kwa mara au kujirudiarudia na ambayo inatumika katika kukuza na kuendeleza kazi ya kifasihi au ya sanaa (Daemmrich, 1985) anaeleza kuwa motifu katika masimulizi ina uwezo wa kuendelea kushughulikia mafundisho yaliyotokea zamani kama kitengo kimoja au katika mkusanyiko. Anasema kwamba motifu huathiri masimulizi moja kwa moja kwa kuendeleza kitendo mbele. Motifu ya mama wa kambo inaporejelewa huashiria kwamba mtoto wa kambo aliteswa. Hivyo basi motifu ni chanzo dhabiti cha masimulizi. Motifu ni vikale ambapo mhusika, dhana au muundo kongwe unarudiwarudiwa. Yaweza

kuwa hali ya yatima, vile anavyochukuliwa na walinzi wake na jinsi ambavyo anajiokoa kutokana na watesi wake. Motifu hizi ndizo zinajenga mhusika yatima. Aidha matumizi yake katika hadithi teule za Kiswahili ndio yatakayojenga msingi wa utafiti huu.

Kutokana na utafiti mwingi ambao umefanywa na watafiti kuhusiana na mada hii ya mayatima, suala la yatima kuishi maisha ya mateso lingali linajitokeza katika hadithi nyingi zinazoandikwa zikiwa kama kioo cha jamii. Hii ni dhihirisho kuwa, suala la maisha ya watoto mayatima linaonekana kama ambalo halijapata suluhu. Hivi basi, kuna haja ya utafiti zaidi kuelekezwa kwenye suala hili ili kulichunguza kwa kina suala hili na kulenga kuchangia kutafuta suluhu ya kina.

### 1.1 Suala la Utafiti

Utafiti huu umenuia kuchunguza motifu za yatima katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Mhusika yatima kama kikale ni motifu ambayo hupatikana katika kazi za waandishi wengi katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kutokana na sababu kwamba matumizi ya mhusika yatima katika utunzi wa kazi za fasihi yamerudiwarudiwa katika kazi nyingi na kwa vipindi virefu vya historia. Hali hii hubainika kwa vile fasihi huchota malighafi yake katika maisha halisi. Kwa hivyo, matumizi yake hushadidia ufafanuzi wa uhalisia wa maisha ya binadamu kama yalivyo mahali popote ulimwenguni. Vitabu vilivyoshughulikiwa ni: *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), *Yatima* (Wamitila, 2006) na *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006). Motifu za yatima katika fasihi andishi ya watoto ni suala ambalo halijashughulikiwa kwa uzito wake. Ni suala ambalo linahitaji kufanyiwa

uchunguzi wa kina. Mada hii basi imechaguliwa ili suala hili lipate kuchunguzwa kwa undani. Kwa hivyo, kupitia kwenye vitabu hivi, utafiti huu umelenga kueleza hali zinazochangia watoto kuwa yatima kwa mujibu wa waandishi wa hadithi teule, changamoto zinazowakumba watoto hao yatima na jinsi changamoto hizo zinavyosuluhishwa na watoto yatima.

**1.2 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu umedhamiria kujibu maswali yafuatayo:

1. Ni hali zipi zinazochangia watoto kuwa yatima katika kazi teule?
2. Ni changamoto zipi zinazowakumba watoto yatima katika kazi teule?
3. Je, mtoto yatima hujiopoa vipi kutokana na changamoto hizo?

**1.3 Malengo ya Utafiti**

1. Kubainisha hali ambazo zinachangia watoto kuwa yatima katika kazi teule za fasihi ya watoto.
2. Kuonyesha changamoto zinazowakumba watoto yatima katika hadithi teule.
3. Kuonyesha jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto hizo kwa mujibu wa waandishi wa hadithi teule.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mada kuhusu motifu za yatima katika riwaya za watoto imechaguliwa ili kuonyesha jinsi ambavyo motifu hizi zinavyojitokeza kwenye hadithi teule ili kuelewa hali za kihisia kama vile kusikitisha au huruma kuhusu yatima.

Kutokana na idadi kubwa ya vifo ambavyo hutokea kila siku, kumekuwa na mayatima wengi ambao huachwa bila walezi. Baadhi yao huachwa chini ya ulinzi wa jamaa zao na wengine huwafanyia maovu ya kila aina. Kwa hivyo, kuna haja ya kutathmini namna ambavyo jambo hili limeshughulikiwa na waandishi katika fasihi. Hii itaonyesha ustadi wa waandishi katika utumiaji wa motifu kama kiungo cha usimuliaji katika hadithi za watoto zilizoteuliwa. Pia, jambo hili linapoangaziwa litawasaidia watoto kukabiliana na hali halisi katika jamii zao.

Isitoshe, mada ya utafiti huu imechaguliwa kwa kuzingatia mtazamo wake David (2009) kwamba watoto ni viumbe muhimu sana katika jamii na wanahitaji malezi mema pamoja na ulinzi. Baadhi ya walezi wa yatima hupuuza majukumu yao na kuwaacha yatima kuteseka. Kupitia kwa mada ya watoto yatima, tutapata mafunzo fulani kuhusu hali ya baadaye ya yatima baada ya kuona hali yake ya hapo awali na madhila aliopitia kufikia mahali alipo.

Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa waandishi wa vitabu vya watoto hasa katika kuangazia suala la yatima katika jamii. Wahakiki nao watafaidika kwa sababu utafiti huu

utawapelekea kuelewa vyema tapo hili la fasihi ya watoto. Licha ya hayo, wataweza kuvitambua vile vitabu ambavyo vinawalenga watoto na kuwa na manufaa kwao kama wanajamii na vizazi vya kesho. Aidha, walimu watafaidika na utafiti huu kwani wataweza kung'amua changamoto hizi miongoni mwa wanafunzi wao na kuibua mbinu za kuwasaidia wanapokuwa shuleni. Wakuza mitaala nao watafaidika hasa wakati ambapo wanateua vitabu vya fasihi ya watoto. Wanajamii nao wataweza kupata namna ya kuwasaidia watoto hawa.

### 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kuna wahusika mbalimbali ambao hutumiwa na waandishi kutekeleza majukumu mbalimbali katika kazi ya sanaa. Kupitia kwao tunabainishiwa mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza jinsi motifu za yatima zilivyosawiriwa katika vitabu vitatu vya watoto vya Kiswahili na jinsi vinavyochangia kufafanulia dhamira za waandishi. Vitabu hivi vimeteuliwa kwa kuwa baada ya kuvipitia vilionyesha kuyatimiza malengo ya utafiti huu na pia vina data ya kutosha ambayo inaweza kuchanganuliwa kwa manufaa ya utafiti huu.

Vitabu vyenyewe ni: *Mama wa Kambo* (2005) iliyoandikwa na Kisovi. M. N. *Yatima* (2006) iliyoandikwa na Wamitila K.W. na *Mateso ya Johari* (2006) iliyoandikwa na Ng'ang'a., S.

Vitabu teule vilivyotajwa vimechaguliwa kwa uhakiki na utafiti huu kwa sababu kupitia mapitio yaliyofanywa, vimo miongoni mwa vile vinavyosawiri motifu za yatima katika utunzi wao. Vile vile vimeshughulikia mhusika yatima kama kikale na mbinu ya kuwasilisha ujumbe katika fasihi ya watoto. Vitabu hivi pia, ni miongoni mwa vile ambavyo vimependekezwa na kupitishwa na Taasisi ya Elimu nchini Kenya kwamba visomwe na wanafunzi walio katika darasa la nne hadi la nane. Aidha vitabu hivi vina wahusika wakuu ambao ni yatima, hivyo lengo kuu la waandishi wa vitabu hivi linaweza kufasiriwa kuwa wanaangazia masuala muhimu yanayowakumba watoto yatima katika jamii. Hivyo, vinatarajiwa kutoa data ya kutosheleza mahitaji ya utafiti huu.

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Fasihi ya watoto imeshughulikiwa na wasomi tofautitofauti kwa kutegemea mikabala tofautitofauti. Kuna wale ambao wameshughulikia fasihi kwa ujumla, wengine wameshughulikia suala la yatima na kuna wale walioshughulikia motifu za aina tofauti bila kuzingatia motifu za yatima.

Kahenya (1992) alifanya utafiti kuhusu umuhimu wa vichekesho vya TinTin. Akishughulikia usawiri wa wahusika katika utafiti wake. Kwa mujibu wa mwandishi huyu, usawiri wa mhusika anayefaulu kutatua shida katika fasihi ya watoto anadhihirisha ukweli wa maisha. Ukweli huu ni kuwa kunao uwezekano wa kufaulu katika maisha ya kawaida wanavyokabiliana na madhila mbalimbali. Anaendelea kusema kuwa watoto hujinasibisha na mhusika anayeshinda, hivyo fasihi ile ikawa halisi kwao. Utafiti huu

umenufaika kutokana na uchunguzi wa Kahenya kwa vile ameshughulikia usawiri wa wahusika. Hata hivyo, hadithi alizozingatia Kahenya ni tofauti na zile zinazoshughulikiwa kwenye utafiti huu.

Kulingana na utafiti wa Mpesha (1995) ametoa fasiri ya fasihi ya watoto kwa kuangazia sifa za fasihi hii. Kwa mujibu wa mwandishi huyu, fasihi ya watoto huwa fupi. Kwamba watoto hupendelea fasihi chochezi na inayoonyesha hisia. Ni fasihi ambayo huhusisha kuzungumza kwa wingi kuliko maelezo. Mhusika mkuu huwa mtoto ambaye matendo yake yanampa msomaji matumaini. Lugha yake hueleweka kwa watoto na ploti huwa na mpangilio mahususi. Aidha sifa nyingine anayoelezea muhimu ni kuwa hadithi za watoto huwa za kifantasia (zinazoeleza matukio yaliyokiuka mantiki) na za kijasira (ambazo wahusika huonyesha ujasiri katika kukabiliana na hali ngumu zinazowakumba). Baadhi ya sifa ambazo amezungumzia ni muhimu kwa utafiti huu.

Tomison (1996) akitafiti kuhusu uhusiano kati ya dhuluma kwa watoto na madawa ya kulevya, anaonyesha kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya mambo haya mawili. Anatambua vyanzo mbalimbali vya dhuluma kama vile tabia za kibinafsi, matatizo ya kinyumbani na mambo mengine ya kijamii. Utafiti wake ulitambua aina mbalimbali za dhuluma kama vile: kutowatunza watoto kabisa, mauaji na matumizi ya nguvu iliyopita kiasi. Utafiti huu umenufaika kutokana na utafiti wa Tomison kwa upande wa nadharia kwani anaangazia uhalisi wa mambo katika jamii.

Kwa mujibu wa Ayieko (1997) watoto wanaofiwa na wazazi wao huzidiwa na shida mbalimbali kama vile kutoangaliwa ipasavyo, kutotunzwa na kutopata nasaha waliokuwa wakipewa na wazazi wao. Vile vile anasema kuwa yatima hupokonywa fursa ya kuwa na nyumba na mashamba. Kutokana na haya anasema kuwa yatima hujipata na changamoto ya kutopata elimu, lishe bora na afya bora. Utafiti wa Ayieko unaufaa utafiti huu kwa vile ameangazia madhila ambayo yatima hupitia baada ya kufa kwa wazazi wake. Hata hivyo, utafiti wake Ayieko (1997) unatofautiana na wangu kwa kuwa Ayieko aliufanya utafiti wake kule nyanjani ilihali utafiti wangu umelenga kuchanganua suala hili kama lilivyosawiriwa kupitia kwa hadithi za watoto.

Hadithi zinazohusu yatima ni tofauti katika viwango fulani na hufanana katika viwango vingine (Melanie, 1999) anasema kuwa, kuna ruwaza fulani katika ngano za watoto ambazo zimebadilishwa na kutumiwa katika masimulizi ya kubuni ya watoto. Anaeleza kuwa yatima kwa undani sana husimamia hisia na uchungu wetu sote hivyo basi mhusika huyu huendelea kuweko katika fasihi ya watoto. Mhusika yatima ataendelea kutuashiria hadi siku ambayo sote tutaacha kuhisi uchungu wa kutengwa. Matumizi ya elementi kutoka kwa ngano kuhusu yatima katika fasihi huonyesha kina ambacho mhusika huyu anatoa mwangwi. Uchunguzi wa Melanie uliufaa utafiti huu kwa vile ameshughulikia yatima kama kikale.

Akitafiti kuhusu yatima kama kikale cha ukamilifu Judy (1999) amechunguza yatima na jinsi ambavyo anakuwa na hamu ya kurudia hali yake ya hapo awali. Anaeleza kuwa

yatima huwa na ule msukumo au sauti ya ndani ambayo humhimiza kuondoka bila kujali vizuizi na kuenda ili apate kile ambacho kitamridhisha na kumfanya mkamilifu. Kazi yake imechangia katika utafiti huu kwa upande wa nadharia. Tofauti na utafiti huu, yeye amejikita katika msukumo wa ndani wa yatima wa kutaka kuwa mkamilifu huku utafiti wangu unachunguza hata hali za nje zinazomsukuma yatima kutaka kuwa mkamilifu.

Tafiti nyingi zilizoshughulikia watoto yatima si za kifasihi bali ni za taaluma nyingine. Tafiti za Sengendo (1997), Snicket (1999) na Nyambedha, na wengine (2003) zilifanywa kuhusu mhusika yatima lakini tafiti walizoshughulikia si za kifasihi bali ni za taaluma ya Sosiolojia. Hata hivyo tafiti zao zimeufaa utafiti huu kwa kule kuangazia watoto yatima na madhila wanayopitia baada ya wazazi wao kuaga. Tofauti na utafiti huu wao wamejikita katika taaluma nyingine isiyo ya kifasihi. Walitafiti kwa mtazamo wa Kisosiolojia. Ni vizuri pia kuweza kulichunguza suala hili kwa kwa mitazamo ya taaluma nyingine kama ninavyolichunguza hapa kifasihi.

Akizungumza kuhusu riwaya za Maillu, Odhiambo (2004) anasema kuwa katika riwaya zake ameshughulikia changamoto zinazomkumba yatima wa jinsia ya kike. Amejikita katika kubainisha madhila anayopitia mtoto wa kike ambaye ni yatima. Anampa mtoto nafasi ya kuwa fanani, yaani mtoto mwenyewe anaitamba hadithi yake. Mtazamo huu unamfanya mtoto kuielewa hadithi barabara kwani anayeitamba ni mdhulumiwa mwenyewe. Uamuzi anaoufanya unakuwa funzo kwa watoto wengine wanaosoma

hadithi yake. Utafiti wa Odhiambo uliufaa utafiti huu kwa vile ameshughulikia mhusika yatima. Tofauti na utafiti huu yeye ameshughulikia yatima wa jinsia ya kike.

Akitafiti kuhusu masuala ibuka katika hadithi za watoto, Karanja (2005) ameangazia maudhui katika kazi za watoto ambayo ni kiini cha hadithi. Anasema kuwa maudhui huleta uhalisia kwa jinsi ambavyo watoto wanaweza kujinasibisha na masuala anayozungumzia. Hadithi hizi ni kama kioo kinachomulika uhalisia katika dunia ya leo. Kazi ya Karanja imekuwa njia bora ya kuboresha mada hii kwa sababu ya kuangazia uhalisia katika jamii ya leo. Tofauti na utafiti huu yeye ameshughulikia masuala-ibuka yanayopatikana katika hadithi za watoto.

Winding (2007) ametafiti kuhusu kupotea na kupatikana kwa shujaa yatima katika visasili na ngano za vichimba kazi. Anaeleza kuwa watoto wanaokataliwa, kutengwa au kutupwa na jamaa zao mara nyingi hupokonywa urithi na mwishowe wakakuzwa na watu wengine au hata wanyama au ndege wa mwituni. Yatima hawa huwa mashujaa na huibuka kuwa malkia au wafalme. Utafiti huu umenufaika kutokana na uchunguzi wa Winding kwa vile ambavo anazungumzia mhusika yatima ambaye anashughulikiwa katika utafiti huu. Tofauti na utafiti huu, yeye anazungumzia kupotea na kupatikana kwa yatima shujaa ilhali utafiti huu unaangazia motifu za yatima.

Katika utafiti wake kuhusu dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili (Kavuria, 2008) amezungumzia dhuluma dhidi ya watoto kwa jumla. Amechunguza vile

maudhui ya dhuluma dhidi ya watoto yanavyosawiriwa kwa kubainisha aina za dhuluma. Pia anabainisha sababu za utendaji wa dhuluma hizo, asasi zinazotekeleza dhuluma hizo, pamoja na athari kwa maisha ya mtoto. Kazi ya Kavuria itaufaa utafiti huu tukiangazia changamoto ambazo mtoto yatima hukumbana nazo. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa sababu yeye ameshughulikia watoto kwa jumla ilhali utafiti huu umejikita katika mtoto yatima.

Kulingana na Hugborg (2010) akitafiti kuhusu uhusiano wa kifamilia katika Harrypotter. Anasema kwamba kinyume na mashujaa wa kifasihi ambao huenda katika ulimwengu ili wapate mahali pao katika ulimwengu, yatima huenda katika ulimwengu kutafuta familia anayoweza kujiunga nayo na imukubali. Alisema haya akidhamiria kuelewa jinsi ambavyo watu wa familia ya yatima humchukua baada ya kufa kwa wazazi wake. Anasema kuwa mara nyingi watu wa jamaa yake hawamkubali. Katika utafiti wake ametumia nadharia ya vikale ili kutambulisha vielelezo vya familia vinavyomzingira yatima. Katika kufanya hivi amefasili sifa bainifu za kila kikale kuhusiana na hadithi za vichimbakazi, sanaa ya jadi na dini. Utafiti wa Hugborg utaufaa utafiti huu kwa upande wa nadharia. Tofauti na utafiti huu, utafiti wake unashughulikia uhusiano wa kifamilia hasa vielelezo vya kifamilia vinavyomzunguka yatima huku utafiti wangu unachukua mtazamo mpana kwa kuangazia msukumo wa ndani nan je ya yatima kutaka kuwa mkamilifu na pia kulichunguza suala hili kwa misingi na nadharia za fasihi. Haya yote haijashughulikiwa na watafiki waliotangulia.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu umetumia nadharia changamano. Nadharia ya vikale iliyoasisiwa na Northrop Frye (1950-1954) na nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa na Georg Hegel na kuendelezwa na Lukacs (1972) na Larkin (1977). Sababu kuu ya kutumia nadharia changamano ni kwamba nadharia ya vikale haingeweza kutekeleza kila jukumu la utafiti huu pekee yake. Lazima ingefidiwa na nadharia ya Uhalisia ili kudhibiti utafiti katika mwelekeo na malengo ambayo utafiti huu umekusudia. Nadharia ya vikale imeelezea picha zinazojirudia au zinazotokea mara kwa mara katika kazi ya sanaa. Nayo nadharia ya Uhalisia imeelezea jinsi matukio yanayoshughulikiwa na waandishi yanavyodhibitika katika ulimwengu halisi. Kwa hivyo nadharia hizi zinachangiana pale ambapo nadharia moja ingeshindwa kutekeleza kutoa mwongozo tosha katika kulitafiti suala kuu la utafiti huu.

### 1.7.1 Nadharia ya Vikale

Kulingana na Frye (1957), Plaks (1976) na Wafula (1999) kikale ni taswira kongwe inayojitokeza mara kwa mara katika kazi ya kifasihi. Kikale huwasilisha dhana fulani kongwe inayopatikana katika jamii inayozungumziwa. Vile vile kikale kulingana na Wamitila (2003) hurejelea mhusika, motifu, ishara au taashira ambayo imekuwepo tangu zamani na inayojitokeza mara nyingi katika fasihi.

Kwa mujibu wa McMahon na wengine (1990) dhana ya vikale inahusishwa na mwanasaikolojia wa Uswizi anayejulikana kama Carl Gustav Jung (1875-1961). Wakiwa

na mwana-anthropolojia James Frazer, wanaeleza kuwa Jung wakati mmoja aliota kuhusu miili ya wafu iliyokuwa ndani ya majeneza. Baada ya kisa hiki, Jung aliamua kuchunguza visasili vya jamii mbalimbali kisha kuona sifa zinazofanana na ambazo hujitokeza katika fasihi hizo. Katika uchunguzi wake kuhusu visasili, ilibainika kwamba katika staarabu zote (kongwe na mpya) kulikuwa na hadithi zenye taswira ya mashujaa wa ajabu. Pia, kulikuwa na dhana ya "mama" ambaye ni mwenye nguvu na anayewatunza wanadamu, hasa "mama ardhi" anayewapatia chakula na ulinzi. Ugunduzi huu, haswa dhana au taswira shujaa imekuzwa zaidi na waandishi wengine kama Campbell (2004). Pia katika uchunguzi wake, dhana ya miungu ilijirudia katika hadithi zote, kutokana an ugunduzi huu, Jung aliweza kuhitimisha kwamba "Ung'amuzi bwete" ni 'kisima' cha imani za vikale na za kidini ambazo hushika usukani wa tabia na mienendo ya binadamu.

Kulingana na Jung, dhana hizi ambazo zimepokezwa kutoka kizazi hadi kizazi zinapatikana katika jamii na ustaarabu wa nyakati mbalimbali. Sifa bia zinazojidhihirisha katika wanadamu ni matokeo ya nguvu za vikale ambavyo hukaa katika sehemu ya akili ya binadamu ambayo aliipa jina la ung'amuzi bwete jumuishi. Sehemu hii hurithiwa na kila binadamu. Binadamu basi huongozwa na imani ambazo zimerithiwa kutoka kwa visasili. Mawazo hayo hupatikana katika kizazi chote cha binadamu ulimwenguni kote katika nyakati na vizazi mbalimbali. Mawazo haya ya kimsingi Jung aliyaita vikale.

Kwa mujibu wa Jung ruwaza za vikale zimo ndani ya ung'amuzi bwete jumuishi na huhusisha kumbukumbu za jamii mbalimbali, matukio na uhusiano wa tangu zama za kale. Uhakiki wa vikale unahoji kuwa kuna ishara, taswira, wahusika na motifu za pamoja ambazo hudokeza mwitikio sawa na binadamu wote. Jung aliamini kuwa vikale ni nguvu za asili ambazo zina utendakazi wa lazima katika uumbaji wa ulimwengu na katika akili ya mwanadamu.

Kisanaa nadharia ya vikale iliasisiwa na mhakiki kutoka Canada anayeitwa Northrop Frye kati ya miaka ya 1950 na 1954 katika chuo kikuu cha Princeton kupitia kwa mihadhara ya umma. Kinyume na Jung, Frye aliangalia vikale kimuundo.

Kulingana na Plaks (1976), Frye alichukua mhimili wa kimsingi wa uelewaji wa ishara za kisanaa kuwa na uhusiano wa kitamaduni na kijamii. Katika uelewaji huo, masharti au sheria zinazokubalika huwekewa maigizo ili kufanya ubunifu wao wa kisanaa kuwezekana. Anasema kuwa kuna hazina kubwa ya muundo, motifu, taashira na wahusika katika vikale ambavyo haiwezi kuwa miliki ya mwandishi mmoja. Waandishi wengine huchota sheria na mbinu hizi kutoka kwa vikale na kuzitumia katika utunzi wao. Northrop anaelezea kuwa kikale ni ishara au taashira ambayo huzua taswira inayojirudiarudia katika kazi ya sanaa kiasi kwamba inatambuliwa kama kiungo cha ujuzi wa mtunzi wa kazi fulani.

Fasihi inastahili kusisitiza usawiri wa maisha kama yalivyo (Frye, 1957). Anaendelea kueleza kwamba misingi ya miundo ya fasihi inafaa kutolewa kutoka kwa uhakiki wa vikale ambao ndio huzingatia fasihi kwa ujumla wake. Namna ambavyo visasili vinakuwa vichache ndivyo kiwango kinachosadifu uhalisia wa maisha kama yalivyo kinavyofikiwa. Kwa hivyo uwasilishaji wa sanaa kwa utaratibu wa visakale na hadithi kuhusu miungu ambapo wahusika wana nguvu zaidi za utendaji ndio mifano ya fasihi ya kidhahania inayokubalika.

Uchunguzi wa vikale huanza kwa ulimwengu wa visasili, sanaa ya kidhahania yenye dhamira za kubuni kinyume na upokezaji wa kaida za utunzi wa kisanaa zilizozoelewa. Visasili katika usimulizi wake huigiza matendo yanayokaribia mahitaji ya binadamu. Katika usimulizi, visasili huigiza matendo yanayokaribia mahitaji ya binadamu. Miungu hutamani wanawake warembo, hupenda vita, huliwaza na kusaidia binadamu akiwa katika matatizo au hutazama tu kutoka kwa umbali wa maisha yao yanayodumu. Kisasili ni sawa na ulimwengu au dunia inayoangaliwa kama uwanja wa vitendo ikizingatiwa kwamba maana au mfano wa kazi ya sanaa ni muundo wa kitaswira unaosababisha dhana fulani. Ulimwengu basi katika taswira ya visasili unawakilishwa kijazanda ambapo kila kitu kina uwezo wa kufanana na kingine. Frye anaeleza kwamba uhalisia huchunguza jinsi ambavyo kitu kinafanana na kile kinachojulikana. Wakati kile ambacho kimeandikwa kinafanana na kile ambacho kinajulikana, kinakuwa sanaa ya tashbihi inayokusudiwa. Jinsi uhalisia ulivyo sanaa ya tashbihi inayokusudiwa, ndivyo kisasili

kilivyo sanaa ya utambuzi wa jazanda inayokusudiwa. Katika visasili, misingi ya miundo ya kazi ya sanaa kama matumizi ya motifu pia hutambuliwa na kutengwa.

Ili visasili vikubalike, mlinganisho wa sifa za wahusika na matendo yao, mandhari au tabia ya vitu vinavyowazunguka lazima ufanyike ili kutoa wazi ule muundo wake wa kijazanda. Mlinganisho huu unaitwa majazi na Frye. Majazi ni mbinu ya kisanaa ya kuwapa wahusika majina yanayochukuana na sifa au matendo yao. Majina kama haya huweza kuchukuana na sifa za mahali au mandhari zinazowazunguka wahusika wenye majina hayo. Nadharia ya vikale pia huchunguza matumizi ya mbinu ya majazi.

Frye anafasiri mtazamo wa Jung kuhusu maana ya vikale unaoongozwa na ung'amuzi bwete kwa njia tofauti. Kulingana na Frye, maana hutokana na sheria ambazo zinakubalika pamoja na umatini wa kazi yenyewe ya sanaa. Mtazamo wake ni tofauti na imani ya Jung ambapo yeye anaangalia katika misingi ya kisaikolojia. Kikale kwa Frye ni njia ya uwasilishi wa ujumbe. Kwa hivyo, kikale ni ishara ya kisanaa au ishara nyingine ambazo hutumika kwa kurudiwarudiwa katika kazi ya kifasihi na kuifanya kukubaliwa kuwa mizani ya kupimia kazi nyingine zinazotungwa baadaye. Mtazamo huu wa Frye umeweza kuungwa mkono na wasomi wengine wakiwemo Guerin (2005), Esterhammer na Angela (2005), Walker (2002) na Russel (2000).

Mihimili ya Nadharia ya Vikale kwa mujibu wa Northrop Frye (1957) ambayo imetufaa kwa utafiti huu ni ifuatayo:

1. Misingi ya miundo ya fasihi inanyambuliwa kwa vikale ambavyo huchukulia fasihi kwa lengo la upana wake. Misingi hii ina uhusiano mkubwa na visasili na imani linganishi ya watu.Mhimili huu ulituwezesha kumwelewa mhusika yatima kama kikale
2. Sanaa ya ubunifu inasonga kutoka kwa visasili na vikale na kwenda kwa uigaji, jazanda na istiari ambazo zinafikia kiwango cha uhalisia au uwakilishi unaofanana na hali halisi ya maisha.Mhimili huu ulituwezesha kuelewa hali zinazochangia watoto kuwa yatima.
3. Uhalisia huanza kwa uchunguzi wa visasili na vikale. Vikale ni maigizo ya vitendo vinavyokaribiana au vilivyo katika mipaka ya matamanio asilia ya walimwengu. Miungu hufurahia wanawake warembo, hupigana wao kwa wao kwa nguvu nyingi, huliwaza na kumsaidia mwanadamu anayedhulumiwa au humtazama akiteseka bila kuingilia kati. Mhimili huu ulitusaidia kubaini matukio yanayoandamana na motifu za yatima katika kazi teule, kama vile kuelewa changamoto zinazosawiriwa ambazo ni masuala ya Uhalisia wa kijamii. Vile vile ulitusaidia kuelewa jinsi ambavyo yatima anajiopoa kutokana na changamoto hizo.
4. Katika mfumo wa kiuhalisia ujumbe na usawiri wa kazi ya sanaa unazingatiwa badala ya kuzingatia muundo wake. Hivyo dunia huwasilishwa kama mahali penye machukizo, umaskini, mazingaombwe, usiiri, ugandamizaji, mateso na kuchanganyikiwa. Mhimili huu ulituwezesha kuelewa jinsi ambavyo yatima hukabiliana na changamoto anazokumbana nazo katika dunia.

Mihimili iliyotajwa ilitufaa katika utafiti wetu kwa sababu imedhihirika ya kwamba matumizi ya motifu za yatima katika hadithi za Kiswahili ni mbinu ambayo imekuwepo katika visakale na visasili vingi ambavyo hupatikana katika jamii mbalimbali ulimwenguni na huchotwa tu na watunzi katika vipindi mbali mbali katika utunzi wao.

### 1.7.2 Nadharia ya Uhalisia

Uhalisia ni mwelekeo unaokakatiza usanii wa matukio katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Kwa mujibu wa Larkin (1977) neno uhalisia lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko ufaransa katika mwaka wa 1850 ili kueleza kazi za sanaa zinazojikita katika kusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa kuwa. Kama nadharia ya Uhakiki, Uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Kusawiriwa na kueleweka kwa uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kutokana na haya maelezo inawezekana kusema kuwa kila kizazi huwa na uhalisia wake. Kazi ya Uhalisia iliwekewa msingi na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake cha *Aesthetik*. Matumizi ya neno hili yalipendekezwa na Hegel ili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambao una mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa wazi wazi na hali aliyomo. Kwa kiasi kikubwa, uchunguzi wa utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisi hivi kwamba ni vigumu kuzungumzia riwaya bila ya kurejelea mawazo au dhana inayohusishwa ya uhalisia.

Nadharia ya Uhalisia husisitiza usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake. Katika mtazamo wa uhalisia, mambo yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika katika ulimwengu halisi. Mwanasanaa katika misingi ya kihalisia anapaswa kuelewa ulimwengu wake kama kitu changamano na ambacho kinaweza kubadilika. Mwandishi wa kiuhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida na vilevile huyaakisi maisha katika ngazi za kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Ni muhimu kuelewa kuwa mchango mkubwa na nadharia ya uhalisia ni kuchora maisha kama yalivyo.

Uhalisia unapinga aina yoyote ya majaribio. Mwandishi analazimika kuuteua mtazamo wa kisimulizi ambao utamwezesha kuyawasilisha maisha kwa usahihi. Mwanasanaa aidha anatarajiwa kutoa picha za wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii. Msisitizo uliopo ni kuukaribia ukweli uliopo katika jamii inayohusika.

Kwa mujibu wa Larkin (1977) wanauhalisia waliamini kuwa kusudi la mwandishi kwa jamii ni kuwarejesha watu katika ulimwengu wao wa kawaida, na kuwa ulimwengu ambao mwandishi atauumba lazima uwe halisi.

Nadharia ya Uhalisia ilianza kuhusishwa katika fasihi kwa sababu waasisi wa nadharia hii waliona kwamba kunao uhusiano mkubwa kati ya kazi za sanaa na mawazo ya msanii kuhusu mazingira anamojipata. Hivyo basi madhumuni ya kutumia nadharia hii ni kuihakiki kazi ya msanii ili kuona ni kwa kiasi gani anadhihirisha uhalisia na umuhimu wake katika fasihi ya watoto (Lukacs, 1972). Mwandishi katika uhalisia hana budi kutoa

picha ya jamii na hivyo kuwa kama kurunzi ya jamii. Jukumu la msanii linapaswa kuwa la ukweli na vilevile liweze kudhihirisha ukweli huu ili kujaribu kuufikia uhalisia. Mwandishi anastahili kutumia kipawa chake kusawiri wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii ya wakati wake kwa sababu mazingira haya huwa ya uhalisi unaoaminika.

Huck (1976), anasema kwamba kitabu kinachohusisha uhalisia huwaelekeza watoto katika utu kwa sababu huwa kinadhihirisha ukweli ulioko katika maisha. Watoto hupata kuelewa dhiki za binadamu na pia mahusiano ya kibinadamu. Watoto huweza kuvutiwa na kuelewa kazi inayoeleza mambo wanayoweza kujihusisha nayo katika uhalisi wa maisha yao.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Dhima ya mwandishi anayetumia nadharia ya uhalisia ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Mwelekeo huu umeungwa mkono na waandishi na watafiti na hata wasomi wengine wakiwemo Lynch-Brown na Tomlison (2008), Norton na Norton (2011) na Russell (2012), Ni kutokana na uhalisia ambapo tunapata dhana ya fasihi kuwa 'ni kioo cha jamii'.

Nadharia ya uhalisia inajumuisha mihimili ifuatayo:

**Mihimili**

1. Msanii huandika kuhusu maisha yalivyo akiwa anaathiriwa na jamii pamoja na mazingira yake. Kazi katika misingi ya kihalisia inaangazia maisha katika ngazi zote za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kijamii na kadhalika. Mhimili huu umetuwezesha kuelewa usawiri wa yatima, changamoto anazokumbana nazo na jinsi ambavyo anapata suluhisho.
2. Wahusika katika kazi za kihalisia husawiriwa wakiwa wa kawaida na wakiwakilisha jamii zao. Ukweli unafaa uonekane katika kuwaumba wahusika wa kawaida katika mandhari ya kawaida. Msanii wa kihalisia anawapata wahusika wake katika jamii yake iliyo ya kawaida na inayojulikana. Mhimili huu umetusaidia kuelewa mhusika mkuu, yatima, na wahusika wengine wanaomjenga.
3. Lugha katika kazi ya kihalisia huwa ni ya kawaida na wahusika wanaitumia kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu. Mhimili huu umetuwezesha kuelewa changamoto zinazomkumba yatima na njia ambazo anatumia ili kujiopoa na changamoto hizo.
4. Mandhari na matukio yanafaa kuwa yale yanayoweza kuonekana, kujulikana au kuwezekana. Maudhui na matukio kwa kiasi kikubwa yanatakiwa kulingana na yale ya jamii inayorejelewa. Mhimili huu umetuwezesha kuelewa jinsi ambavyo yatima hukumbana na hali yake ngumu katika ulimwengu halisi.
5. Msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Yeye huchunguza mabadiliko ambayo hutokea katika kipindi fulani cha historia na namna ambavyo mabadiliko hayo husababisha hali mbalimbali. Hivyo basi,

mwandishi wa kihalisia hutilia maanani mabadiliko ambayo yanatokea ili aweze kuwasawiri wahusika wake. Mhimili huu umetusaidia kubainisha hali ambazo zinachangia watoto kuwa yatima.

6. Mhusika wa kisaikolojia hutenda kulingana na hali zilizomzunguka.

Mihimili iliyotajwa imesaidia kuelewa ya kwamba watunzi hushughulikia masuala yanayotendeka katika jamii na ubunifu wao huakisi kwa kiwango kikubwa yale yanayotendeka katika ulimwengu halisi.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu umezingatia muundo wa kimaelezo. Muundo huu huchunguza hali ya mambo ilivyo katika mazingira fulani na mielekeo ya watu kuhusu hali na mambo mbalimbali. Vile vile hudhihirisha picha ya kitu kilivyo kwa njia sahihi.

### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu umefanywa kupitia kwa usomaji katika maktaba ya kisasa ya chuo kikuu cha Kenyatta (Kenyatta University Post-Modern Library). Kwani ulihusu usomaji wa hadithi mahususi. Tafiti za awali zimesomwa na mtafiti ili kuelewa kuhusu nadharia, mbinu za ukusanyaji data, uwasilishaji na uchanganuzi wa matokeo ya utafiti. Data ilitokana na usomaji wa hadithi teule za watoto ambazo zilichanganuliwa kwa mwongozo wa nadharia hizi amabazo tumezitaja hapa.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli inayolengwa katika utafiti huu ni vitabu teule vya hadithi za watoto. Kwa hivyo, sampuli ambayo imetumiwa imeteuliwa kwa kuzingatia mbinu kusudio. Hii ni kwa sababu utafiti unalenga hadithi mahususi za Kiswahili ambazo zimeteuliwa kwa kuzingatia data inayohitajika. Hadithi zenyewe ni: *Alitoroka Kwao* (2001) *Yatima* (2006) na *Mateso ya Johari* (2007). Hadithi hizi zimemsawiri yatima na zinalenga watoto kati ya umri wa miaka tisa hadi kumi na tatu. Mtafiti amesoma hadithi hizi kwa kina ili kupata data faafu kwa utafiti wake. Katika kuzichagua hadithi hizi, nilizingatia kuwa ziwe ni hadithi za watoto na mwaka wa uchapisho wa kitabu ili kwamba hadithi zisiwe zimechapishwa zaidi ya miaka kumi iliyopita. Pia nilizingatia kuwa hadithi iwe inasimulia mazingira ya mtoto wa kiafrika na pia isiwe imeshatumiwa na mtafiti au watafiti wengine kwa kuchunguza mada ninayochunguza kwenye utafiti huu.

### 1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Data imekusanywa kutoka kwa hadithi tatu teule za watoto. Utafiti huu umedhamiria kuchunguza hadithi hizi ili kupata data ya kuchanganuliwa. Data hii ni usawiri wa mateso ya mtoto yatima na njia anazotumia kujaribu kujiopoa. Maktabani, mtafiti amesoma maandishi ambayo yanagusia motifu za yatima na kupata data faafu kwa utafiti wake na maandishi. Aidha, amepata kuyafahamu mambo muhimu na misinngi ya motifu hizi na kuyaandika katika daftari lake ili kumwezesha kukamilisha utafiti wake kwa kupata data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti huu.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data imekusanywa kwa kuzingatia usawiri wa mateso ya mtoto yatima na njia anazotumia kujaribu kujiopoa na kuyaandika kwenye daftari. Hali hizi zimechanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa mwongozo wa nadharia teule. Kwa mwongozo wa nadharia hizi, mtafiti amebainisha hali zinazochangia watoto kuwa yatima katika hadithi teule za watoto. Pia ameonyesha changamoto zinazowakumba watoto yatima katika hadithi teule za watoto zilizosomwa. Hali kadhalika amechunguza na kuonyesha jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto anazokumbana nazo. Uchanganuzi wa data ambazo ni motifu za yatima katika hadithi teule umeshirikisha pia matumizi ya nadharia changamano ya vikale na uhalisia katika kuchanganua usawiri wa mateso ya mtoto yatima na njia za kujiopoa.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data zote zilizokusanywa na kuchanganuliwa ikiwemo usawiri wa mateso ya mtoto yatima na njia anazotumia kujiopoa zimewasilishwa kwa njia ya maelezo na nukuu za vifungu vinavyotoa picha halisi ya hali inayochanganuliwa. Maelezo haya yamezingatia ufafanuzi wa motifu za yatima katika hadithi teule za watoto. Hususan, maelezo yamebainisha hali zinazochangia watoto kuwa yatima. Pia, changamoto zinazowakumba watoto yatima katika hadithi zimewekwa bayana. Isitoshe, mbinu ambazo mtoto yatima hutumia kujiopoa katika hadithi husika zimeangaziwa. Uwasilishaji wa data umefanywa kwa kuongozwa na malengo na maswali ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia teule.

# SURA YA PILI

# 2.0 HALI ZINAZOCHANGIA WATOTO KUWA YATIMA

## 2.1 Utangulizi

Watoto yatima ni watoto walio chini ya miaka kumi na minane na ambao wamefiwa na baba, mama au wazazi wote wawili (baba na mama) Kisia (1996). Kwa njia nyingine, hawa ni watoto walio chini ya miaka kumi na minane, ambao wanakosa au wanaelekea kukosa matunzo na ulinzi wa kutosha. Katika hadithi zote teule tatu; *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), *Yatima* (Wamitila, 2006) na *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) zinazoangaziwa katika utafiti huu, suala la maisha ya yatima linajitokeza waziwazi. Mara nyingi, jina hili la yatima hurejelea sana kwa kuzungumzia watoto wasioweza kuyakimu mahitaji yao au kujishughulikia kwa vyovyote vile; kando na wale wanaopoteza wazazi wakiwa wanaweza kujitosheleza mahitaji yao. Inakisiwa kuwa idadi ya watoto yatima ulimwenguni inazidi kuongezeka kwa kiasi kikubwa sana, Hollingsworth (2013). Hata hivyo, hali hii ya uyatima huchangiwa na hali mbalimbali katika maisha ya wahusika wakuu ambao ni watoto yatima. Kwa hivyo, sura hii inalenga kubainisha hali zinazochangia watoto kuwa yatima katika hadithi tatu zilizoteuliwa katika fasihi ya watoto. Ili kueleweka vyema, sura hii inaanza kwa kutoa muhtasari wa hadithi hizi moja baada ya nyingine. Baadaye itaangazia uchanganuzi wa hali zinazochangia watoto kuwa yatima.

## 2.2 Muhtasari wa Hadithi Teule

### *2.2.1 Mama wa Kambo ( Kisovi, 2005)*

Katika hadithi hii, Konelia, kijana mwenye sifa nzuri, alimwoa Maua, msichana mrembo sana kisha baadaye wakajaliwa mtoto msichana na kumpa jina Kalaa. Maua aliaga dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi. Hali ya maisha ya upweke na huzuni ilionekana kumzidi Konelia. Jirani yake ambaye pia ni rafikiye; Taadhima, kwa kushirikiana na mkewe, walimshauri na kumsaidia Konelia kumwoa Kitete, msichana mrembo sana, ila tu ana wivu. Kitete alianza kumtesa sana mwanawe wa kambo haswa wakati ambapo Konelia alikuwa ameenda kufanya kazi maeneo ya mbali na nyumbani. Baada ya muda, Kitete alijaliwa kupata mtoto wa kike pia, wakampa jina Pendo.

Kitete aliendelea kumtesa Kalaa huku majirani wakiwa wameshangazwa na hali hii. La kushangaza ni kwamba hakuna aliyetaka kuingilia kati. Hata hivyo, Konelia aliweza kuona tofauti fulani kati ya Kalaa na Pendo akizingatia hali zao za afya. Alipomuuliza mkewe kiini cha tofauti hizi, Kitete alimgeukia kumlaumu Kalaa na kumshangaa yeye ni msichana wa aina gani asiyependa kujilinda vyema. Mateso ya Kalaa yalizidi. Siku moja akiwa katika hali ya kuwaza na kuwazua alisikia sauti ikimuagiza kuwa kila anapokuwa na njaa aimbe wimbo fulani. Alipoimba, aliona meza mbele yake ikiwa imeandaliwa kila aina ya chakula. Kupitia kwa njia hii, Kalaa aliweza kujiepusha na shida ya njaa.

Siku nyingine mbiu ya mgambo ilisikika ikilia ikiashiria kuwa kuna vijana wageni kwa mfalme. Kitete alimtayarisha mwanawe Pendo aende ahudhurie tamasha hizo kwa

mfalme huku akimwamrisha Kalaa abaki nyumbani. Alisema kuwa vijana hao hawawezi kumwangalia mtu ovyo kama yeye. Kwa mara ya pili, akiwa analia kwa uchungu wa kuzuiliwa asiweze kuwashuhudia wageni hao, alisikia sauti ikimshauri ajipe moyo na aende kwenye tamasha hizo. Hapo basi akashtukia kujipata amezungukwa na vitu vingi pamoja na mavazi mazuri sana. Alivaa na kuonekana mrembo zaidi na kwenda kwenye sherehe. Alipoanza kucheza, vijana wale walianza kumsongea na hapo ndipo Kitete alionekana akimuashiria Pendo ajongee naye pia wakacheze na hao wageni.

Baadaye vijana hao walimtembelea Pendo kwa kuleta posa. Vijana hao waligundua kuwa huko pia ndiko atokako Kalaa. Mmoja wa vijana hao alitaka mkonowe Kalaa katika ndoa. Kitete akamuumbua na kumhujumu ili kupunguza uwezekano huo wa Kalaa kujipatia mchumba. Alifanya haya ili Kalaa daima aishi kuwa mtumishi wake. Mara alitokea kijana aliyevaa matambara na mwenye jina Baraka, akitaka mkonowe Kalaa katika ndoa. Kwa haraka sana na ushawishi mwingi kwa babake Kalaa, Kitete aliunga mkono posa hiyo. Kalaa naye hususan kwa kuzingatia mateso aliyokuwa akipata, alimkubali kijana huyo licha ya umaskini wake.

Punde si punde, kulitokea Bi Kizee mmoja na habari kuwa huyo aliyemwoa Pendo alikuwa jitu na hivi sasa ameshammeza. Kitete alisumbuka nafsi yake sana. Alilia kwa kwikwi na kite. Alijiangusha chini na kujigaragaza. Ilikuwa ni huzuni isiyo kadirika kumpoteza Pendo. Kalaa naye aliwasili siku iliyofuata kwenye msafara wa magari mengi. Msafara huo ulikuwa na watu waliokuwa wakipiga ngoma na kuimba kwa furaha.

Kumbe kijana yule aliyevaa matambara na kuonekana maskini hakuwa maskini bali alikuwa mwana wa mfalme wa mji mmoja wa ughaibuni. Kalaa na mwana wa mfalme waliishi kwa furaha na kubarikiwa kwa kizazi na mali.

### *2.2.2 Yatima (Wamitila, 2006)*

Wazazi wa Katiwa, ambaye ni mhusika mkuu, walifariki na kumwacha akiwa mchanga kisha akachukuliwa na shangaziye Juliana aliyeishi jijini Bambo. Shangazi Juliana alipopata kazi kule Kima, aliamua kumpeleka Katiwa kijijini Masira ili aishi na babu yake. Sababu ya uamuzi huu ni kuwa nyumba waliyokuwa wakienda kuishi kule Kima haingewatosha wote. Ingewatosha tu yeye na wanawe wawili , Kevin na Maria. Makaribisho ya babu hayakuwa mazuri sana, aliwafukuza akidai kwamba yeye si mlezi wa watoto. Hata hivyo shangazi alimuacha Katiwa kwa babu yake na kumueleza kuwa lazima angeyapenda maisha ya pale mlimani kwa babu. Ulikuwa wakati mgumu kwa Katiwa kwa sababu babu hakutaka hata kuongea naye. Siku ya kwanza Katiwa alilala kwenye kibanda cha mbuzi na kondoo. Hata hivyo baada ya muda, babu alianza kubadilika polepole na kuwa mchangamfu kwake Katiwa. Katiwa naye alianza kuandamana na Mule kupeleka mbuzi na kondoo wa babu malishoni.

Siku moja shangazi Juliana alimkujia Katiwa ili warudi naye Bambo. Babu hakufurahia jambo hilo. Katiwa pia alikubali kuandamana na shangazi yake shingo upande, kwani hakuwa tayari kumwacha babu pekee yake.Walienda hadi kwa mwanamke fulani na huko ndiko Katiwa alikokuwa amekusudiwa kuishi. Kulikuwa kwa mama mmoja ambaye

alionekana kutompenda Katiwa. Mwanamke huyu alianza kumtesa Katiwa sana kwa njia ya kumpa kazi nyingi huku akimlimbikizia matusi. Katiwa alipomuuliza kwa nini haendi shule kama watoto wengine alicheka kwa sauti kubwa na kumwambia kuwa watoto wasichana kama yeye huwa hawaendi shule. Akaongezea kuwa watoto hulipiwa pesa na wazazi wao na yeye hana wazazi. Katiwa hakupelekwa shule na kwa sababu hii, watoto wa huyu mama walimdharau na kumsimanga kwa sababu yeye haendi shule. Watoto hao wangefanya makosa kisha waseme kuwa ni Katiwa aliyeyafanya makosa hayo. Hii ilifanya agombezwe na mama yao.

Siku moja Katiwa alienda kununua mkate na maziwa. Ikatokea kuwa bidhaa hizo hazikuwa dukani kwa wakati huo. Lakini aliporudi kumwambia Mam' Peter, mama huyo alimfukuza na kumtaka aketi huko nje kwenye baridi na manyunyu ya mvua hadi atakapozinunua bidhaa hizo.

Katiwa alirudi madukani kutafuta mkate na maziwa, kwa bahati mbaya alianguka kwenye shimo la maji na kupoteza pesa alizokuwa amepewa. Alipofika kwa Mam' Peter, hakutaka kusikia maelezo yake. Alimpiga sana akidai kuwa Katiwa anamdanganya. Katiwa alishangaa sana kwa kuwa watu waliomwona akipigwa hawakuja kumsaidia. Siku iliyofuata alikuwa na maumivu mwili mzima. Jicho lilikuwa limevimba na hangeweza kuinua mikono. Hata hivyo, alilazimika kufanya kazi zote kama kawaida.

Katika tukio lingine Peter aliiba pesa za mamake kisha akamsingizia Katiwa kuwa ndiye aliyeziiba. Kwa sababu hiyo, Mam' Peter alimpiga kama gunia hadi akamfukuza aende alale nje usiku huo wa giza. Alizichukua nguo zake na kumtupia nje. Katiwa alihangaika hadi kuishia kulala katika kijumba cha mlinzi. Siku iliyofuata alichukuliwa na Bettina, mwanamke mmoja aliyemwonea huruma. Bettina alikuwa mwanachama wa kikundi kilichochunguza jinsi watoto walivyoteswa na kusumbuka katika miji mikubwa. Siku iliyofuata, Bettina aliyejulikana kama Mama Rita, alimchukua Katiwa na kumpeleka kwa shangazi yake. Baada ya kumkosa shangazi yake, walirudi kwa Mama Rita. Alikaa huko kwa muda fulani kisha Mama Rita akafanya utafiti kujua kiliko kijiji cha Masira ili amrejeshe Katiwa kwa babu yake. Alipofaulu kujua kiliko kijiji hicho, waliondoka moja kwa moja hadi huko na kuwakuta babu na nyanya ambao walimpokea vizuri sana. Waliamua kuwa Katiwa hangeenda kusomea mjini, bali wao wangeuza mbuzi na kondoo walio nao ili kumlipia karo. Hapo basi ilibidi Katiwa abaki Masira na kuanza shughuli za masomo. Aliendelea kuishi na babu na nyanya hadi walipoaga dunia.

### *2.2.3 Mateso ya Johari (Ng'ang'a, 2006)*

Katika harakati za kumpata Mtemi (Mfalme) mpya wa kijiji cha Mangulu, ilitambuliwa kuwa Kido aliyetarajiwa kuurithi utemi alikuwa hajaoa. Wazee washauri wa Mtemi walishauriana kisha wakampendekeza Debora kama chaguo lao. Baada ya kumshawishi Kido kumkubali msichana huyu mwenye sifa nzuri ila tu umaskini wa familia yao, sherehe za harusi zilifanyika. Baadaye zikafuatwa na sherehe za kumtawaza Kido kuwa Mtemi mpya. Baada ya miaka mitano, wawili hawa hawakuwa wamejaliwa mtoto. Hata

hivyo daktari alikuwa amewashauri kuwa bado wangempata mtoto. Kido alishawishiwa na rafiki yake aliyeitwa Kimau kwamba anabaki nyuma kama mkia. Alimtaka aoe mke mwingine ambaye angemzalia watoto. Lakini washauri wa Kido walipinga uamuzi huo na kumhimiza aache papara na afuate ushauri wa daktari. Kido alishawishika kuoa mke wa pili, Zebeli, ili amzalie mrithi wake kinyume na ushauri wa washauri wa Mtemi.

Hata hivyo, Zebeli alipata mtoto wa kwanza aliyekuwa wa kike, na akampa jina Wakesho. Baada ya miaka minne, akampata mtoto wa pili ambaye vile vile alitokea kuwa wa kike. Jambo hili lilimkera sana Kido hadi kuishia kumtelekeza Zebeli. Alianza kuurejesha uhusiano wake na Debora ambaye alikuwa hajakata tamaa ya kupata mtoto. Baada ya miezi tisa, Debora alijifungua mtoto wa kiume akampa jina la Johari. Zebeli alikereka sana na tukio hilo hadi akapanga njama ya kumuua Johari. Baadaye, Zebeli alimwendea Debora kwa mchawi. Mchawi huyo alimpa Zebeli sumu ambayo aliienda kumwekea Debora kwenye chakula na kusababisha kifo chake. Tukio hili lilimwacha Johari kama yatima. Jambo hili lilimpa Kido mshtuko mkubwa ambao uliifanya hali yake kudhoofika sana.Mwishowe aliaga dunia baada ya miezi miwili na nusu iliyofuatia kifo cha Debora. Johari akiwa ameachwa kwa nyumba ya Zebeli, aliyapitia mateso si haba. Alifanyishwa kazi nyingi kama mtumwa na mwishowe akaachishwa masomo yake akiwa katika darasa la saba. Johari alijaribu kusihi mamake wa kambo amuache aendelee na masomo lakini maombi yake yaliambulia patupu. Masomo ya shule ya msingi yalitolewa bure, lakini Zebeli alikataa kata kata Johari aendelee na masomo.Uamuzi huu ulimhuzunisha sana Johari kwa sababu aliyapenda masomo sana. Kwa vile Johari

alikuwa na umri mdogo sana, ingebidi wanakijiji hiki kungoja kwa muda mrefu sana ndipo waweze kumrithisha Johari mamlaka. Kwa sababu hii, waliamua kuugeuza mfumo wa uongozi ili wanakijiji waweze kumchagua yeyote miongoni mwao kuwa Mtemi.

Akiwa huko shambani alikokuwa akifanya kazi, Johari alianza kuhusiana kwa karibu sana na Mzee Magufuli ambaye alimshauri na hata kumsaidia nauli ya kwenda mjini ili ajaribu bahati yake kimaisha. Jambo hili lilikuwa kinyume na fikra na mipango ya Zebeli. Alipofika mjini alipokelewa vyema na Ezekia, mwanawe mzee Magufuli na wakaanza kuishi pamoja akijifunza kazi ya Umakanika. Johari alifanya bidii na kuwa na maelewano mazuri kazini na wenzake kama vile Okoko hadi kufanywa kuwa msimamizi wa gereji. Johari alimwaandikia Wakesho, ambaye ni dadake wa kambo, barua ya kuwajulia hali. Lakini, kwa kushirikiana na mamake, walimjibu kwa kumkataa kama mmoja wa familia yao. Hatua hii ya kukataliwa na hata kuitwa kwa jina la mamake ilimtonesha Johari kidonda cha moyo. Ezekia alimsikitikia sana Johari na kumpa ushauri kwamba aanze kuweka akiba ili aweze kujisimamia. Ijapokuwa alizihifadhi pesa, raha yake ilikuwa kuungana na jamaa yake. Kwa hivyo Johari aliamua kuwatembelea wakiwa na Mzee Magufuli ili awapatanishe. Walipofika, Zebeli aliwafukuza. Johari alirudi mjini kwa huzuni na kuendelea na kazi yake huku akijiwekea mshahara kwenye akaunti kama hazina.

Siku moja, akiwa kwenye shamrashamra zake mjini alikutana na Waigwa, mmoja wa wanakijiji, ambaye alimweleza habari za mkasa uliokuwa umeikumba familia ya Zebeli. Katika kisa hicho, nyumba yote ilishika moto na kuchomeka pasi na kunusurisha

chochote. Tukio hili liliwapelekea Zebeli na wanawe kuanza kulala kwenye kibanda cha kutengenezwa kwa makaratasi. Johari alishauriana na Ezekia kisha wakanunua vitu vyote vya ujenzi wa nyumba na kuvipakia kwenye lori na kufika kijijini. Walipowasili, walipokelewa na Zebeli huku akiomba msamaha kwa Johari na Mzee Magufuli. Wanakijiji waliungana mikono na kujenga nyumba nyingine iliyotokea kuwa nzuri zaidi katika kijiji hicho. Johari aliahidi kuwarejesha Wakesho na dadake shuleni.

Mwanzoni mwa sura hii, ilielezwa kuwa mtoto yatima ni yule aliyefiwa na baba au mama au wazazi wote wawili.Kwa kuyazingatia maelezo haya, kinachodhihirika ni kuwa hali ya uyatima inachangiwa na kifo cha wazazi wa mtoto yeyote yule. Kwa kuchukua mwelekeo huu, itakuwa na maana kuwa, kwa kusema kwamba kinachochangia watoto kuwa yatima ni kifo. Basi lengo la sura hii litakuwa limefikiwa.

### 2.3 Hali Zinazochangia Watoto kuwa Yatima

Katika utangulizi wa kazi hii, watoto yatima wamejadiliwa na kujitokeza kuwa watoto walio katika hali ngumu ya kimaisha. Mbali na haya, idadi yao inaonekana ikizidi kuongezeka. Hii inaonyesha kuwa, sababu ya hali zinazochangia watoto kuwa yatima zinazidi kuongezeka. Hali ya watoto nayo pia inazidi kuzorota. Kama ilivyojitokeza hapo awali, mojawapo ya malengo ya utafiti huu ni kuzibaini sababu hizi. Kwa hivyo, sehemu hii inaangazia hali mbalimbali zinazochangia watoto kuwa yatima katika hadithi hizi tatu teule. Hali hizi zimejadiliwa katika mada tofauti tofauti kama ifuatavyo;

### 2.3.1 Mizozo Katika Familia

Maelewano katika familia huchangia hisia za usalama katika maisha ya mtu yeyote. Lakini wakati mizozo ya kifamilia inapotokea, huwa ni tishio kubwa sana kwa usalama na udhabiti wa familia hiyo. Iwe kuwa mizozo hii itatokana na jamaa katika familia yoyote ile au nje ya familia, wanafamilia hiyo huwa wanakumbana na hisia zisizokuwa nzuri pamoja na madhara fulani. Ni kweli kwamba mizozo hii isiposuluhishwa, huwa inapelekea familia husika kuvunjika hasa wanafamilia hii wasipotafuta msaada wa kuleta suluhu. Mizozo hutokea wakati wanafamilia wanakuwa na maoni na hisia tofauti kuhusiana na mambo tofauti. Wakati mwingine, mizozo katika familia hutokea kwa sababu ya ukosefu wa maelewano miongoni mwa jamaa na kupelekea wengine katika familia hizo kufikia tamati na uamuzi usio mwafaka. Miongoni mwa sababu ambazo zimezungumziwa na Canary & Canary (2013), kwamba ndizo chanzo cha mizozo katika familia ni pamoja na; ukosefu wa maelewano juu ya rasilimali za familia, tofauti kati ya mitazamo kati ya wazazi na watoto wao, ubishi miongoni mwa watoto katika familia na kadhalika.

Mizozo inayotokea kwa njia ya kukosa kuelewana katika familia imesawiriwa kama mojawapo wa vyanzo mbalimbali vya vifo vya wazazi. Hili ni jambo linalowafanya watoto kuwa yatima. Kulingana na Canary & Canary, (2013), mizozo ya kifamilia husababisha vifo vya wazazi na kuwaacha watoto mayatima. Hali hii husababisha mazingira ambapo mahitaji ya watoto hawa hayashughulikiwi wala kutimizwa. Hii hupelekea watoto hawa kuacha familia zao na kuenda mbali ili kutafuta makazi mazuri.

Kwa mfano katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) hadithi inaanza kwa maelezo kuwa wazazi wa Katiwa walifariki alipokuwa mtoto mchanga na kumwacha akiwa yatima (Wamitila, 2006:1). Baadaye, mwishoni mwa hadithi babu yake Katiwa anamsimulia Katiwa kisa cha kufariki kwa wazazi wake. Hapo inafahamika kuwa babu yake alikosana na mwanawe pamoja na mkewe. Basi akawafukuza nyumbani kwa upanga akiwa amejawa na hasira. Wawili hawa walienda kujificha bondeni hususan ndani ya pango ili kutoroka babu aliyekuwa amejawa na hasira. Vilevile kutokana na mvua kubwa iliyokuwa inanyesha, wawili hao walitaka kujikinga mvua. Na kutokana na mvua hiyo nyingi, ardhi haikuwa imara na hivyo basi ikaporomoka na kuwafukia humo pangoni.

> …Nilikosana na wazazi wako. Huu ulikuwa wakati wa mvua ya masika ambapo niliwafukuza nyumbani kwa panga. Walikwenda kujificha huko bondeni ambapo waliangukiwa na ardhi na kufukiwa huko chini (Wamitila, 2006:84).

Mzozo katika familia ya mzee huyu ambao haukusuluhishwa kwa njia mwafaka ulipelekea Katiwa kuwapoteza wazazi wake. Hata hivyo, mzozo huu unapata msukumo kutokana na ukosefu wa utu kama inavyodhihirika kwa kuzingatia tabia ya babu yake Katiwa. Anamfukuza mwanawe pamoja na mkewe kwa upanga na kuwaelekeza walikokutana na kifo chao. Vilevile, mzozo huu ulipata msukumo mwingine kutoka kwa hali ya ukosefu wa mawasiliano bora kati ya baba na mwanawe. Pia hali ya kukosa kujidhibiti kihisia kama vile hasira inaweza kusababisha madhara. Babu hakuweza kujidhibiti kihisia, hasira zake ziliweza kusababisha kifo cha wazazi wake Katiwa.

Mambo haya yote yanajidhihirisha kwenye funzo analotuambia kuwa alijifunza babu kuwa 'kinachomjenga binadamu ni utu na tabia…' (Wamitila, 2006:84).

Jambo linalojitokeza kwenye wosia huu wa babu ni kuwa tabia huashiria utu. Hivyo basi, tabia zinaweza kuijenga au kuibomoa jamii na kuleta madhara kama kuwatumbukiza watoto katika hali ya uyatima. Ama kwa kweli, hata kama Mzee huyu aliye babu yake Katiwa alighadhabishwa sana na mwanawe, halikuwa jambo la busara yeye kumfukuza mwanawe pamoja na mkewe kwa hasira kwa nia ya kutaka kuwaua, bali angetafuta suluhu mwafaka. Lakini kwa kukosa kufanya hivyo, alikuwa ameshapungukiwa na utu na hivyo basi akasababisha maafa zaidi.

Kwa kurejelea misingi ya nadharia ya Uhalisia kama mojawapo ya nadharia zinazoelekeza hadithi hii ya *Yatima,* kifo kinachompelekea Katiwa kuwa yatima kimesawiriwa kwa njia ambayo inaambatana na hali mambo yanavyotendeka katika ulimwengu halisi. Kwa mfano, maisha katika ulimwengu wa sasa yamekumbwa na visa vingi vya ukosefu wa utu. Aidha tabia zisizoambatana na hali ya maelewano na mawasiliano bora katika jamii. Mara kwa mara, imeshuhudiwa na hata kufahamishwa kupitia kwa vyombo vya habari kuwa mizozo ya aina mbali mbali imesababisha vifo katika familia. Mnamo mwezi wa Januari, 17 mwaka wa 2018 gazeti la 'Daily Nation' lilikuwa na ripoti kuhusu mwanamume mmoja kwa jina Patrick Ndiritu ambaye alimuua bibi yake, kisha akaenda kwa chumba cha watoto wao na kuwaua kinyama kwa kutumia kifaa butu. Baadaye, alijimwagilia petroli na kujichoma. Moto ulikuwa mwingi na

ukateketeza nyumba yao. Tukio hili lilitendeka katika mtaa wa Malaba kaunti ya Juja. Walioshuhudia kisa hicho walisema kwamba kilikuwa cha kusikitisha na kuogofya mno. Vile vile katika gazeti la 'Standard' Novemba, 30 mwaka wa 2016, kisa kingine kiliripotiwa katika Kaunti ya Kisumu, mwanamume mmoja alimuua bibi yake kisha akajiua. Ilisemekana kwamba vifo hivi vilisababishwa na ugomvi wa kifamilia. Kisa kama hiki huacha watoto bila wazazi wao wote na hivyo wanabaki yatima.

Kulingana na Canary & Canary (2013) kumekuwa na visa vingi vya kuzozana katika familia ambavyo vimesababisha watoto kutokuwa na mazingira mazuri ya kuishi. Mizozo mingi imesababisha ndoa nyingi kuvunjika. Hali hii huibua mazingira ambayo mahitaji ya mtoto hayatimizwi. Wakati mwingine watoto huwa mayatima na inawabidi kuondoka ili watafute mahali salama pa kuishi. Matukio yanayohusiana na mizozo yameangaziwa katika hadithi ya *Yatima* (Wamtila, 2006). Ni dhahiri kuwa tukio kama hili la babu yake Katiwa kuwafukuza wanawe nyumbani kwa upanga, liliwafanya wakimbilie usalama wao katika pango ambalo lilisababisha vifo vyao. Pango liliporomoka na ardhi ikawafukia humo ndani walimokuwa wamejikinga mvua. Hili ni tukio ambalo kwa kweli linamrejesha msomaji katika ulimwengu wake wa kawaida.

Mizozo huchangia pakubwa katika hali ya uyatima; husababisha hali ya kutokuwa na usalama kwa watoto. Ni kweli kuwa katika familia huweza kusababisha kifo kwa wazazi wote na kuwafanya watoto yatima. Wakati mwingine husababisha mzazi mmoja kufungwa jela na kubaki na mmoja wa kuwahudumia.

Kulingana na nadharia ya vikale, Frye (2001), mizozo ni vikale vya zamani katika familia. Hakuna familia iwayo yote ambayo haina mizozo. Ugomvi, migogoro na mapigano ni vikale. Vikale hivi huibua mizozo ambayo huweza kusababisha vifo na kuleta uyatima isiposhughulikiwa ipasavyo. Vikale hivi vimekuwepo tangu zamani. Mzozo uliokuwepo kati ya babu na wanawe katika hadithi ya *Yatima (Wamitila, 2006)* ni kikale ambacho kinadhihirika katika familia ya kisasa.

Suala hili la mizozo linadhihirika wazi pia katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) kupitia kwa tabia ya Zebeli, mke wa pili wa Mtemi Kido. Zebeli ni mama ambaye hakumtakia mke mwenzake mazuri. Anapoolewa kwa ajili ya Mtemi kupata mtoto atakayemrithi, alianzisha fitina na hadaa kuhusu Debora. Wakawa wanazozana kila mara na Debora. Debora anauliza, "Kwa nini wanitilia fitina, mbona usijishugulishe na mambo yako? " (Ng'ang'a, 2006:17).

Fitina huleta mizozo na kutoelewana katika familia. Zebeli alifanya hivi akijua kwamba yeye ndiye atakayepata mtoto wa kumrithi Kido. Lakini anaishia kupata watoto wawili wa kike. Sheria ya Kijiji cha Mangulu hairuhusu mtoto wa kike kumrithi babake na hivyo ndivyo Zebeli anavyoanza kuhofia kupoteza bahati aliyokuwa akiidhamiria. Debora ambaye ni mke mwenza wake Zebeli anapojaliwa mtoto wa kiume, Zebeli anajihisi kupoteza bahati. Mtemi Kido naye akawa kila mara anasema, "Debora na mwanawe wana tabia njema , tofauti na Zebeli ambaye huwakaripia watoto kama kichaa."

(Ng'ang'a, 2006:23). Matamshi kama haya kutoka kwa Mtemi Kido ambaye tangu mwanzo alijua Debora na Zebeli hawakuelewana hayakufaa. Kwani hapo ndipo Zebeli alipanga njama ya kumwangamiza Debora na kumpelekea Johari kuwa yatima.

Vile vile tabia ya kukosa subira katika maisha ilimpelekea Mtemi Kido kufanya kila juhudi, ikiwemo kuukaidi ushauri wa wazee washauri wa Mtemi na kumwoa Zebeli kama mke wa pili. Kido hakujali hata ushauri wa daktari kuwa angepata mtoto na Debora. Ni kwa kupitia njia hii ambapo Zebeli alisababisha vifo vya wazazi wote wawili wa Johari na kumtosa kwenye uyatima. Mizozo inapokuwa katika familia, uangalifu katika matendo na matamshi ni muhimu. Kido kama Mtemi alileta majanga katika familia yake kwa kutenda kinyume na alivyoshauriwa. Johari anateseka mikononi mwa Zebeli baada ya kifo cha mamake, na hii ni kwa sababu ya Kido kuukaidi ushauri ilivyoelezwa hapa na Mzee Hekima, aliyekuwa mshauri wake;

> "Huwezi kumuoa mke mwingine vivi hivi. Ushaniambia jinsi daktari alivyowashauri. Mbona unayapapia mambo nanyi bado ni vijana? Acha papara, fuata ushauri wa daktari, ushauri huo usipofaulu, utachukua hatua nyingine." (Ng'ang'a, 2006:15)

Kido aliukaidi ushahidi wa Mzee Hekima, alishindwa kuelewa kwa nini mshauri wake alipinga maoni yake. Basi aliamua kufanya alivyotaka huku akipuuza washauri wake. Anaeleza kuwa;

> "Nitatenda ninavyotaka. Hawa wazee hujifanya wanajua kila kitu. Mzee Hekima akicheza nitamuondoa kama mmoja wa washauri wangu na nimteue mwingine." (Ng'ang'a, 2006:15)

Kwa mujibu wa nadharia ya Kikale, kifo ni picha kongwe inayojirudia katika maisha ya mwanadamu, na kinapotokea mtu akiwa mdogo huwa yatima. Kwa hivyo kifo na uyatima vimefungamanishwa kama kikale kinachoashiria kutokuwepo kwa mzazi , mtegemezi au mtu wa kumsaidia. Hivi ndivyo yanavyokuwa maisha ya Johari baada ya kifo cha mamake mzazi.

### 2.3.2 Tabia za Wivu, Chuki na Tamaa

Wivu pamoja na tamaa ni mienendo ambayo imesawiriwa kama chanzo mojawapo wa vyanzo vya vifo vinavyowapelekea watoto kuwa yatima. Kuna matukio kadhaa, hasa katika hadithi ya *Mateso ya Johari* yanayodhihirisha hali hii. Tukio la kwanza ni wakati ambapo Zebeli aligundua kwamba Debora ni mjamzito. Hali hii ya ujauzito ilimfanya Zebeli asumbuliwe sana na wivu. Alijua kwamba Debora angejifungua mtoto wa kiume kabla yake, basi mtoto wa Debora ndiye angerithi kigoda cha Mtemi. Mimba ya Debora ilizua chuki, wivu na mawazo mabaya kwa mke mwenziwe.

Tukio lingine lililozidisha chuki na wivu ni wakati ambapo Debora alijifungua. La mno, alijifungua mtoto wa kiume aliyepewa jina Johari. Wanakijiji walifurahia kuzaliwa kwa mtoto ambaye angerithi kigoda cha Mtemi. Hili likamchukiza Zebeli jinsi inavyoelezwa hapa;

> … Nyumbani Zebeli aliwachukia Johari na mamake mwisho wa kuchukia. Zebeli alichukizwa sana na namna wanakijiji walivyowapenda Debora na mwanawe. (Ng’ang’a, 2006:23).

Ni dhahiri kuwa Kido alimpenda Debora na mwanawe. Hata hivyo, pendo lake Kido kwake Debora halikuwa la mapendeleo bali lilitokana na tabia zao nzuri zinazoambatana na maadili ya jamii kama inavyojitokeza katika usemi wake Kido wa kila mara kama inavyoelezwa hapa:

> Debora na mwanawe wana tabia njema tofauti na Zebeli ambaye huwakaripia watoto kama kichaa (Ng'ang'a, 2006:23).

Zaidi ya hapo, Debora amechorwa kama mhusika asiyekuwa na ila yoyote:

> … Debora alikuwa mwanamke mnyenyekevu na mwenye maadili mema… (Ng'ang'a, 2006:23).

Kwa sababu hii, Zebeli naye hakuwapenda Debora na mwanawe hata akawa anawaza na kuwazua kila mara jinsi angewaangamiza kufikia kiwango kuwa;

> …aliazimia kufaulisha unyama wake kwa Debora (Ng'ang'a, 2006:23).

Akiwa na azma hiyo, Zebeli aliweza kutumia rasilimali alizokuwa nazo akamwendea Debora kwa mchawi kwa jina Mponda, aliyejulikana sana kijijini Mangulu. Mchawi huyu alimweleza aina mbili za dawa; ile ya kumfanya kuwa kichaa na nyingine ya kumuua. Hapo basi Zebeli akaufanya uamuzi wake:

> … bora mwanamke yule afe. Anaweza kuwa kichaa nikimpa dawa ya aina ya kwanza kisha baadaye awe na akili timamu… (Ng'ang'a, 2006:23).

Hata ingawa dawa hii ilikuwa ya bei ya juu, Zebeli aliamua kuilipia hiyo pasipo na kujali gharama yake. Na kwa hadaa ya kuwa alitaka kuomba Debora msamaha ili wasafiane mioyo, Zebeli alijifanya kurudisha urafiki na Debora ili aweze kumpata kwa urahisi. Basi alimualika jioni ya siku hiyo ili aende kwake kwa chakula cha jioni. Hapo ndipo Zebeli

alimpa sumu Debora na kusababisha kifo kilichompata siku chache zilizofuata. Kifo hiki cha Debora ndicho kilichokuwa chanzo cha maisha yake Johari kama yatima.

Johari anakuwa yatima kwa sababu ya wivu wa Zebeli. Zebeli anamuonea wivu Debora kwa kupata mtoto wa kiume. Mtoto ambaye angekuwa mrithi wa kiti cha utemi. Mwandishi anasema kuwa;

> "Zebeli aliwachukia Johari na mamake mwisho wa kuchukia. Chuki ya Zebeli ilifikia kilele alipogundua kwamba mke mwenziwe alikuwa mjamzito tena. Hali hii mpya ilimchukiza sana." (Ng'ang'a, 2006:23)

Aliwachukia kwa sababu walipendwa na wana kijiji na zaidi walipendwa na mtemi Kido. Inaeleweka kuwa chuki ya Zebeli ilifikia kilele alipogundua ya kwamba mke mwenziwe alikuwa mja mzito tena.

Hali hii mpya ya Debora kuwa mja mzito tena ilimtia Zebeli wivu na chuki ambapo aliamua kumuua Debora. Hali ya wivu na chuki yaweza kuleta madhara katika familia. Familia ya mtemi Kido inakumbwa na pigo la kifo cha Debora kwa sababu ya wivu na chuki ya Zebeli.

Hali hii ilimwathiri sana Mtemi Kido na baada ya miezi miwili na nusu iliyofuatia kifo cha mkewe Debora, inaelezwa kuwa: hali hiyo ilimsukuma Mtemi Kido hadi kaburini. (Ng'ang'a, 2006:34). Hali na tukio hili linamtosa Johari katika maisha ya uyatima. Aidha, katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005) mwandishi anaeleza kuwa Kitete aliibua tabia yake ya wivu kwa Kalaa. Alijifanya mwema mbele za watu, lakini kwa

ndani alimwazia maovu Kalaa (Kisovi, 2005:27). Kwa sababu ya wivu na chuki, Kitete alimtendea Kalaa uovu bila huruma. Alimfanya kuwa mtumishi wake wa nyumbani. Aidha alimtenga Kalaa na Pendo na kumkanya kucheza naye. Vile vile, alimnyima mavazi mazuri na chakula. Kalaa aliteseka sana mikononi mwa Kitete hadi akakonda. Haya yote yanadhihirisha jinsi Kitete alivyomchukia Kalaa.

Katika hadithi ya *Nyanya* ambayo ni hadithi ndani ya hadithi ya Yatima (Wamitila, 2006) inaelezwa kuwa baada ya kifo cha mamake Mwilu, Mwilu aliachwa chini ya ulinzi na uangalizi wa mamake wa kambo (mamake Mwila). Mamake Mwila hakumpenda Mwilu kwa sababu alikuwa na sura nzuri na mwerevu kumshinda mwanawe Mwila. Kwa sababu ya chuki alipanga kumwangamiza Mwilu. Alimzika angali hai na kulijaza shimo alimoanguka Mwilu kwa mchanga. Hiki ni kitendo cha unyama na ukosefu wa utu. Mama huyu anaamua kumfukia Mwilu bila huruma kwa sababu ya wivu na chuki. Mwila hakuwa mwerevu kama Mwilu, jambo hili lilimpa msukumo wa kumtendea Mwilu unyama huu. Hata hivyo, ukweli unapobainika mama Mwila anashtuka kumwona Mwilu na anapojaribu kutoroka anatumbukia kwenye shimo la choo na kufariki. Kifo cha mama Mwila kinakuwa chanzo cha maisha ya Mwila kama yatima. Ni wazi kuwa Mwila anakuwa yatima kwa sababu ya wivu na chuki.

Kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya uhalisia, visa vya wake wenza kutendeana mambo kwa misingi ya kuoneana wivu vimeweza kukithiri sana katika jamii. Gazeti la 'The Star' Oktoba 31 mwaka wa 2016 liliripoti kwamba mwanamke anayejulikana kwa

jina Pamela Wetangula alimuua mke mwenza Lydia Wamalwa kwa kumdunga kisu. Pamela alipelekwa Kortini ili ajibu mashtaka ya kitendo hicho. Tukio hili lilifanyika karibu na eneo walikokuwa wanamjengea Lydia nyumba. Mume wao alikuwa amemwalika Lydia ili aje kuona maendeleo ya ujenzi wa nyumba hiyo. Iliripotiwa kwamba Lydia alikuwa amesafiri kutoka kijiji cha Kibabii alikokuwa anaishi na watoto.

Kisa hiki kinadhihirisha vile tabia ya wivu na chuki inaweza kusababisha kifo na kupelekea watoto kuwa yatima. Pamela alimuua Lydia aliyekuwa mke mwenza wake kwa sababu ya wivu kuhusu nyumba aliyokuwa akijengewa na mume wake. Wivu, chuki na tamaa ni tabia ambazo zimeweza kusababisha maafa mengi katika jamii au hata familia mbalimbali. Inapozidi, ndugu, jamaa au marafiki wameweza kuuana kwa njia mbalimbali. Njia hizi ni pamoja na kufanyiana uchawi, ugaidi au hata kupigana hadi kuuana. Sababu ya haya yote ni kuchukiana, kuoneana wivu au tamaa ya kurithi mali au cheo fulani kazini. Tabia hizi zote zikiwemo tamaa, chuki na wivu, zimo katika ulimwengu halisi. Hizi ni tabia zinazomfanya mhusika kujitakia kila kitu. Hivi ndivyo hali ilivyo kwenye hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) na hivyo basi, inaambatana na mihimili ya nadharia ya uhalisia.

### 2.3.3 Magonjwa

Magonjwa ni mojawapo ya hali ambazo zimesawiriwa kama zile ambazo zinachangia watoto kuwa yatima hasa kwa kusababisha vifo vya wazazi. Katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), imeelezwa kuwa baada ya kumzaa Kalaa, Maua (mamake Kalaa)

alikumbwa na ugonjwa wa ghafla. Konelia na jamaa yake walifanya kila juhudi kumfikisha hospitalini lakini akaaga dunia baada ya siku tatu. Kufuatia kifo cha Maua, Kalaa alijipata yatima akiwa na miaka minne. Magonjwa husababisha vifo vya wazazi na hivyo huleta ongezeko la yatima katika nchi.

Ulimwengu wa leo umejaa visa vya magonjwa yanayotokea kwa ghafla kama vile homa ya chikungunya. Ugonjwa huu husambazwa na mbu na huandamana na maumivu makali ya viungo vya mwili. Mbali na homa ya chuikungunya, kuna magonjwa mengine kama: Ebola, Ukimwi, Saratani ya aina mbalimbali na hata kirusi cha Zuka. Kirusi cha Zuka kimeweza kuzuka ulimwenguni hivi majuzi. Kwa mujibu wa Tadele & Kloos (2013) inakisiwa kuwa kote duniani kunao watoto milioni kumi na saba nukta nane walio chini ya miaka kumi na nane ambao ni yatima. Wamekuwa yatima kutokana na kuwapoteza wazazi wao kupitia janga la Ukimwi.

Constatino & Ganga (2013), wanasema kuwa magonjwa yameleta vifo vingi katika sehemu mbalimbali za Afrika ya kati na magharibi. Kwa sababu hii, katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005) mwandishi anaeleza vile kifo cha Maua aliyekuwa mamake kilimfanya Kalaa kuwa Yatima, namna inavyosawiri kifo kilichochangia hali ya Kalaa kuwa yatima. Hivi basi, hadithi hii imejikita katika misingi ya nadharia ya uhalisia kwani kama anavyoeleza Huck (1976), hali hiyo inadhihirisha ukweli ulioko katika maisha. Kwa mfano, mamake Kalaa amesawiriwa kuwa binadamu wa kawaida na katika mazingiria yanayoambatana na hali za kawaida za maisha katika jamii.

### 2.3.4 Mikasa

Mara kwa mara mikasa hutokea na hata kuuchukua uhai wa wanadamu. Mikasa hutokea mara kwa mara nchini Kenya na kwingineko. Baadhi ya mikasa hii ni kama mvua kubwa ambayo huambatana na gharika pamoja na maporomoko ya ardhi. Kwa mfano, mnamo mwezi wa Agosti, mwaka wa 2016, gazeti la 'Standard' liliripoti kuhusu mvua mkubwa iliyoambatana na ngurumo za radi iliyonyesha na kusababisha mafuriko katika eneo la Budalangi, Kaunti ya Busia. Ilisemekana kuwa Mto Nzoia ulifurika na maji yake yakatapakaa kila mahali. Mafuriko haya yalisababisha kuhamishwa kwa watu na mifugo hadi kanisa la Kianglikana; Musoma. Mahali hapa palikuwa salama. Hata hivyo, mafuriko haya yaliharibu mimea na mifugo wengi walisombwa na maji. Isitoshe watu kadhaa walikufa maji. Ilisemekana kuwa familia 1,200 zilikosa makao. Mikasa kama hii husababisha vifo na hivyo watoto kuachwa yatima.

Kumekuwa na ripoti za athari za mvua kubwa kupitia kwa Runinga, idhaa ya 'NTV' na hata magazetini kama gazeti la 'Daily Nation' mwezi wa Mei mwaka wa 2017. Kwa mujibu wa ripoti hizi, maeneo kama vile Kaunti ya Kirinyaga, Kaunti ya Eldoret na hata maeneo ya Pwani, Turkana, Wajir na hata Isiolo yameathirika sana kufuatia mvua kubwa iliyonyesha mwezi wa nne na kusababisha maporomoko. Kunapokuwa na maporomoko haya, maisha ya binadamu huwa yanaathirika kwa njia mbalimbali ikiwemo kupoteza maisha. Katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), babu yake Katiwa anasimulia kisa kinachohusiana na kifo cha wazazi wa Katiwa. Licha ya kuwa vifo hivyo viwili vya wazazi wa Katiwa vilitokana na mgogoro wa kifamilia, hasa kifo chenyewe

kilisababishwa moja kwa moja na mkasa wa kuporomokewa na ardhi kufuatia mvua ya masika iliyokuwa ikinyesha kwa wakati huo.

Aidha katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) kuna kisa cha nyanya ambaye anasimulia kuhusu vijana wawili; Mwilu na Mwila. Mamake Mwilu anapoaga dunia, mama ya Mwila anachimba shimo na kumfukia humo ndani. Ukweli unapogunduliwa, mamake Mwila anajaribu kutoroka na kwa bahati mbaya anatumbukia ndani ya shimo la choo na kuaga dunia. Mkasa wa mamake Mwila kutumbukia ndani ya shimo la choo ulisababisha Mwila kuwa yatima. Mama huyu alimtakia Mwilu mabaya lakini yalimpata yeye mwenyewe.  Ni wazi kwamba baada ya kifo chake, Mwila pia alijipata katika hali ya kuwa yatima.

Kwa mtazamo wa nadharia ya vikale, Frye (2001) mikasa ni vikale ambavyo vimekuwako tangu zamani katika jamii. Jamii hukumbana na mikasa mbalimbali kama vile ukame, mafuriko, vita, ajali na mikasa mingine ambayo husababisha vifo vya wanajamii. Mkasa wa kuporomoka kwa ardhi na kufukia wazazi wake Katiwa katika hadithi ya *Yatima.* Ni kikale ambacho kilisababisha uyatima na kumtumbukiza katika mateso si haba.

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii, hali zinazochangia watoto kuwa yatima zimejadiliwa. Sura hii imetoa uchanganuzi unaolenga kuzibaini hali zinazopelekea watoto kuwa yatima. Hali hizi ni pamoja na mizozo katika familia, tabia kama wivu, chuki, tamaa na magonjwa. Utafiti huu umebaini kuwa, mizozo ya familia ni jambo ambalo hutokea kila mara katika jamii. Hata hivyo, mizozo hii isiposhughulikiwa kwa njia inayofaa ili kuleta maridhiano na uelewano miongoni mwa jamaa, huweza kusababisha maafa ambayo huwaacha watoto katika hali ya uyatima. Katiwa ni mhusika ambaye anajipata katika hali ya uyatima kutokana na tendo la babu yake kuzozana na babake. Kwa ghadhabu kuu anamfukuza nyumbani pamoja na mkewe (mamake Katiwa) hadi kule wanapokutana na kifo chao.

Vilevile, tabia kama vile wivu, chuki na tamaa ni miongoni mwa tabia za kibinadamu ambazo wakati mwingine huleta madhara na hata maafa. Ni dhahiri kwamba, Zebeli anasababisha maafa ya wazazi wote wawili wa Johari na kumwacha akiwa yatima. Suala la magonjwa yanayotokea kighafla na kusababisha vifo, huku yakiwaacha watoto yatima. Mwishoni, sura hii imejadili hali ya mikasa ambayo, kwa wakati mwingine, hutokana na hali za kiasili na kusababisha maafa yanayopelekea watoto kuwa yatima. Sura inayofuata, itaangazia changamoto zinazowakumba watoto yatima kwa kurejelea hadithi zizi hizi tatu teule.

## SURA YA TATU

## CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA WATOTO YATIMA

### 3.1 Utangulizi

Sura iliyopita, ililishughulikia suala la hali zinazochangia watoto kuwa yatima. Sura hii, inaangazia changamoto zinazowakumba watoto yatima. Ni vyema kutanguliza kwa kueleza kuwa changamoto ni kitu, hali au jambo linalomzuia mtu asiweze kuyafikia malengo yake. Pia, ni mazingira kinzani au kikwazo kinachomjia mtu maishani mwake ili kupima uwezo wake wa kukabiliana nacho. Kwa mtazamo mwingine, changamoto ni matatizo katika maisha tunayoyaishi. Inaeleweka kuwa lengo kuu la changamoto ni kumsaidia mtu awe mbunifu na mvumbuzi. Kwa kawaida, maisha ya yatima huwa na changamoto nyingi. Hata hivyo, katika sura hii, kitakachoangaziwa ni changamoto za watoto yatima kama zinavyojitokeza katika hadithi tatu teule. Kama inavyoeleweka kwa jumla, katika maisha ya mtoto yatima, changamoto kuu ni kukosa mzazi au wazazi. Hivyo basi yeye hukosa mambo fulani ambayo mtoto hupata kutoka kwa wazazi wake. Katika hadithi tatu zilizoteuliwa katika utafiti huu, na kufuatia uchanganuzi uliofanywa, changamoto zinazowakumba watoto yatima zimeainishwa katika mada kuu ya; ‘watoto yatima kunyimwa haki zao.’

#### 3.1.1 Dhana ya Haki za Watoto

Sheria ya nchi ya Kenya, hususan sura ya sita, katika katiba ya Kenya (Republic of Kenya, 2010), ina vipengele vinavyozungumzia haki za Wakenya wote kwa jumla na pia

vipengele vinavyozungumzia haki za watoto. Katika sura ya sita, kipengele cha 41 kinaangazia kwa kina suala nzima la haki za watoto. Kwa jumla, Katiba ya Kenya (Ibid, 2010), katika sura hii na kipengele hiki inaliweka wazi suala la watoto kwa kukariri kuwa, "Watoto ni sehemu muhimu katika jamii na kuwa ni jukumu la wazazi, familia, jamii na serikali kuwalea, kuwalinda na kuwasomesha watoto." Jambo lililo la kimsingi katika sura hii kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu ni kuwa; kila mtoto ana haki zake. Haki hizi ni pamoja na: malezi bora, elimu, kulindwa dhidi ya kubaguliwa, kutumiwa vibaya, kutupwa au kunyanyaswa; aina yoyote ya kunyanyaswa na kazi yoyote itakayohatarisha maslahi yake; haki ya kupata chakula cha kutosha, makazi, huduma za malezi ya kiafya na huduma za kijamii. Kipengele hiki pia kinaorodhesha kuwa watoto wenye mahitaji maalumu wana haki ya kupewa ulinzi maalum na Serikali na jamii. Hatimaye, kipengele hiki kimekariri kuwa, Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo kutekeleza maelezo ya Katiba hii na ya nyenzo za viwango vya kimataifa kuhusu haki za mtoto.

Kwa mtazamo wa sheria na haki za watoto, yapo matukio katika hadithi zinazozingatiwa katika utafiti huu ambayo yamewasawiri wahusika, hususan watoto. Watoto wamesawiriwa wakiwa katika hali ya kukumbwa na changamoto ambazo kimsingi zinatokana na ukiukaji wa sheria. Katika sehemu zifuatazo, changamoto hizi zitajadiliwa kwa misingi ya kuwanyima watoto yatima haki na uhuru wao kama inavyokaririwa katika hadithi teule.

### 3.2 Kufanyishwa kazi nyingi na ngumu

Kwa mujibu wa Senefeld, Strasser na Campbell (2009), kuna visa vingi ambapo watoto yatima huteswa na watu wa ukoo wanaoishi nao au walezi wao. Watafiti hawa wanaeleza kuwa mateso dhidi ya watoto yatima hujumlisha dhuluma za aina mbalimbali dhidi yao kama vile dhuluma ya kimapenzi, kunyimwa haki ya malezi bora na hata kufanyishwa kazi ngumu.

Katika hadithi hizi teule, visa kama hivi hutokea katika maisha ya watoto yatima kama wahusika wakuu. Wahusika hawa wanakumbana na changamoto si haba. Mojawapo ya changamoto hizo ni kufanyishwa kazi nyingi tena ngumu. Kama vile, kuamka mapema na kuanza kufanya kazi za nyumbani hadi machweo pasi na kupewa muda wa kupumzika. Watoto wanaoteswa hukua wakihisi kuwa hawapendwi na kuthaminiwa. Mtoto aliye na mawazo haya huwa na maisha mabaya na hadhi yake huwa duni kwa vile hajithamini wala kujiamini. Kwa mfano, katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), inaelezwa kuwa Kalaa ambaye ni mhusika mkuu na ni yatima, alifanyishwa kazi nyingi iliyozidi umri wake. Inabainika kuwa Kitete alimfanya Kalaa mtumishi wake; alimtaka kuamka jogoo la kwanza, kuandaa kiamsha kinywa na kuwapashia moto maji ya kuoga (Kisovi, 2005:28).

Matendo haya yanakiuka sheria kama ilivyokaririwa katika Sheria ya Watoto (2010) Sehemu ya Kumi Kitengo cha 1. Sheria imeweka kiwango cha umri wa kuajiriwa kuwa miaka kumi na sita na zaidi, Katiba ya Kenya (2010). Aidha, inafahamika kuwa Kitete,

mamake Kalaa wa kambo, angesikika akimuamrisha Kalaa ‘kabla ya kunywa chai ni lazima ufue nguo na kuzianika…” (Kisovi, 2005:28). Zaidi ya hayo, mwandishi anaeleza kuwa kazi hizo zilikuwa ngumu na za lazima. Hata baada ya kuondoka kwa Pendo, dadake Kalaa wa kambo, akienda kuolewa, ilitokea kuwa:

> Kitete aliendelea kumtesa na kumfanyiza kazi nyingi mwana huyu wa watu bila ya imani wala huruma…alizoea kumwambia, “Kazi yako itakuwa ya kunitumikia na daima hutapata raha zozote” (Kisovi, 2005:47).

Watoto huwa na raha na siha njema wakati maisha yao yanaweza kutabirika kuwa yaliyo na usalama. Jambo hili huwapa watoto utulivu wa kimawazo. Hivi ni kinyume na alivyotarajia Kalaa. Kitete, mamake wa Kambo alihakikisha kwamba Kalaa hana raha wala utulivu wa kimawazo. Alimfanyisha kazi ngumu na nyingi bila huruma wala imani.

Doodson & Davies (2014) wanasema kuwa tafiti zinaonyesha kuwa familia nyingi za kambo huwa na matatizo mengi ambayo husababishwa na mienendo ya mama wa kambo kama vile kuwapendelea watoto wake na kupuuza na kuwaonea watoto aliowapata alipoolewa katika familia husika. Kwa mfano, inadhihirika waziwazi kuwa Kitete, kwa sababu ya mwenendo wake wa kumpendelea mwanawe dhidi ya Kalaa, alikusudia kumtesa Kalaa kwa vyovyote vile. Katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) inafahimika kuwa wakati Katiwa alienda kuishi na Mam’ Peter, alifanyishwa huko kazi nyingi za kuchosha kama mwandishi anavyoeleza:

> Alifanya kazi zote za nyumba ingawa umri wake ulikuwa mdogo…alisafisha nyumba, alitoa mikeka ya nyumba nje na kuondoa vumbi, alipanguza vioo vya madirisha ya nyumba, alizunguka nyumba na kutoa majani ya miti yaliyoanguka huko chini na kuyatia katika shimo la uchafu. Mwishowe aliwapelekea mbwa waliokuwa pale chakula… na kumpelekea kuchoka tiki (Wamitila, 2006:47).

Hata baada ya kula chakula kulichokuwa kimeharibika na kumpelekea kusokotwa na tumbo usiku kucha, Katiwa alijaribu kumsihi Mam' Peter aweze kumpeleka kwa daktari, Mam' Peter alimdanganya kuwa shangaziye atakuja kumpeleka. Mwandishi anasema kuwa:

> Mam' Peter hakujali kama alikuwa na maumivu au la. Aliendelea kumwachia kazi nyingi za kufanya. Alimwachia mlima wa vyombo vya jikoni wa kuosha: masahani, vikombe, vijiko, nyuma, masufuria na glasi… (Wamitila, 2006:59).

Kama ilivyokuwa na Kitete kukusudia kumtesa Kalaa katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), vivyo hivyo ndivyo inavyodhihirika katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), kwa mateso aliyompa Mam' Peter, msichana huyu aliyeletewa na shangazi Juliana. Hakujali kama Katiwa kachoka wala kuwa na maumivu kutokana na kazi nyingi aliyomrundikia ila tu aone kazi zote zimefanyika.

Katika malezi, mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ambayo ni sharti yakidhiwe na kutoshelezwa ni kuonyeshwa mapenzi. Mapenzi yanahitajika kwa kukua ifaavyo kihisia katika maisha. Katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), Katiwa hayapati wala haonyeshwi mapenzi kama inavyohitajika kwa watoto wa umri wake. Wakati anaposokotwa na tumbo baada ya kula chakula kibaya, Mam' Peter hakujali hali yake hata kidogo. Alimuambia kuwa huo haukuwa wakati wa kuumwa na tumbo. Alimwambia kuwa asimsumbue na kumwamrisha kuenda kulala mara moja.

Hali inatokea kuwa ile ile katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), pale ambapo Johari anafanyishwa kazi mchana kutwa na mamaye wa kambo, kama ilivyokuwa na Kalaa kufanyishwa kazi zote za nyumba bila wakati wa kupumzika, katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005). Johari aliyesawiriwa kama mpole, mwenye maadili mema na aliye na bidii anapata mateso ya kufanyishwa kazi nyingi na ngumu na mamake wa kambo, Zebeli, bila kutoa malalamishi yoyote. Hata baada ya kifo cha mamake mzazi, Zebeli ambaye ni mamake Johari wa kambo, mwandishi anaeleza kuwa Zebeli alikuwa akimfanyisha kazi kama mtumwa (Ng'ang'a, 2006) kama ilivyo katika nukuu ifuatayo:

> Johari angepewa kazi ya kujaza pipa zima la maji jioni baada ya kutoka shuleni (Ng'ang'a, 2006:32).

Mwandishi anaeleza zaidi kuwa hata ingawaje Johari alikuwa mwanzoni akienda shule kama Wakesho, ambaye ni dadake wa kambo, alikuwa pia akizifanya kazi zote za nyumbani peke yake. Katika sura inayozungumzia maisha mapya ya Johari yasemekana kuwa:

> Zebeli alikuwa anamwamsha alfajiri na mapema ili awatayarishie wanawe kiamsha kinywa ili waende shuleni… Johari angeamrishwa kwenda shambani akapalilie mimea… (Ng'ang'a, 2006:36).

Kulingana na nadharia ya uhalisia, Larkin, (1977), hali ya kufanyishwa kazi nyingi na ngumu kwa yatima ni mfano mzuri wa mhimili wa kihalisia. Yatima wengi hufanyishwa kazi nyingi na ngumu. Hali hii wakati mwingine huwapelekea kutoroka na kutafuta mahali pengine pa kuishi kwa usalama na bila kubaguliwa au kuonewa.

Jambo linalojitokeza waziwazi ni kuwa, matukio haya yote yanayomsawiri yatima kuwa yule anayefanyishwa kazi nyingi na ngumu, yamesimuliwa kwa hali inayomrejesha msomaji katika ulimwengu wa kawaida. Ni matukio ambayo yanatendeka mara kwa mara katika jamii na familia tunamoishi. Hivyo basi, inakuwa rahisi kuambatanisha matukio hayo na matukio ya maisha ya kila siku.

### 3.3 Kunyimwa haki ya Elimu

Haki ni dhana ambayo ina maana ya kumtendea mtu ipasavyo kulingana na sifa au tabia zake TUKI, (2004). Palipo na haki pana usawa na amani. Watoto ni wanajamii wanaopenda kuona haki ikitekelezwa. Wanaamini kuwa haki ikitekelezwa, inasuluhisha baadhi ya matatizo katika jamii kama vile maonevu, dhuluma na ubaguzi. Kutokana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa haki za kibinadamu pamoja na kipengele cha Sheria ya Watoto ya mwaka wa 2001, watoto wana haki zao ambazo ni lazima zizingatiwe, *The Children Act* (2001). Mojawapo wa haki hizi ni haki ya elimu. Sehemu hii inalishughulikia suala la ukiukaji wa kuwahakikishia watoto yatima haki yao ya elimu na kupelekea watoto hao kukumbana na changamoto nyingi zinazotokana na ukosefu wa elimu.

Kwa kurejelea hadithi ya *Yatima, (*Wamitila, 2006) mhusika mkuu, Katiwa, anaonekana mwanzoni akiishi na shangazi yake ambaye hakujali kumpeleka shuleni. Hata hivyo, na kwa tendo lililoashiria ubaguzi, Shangaziye Katiwa aliwapeleka watoto wake, Maria na Kevin shuleni ili kupata elimu. Baadaye shangaziye Katiwa anampeleka kuishi na babu

yake huko Masira. Katiwa anaishia kuchunga kondoo na mbuzi akisaidiwa na Mule ambaye ndiye aliyekuwa mchungaji wa mifugo ya babu yake Katiwa. Hata ingawa walikuwa na umri wa kuwa shuleni, wawili hao; Katiwa na Mule, hawakuenda shule. Walinyimwa haki yao ya elimu. Jambo hili la kunyima mtoto haki limetiliwa mkazo katika Mkataba wa Watoto (2001) unaosisitiza kuwa kila mtoto anayo haki ya elimu. Baada ya muda mfupi wa kuishi na babu yake, shangaziye Katiwa anamchukua na kumpeleka kuishi na Mam' Peter kama yaya. Hapa pia Katiwa hakupata kupewa haki yake ya elimu bali mwandishi anaeleza kuwa:

> Mchana watoto wa Mam' Peter walipokwenda shuleni, Katiwa alibaki nyumbani. Wakati huo alipaswa kusafisha nyumba… (Wamitila, 2006:47).

Hali hii ya kunyimwa haki ya elimu inaendelea hadi Katiwa anapoopolewa na mwanachama wa kikundi wa kushughulikia haki za watoto, Bettina, na kurudishwa kwa babu yake. Babu kwa upande mwingine anaipinga mipango ya Katiwa kusomeshewa mjini alivyotaka Bettina. Anaamua kutumia rasilimali alizokuwa nazo kumsomesha Katiwa pamoja na Mule. Na hapo ndipo wanapata haki yao ya elimu, haki waliyokuwa wamenyimwa kwa muda mrefu sana.

Aidha, katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), inaarifiwa kuwa Johari alikuwa anasoma pamoja na watoto wake Zebeli. Baada ya miezi mitatu kufuatia kifo cha babake, Johari aliachishwa shule (Ng'ang'a, 2006:35) akiwa katika darasa la saba, hata ingawa watoto wake Zebeli kwa upande mwingine waliendelea na masomo yao. Huku haya yakitendeka, Zebeli alikuwa anamwamrisha Johari kuamka alfajiri na mapema ili

awatayarishie wanawe kiamsha kinywa. Baada ya kupata kiamsha kinywa, walienda shuleni huku Johari akiamrishwa kwenda shambani kupalilia mimea (Ng'ang'a, 2006:36). Hata hivyo, hii haikuwa kwa kupenda kwake Johari. Ilikuwa kwa kauli yake Zebeli kumnyima Johari haki yake ya elimu kama anavyoeleza mwandishi:

> Johari alijaribu kumsihi mamake wa kambo amwache aendelee na masomo lakini maombi yake yaliambulia patupu… (Ng'ang'a, 2006:35).

Kauli ya Zebeli kumnyima Johari haki yake ya elimu inadhihirika zaidi hapo mwandishi anapoeleza vile ambavyo jirani yake Zebeli alijaribu kumsihi amwache Johari asome kwani aliutambua umuhimu wa elimu. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Mama Wakesho, mwache Johari asome. Siku hizi hakuna urithi ulio aali kama elimu. (Ng'ang'a, 2006:35).

Hata hivyo, mwandishi anakariri namna ambavyo Zebeli alimkemea kwa ukali jirani huyu kuhusu maoni yake na kumtia woga mwingi kwa kusema:

> Wewe ndiwe nani? Mbona unanikosea heshima kiasi hicho! Boma hili ni langu na ni lazima uamuzi wangu uzingatiwe… (Ng'ang'a, 2006:36).

Na kwa kauli hii, Zebeli anaendelea kumnyima Johari haki yake ya elimu pasipo na kujali matokeo ya tendo hili.

Katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), Mzee Magufuli ni mhusika ambaye anamsaidia Johari baada ya kuguswa na maisha yake ya dhiki na kuamua kumuokoa. Kwa mujibu wa nadharia ya vikale Frye (1957) mzee huyu, hutokea wakati nguli yuko katika hali zisizokuwa na matumaini na za kukata tamaa. Ni mhusika mkarimu na mwenye uwezo wa kuhisi jambo haraka na kila wakati yuko tayari kusaidia.

Hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), imemsawiri mhusika mkuu, Kalaa, kama mtoto aliyenyimwa haki ya elimu. Jinsi maisha yake yote yalivyosimuliwa katika hadithi hii, hakuna wakati ambapo anapata elimu shuleni. Watoto wengine wanapoenda shuleni, yeye anabaki nyumbani kufanya kazi anayopewa na mamake wa kambo. Hii inadhihirisha kwamba Kalaa amekosa kabisa kupata haki yake ya elimu.

### 3.4 Mtoto yatima kukosa mahitaji ya Kimsingi

Aina nyingine ya kunyimwa haki inayodhihirika katika hadithi hizi teule ni ile ya mtoto yatima kukosa mahitaji ya kimsingi. Mahitaji ya kimsingi hujumuisha mambo chakula, elimu, afya na ulinzi wa sharia na makuzi sahihi ya watoto. Hali hii inajidhihirisha pale ambapo Kalaa katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Wamitila, 2006), ananyimwa mavazi mazuri akawa anavaa matambara. Hata hivyo, Konelia, babake Kalaa, anapomuuliza Kitete ambaye ni mamake Kalaa wa kambo, Kitete anamgeukia kumshangaa Kalaa kwa kusema kuwa yeye hupendelea kuvaa nguo moja tu, iwe imeraruka au la (Kisovi, 2006:31). Anadai kwamba wakati mwingine hushindwa Kalaa ni msichana wa aina gani ikiwa hata kuoga analazimishwa. (Kisovi, 2006:31). Kwa upande mwingine, hali ni ile ile katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) ambapo Johari ananyimwa mambo ya kimsingi kama lishe inavyokaririwa na mwandishi kwenye nukuu hii:

> Johari alipimiwa chakula kama dawa. Nao wanawe Zebeli wakilishwa mapochopocho, vitumbo vyao vilivimbiana kama vitoma vya maziwa. Mara nyingi wanawe Zebeli wangelishwa mayai na kunywa maziwa huku Johari akila chakula cha maharagwe yenye viwavi (Ng'ang'a, 2006:33).

Kulingana na nadharia ya uhalisia, hali ya mtoto yatima kunyimwa haki ya mahitaji ya kimsingi na uhuru ni mambo ya kihalisia. Hufanyika katika jamii ya kawaida na

ulimwengu halisi. Watoto wengi hasa yatima hunyimwa haki na uhuru na walinzi wao. Hili hufanyika kwa sababu hawana mtu wa kuwatetea na kuwakinga kutokana na hatari hii. Kwa hivyo wengi huvumilia mateso kwa kutumainia kuopolewa siku moja.

### 3.5 Yatima kutengwa, kubaguliwa na kutelekezwa na jamii

Kell (1983) anaeleza kuwa kutengwa na watu humfanya mtu ahisi upweke unaoweza kumletea madhara ya kihisia. Mayatima wengi katika jamii hutengwa na kubaguliwa, kauli hii inaungana na mhimili wa nadharia ya uhalisia ambao unaelezea kutengwa kama jambo linalofanyika katika jamii. Kutengwa ni jambo halisi ambalo utalipata katika jamii la kawaida. Mayatima wengi katika jamii hutengwa na kubaguliwa.

Katika ulimwengu wa sasa, kumekuwa na visa vingi vya watoto, hususan yatima kubaguliwa, kutengwa na jamii au ikizidi, kutelekezwa. Mara kwa mara, watoto kama hawa huishia kurandaranda mitaani na mijini kama chokoraa. Aidha, wengine huishia kwenye ajira ya watoto (Kisia 1996). Sehemu hii inalenga kuzichanganua hali za kutengwa, kubaguliwa na hata kutelekezwa kwa mtoto yatima katika hadithi tatu teule zinazoangaziwa katika utafiti huu.

Kwa kuirejelea hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2006), inaarifiwa kuwa Kitete alianza kumtenga Kalaa kutoka kwake Pendo. Mwanzoni kabisa mwandishi anaeleza kuwa Kitete alimbandika Kalaa lakabu ya 'Wakale', ikiwa na maana ya 'wa zamani'. Hii iliashiria kuwa alimwona Kalaa kuwa mtoto aliyekuwa na hali iliyopitwa na wakati.

Akimlinganisha na mwanawe Pendo, anamwona Pendo kuwa na hali ya kisasa, labda kimasomo, kimavazi na kadhalika. Baada ya hapo inaelezwa kuwa Kitete alianza kumtenga Kalaa na Pendo. Mara nyingi alimwambia Kalaa 'sitaki ucheze na Pendo-utamchafua' (Kisovi, 2005:28).

Kutenganishwa kwa watoto na mama yao, au watu wanaowaamini husababisha upweke na wasiwasi usioisha. Akishadidia hoja hii Bowbly (1969) anaeleza kuwa ukuaji wa wanadamu hasa watoto hukamilika vizuri wakiwa karibu na mtu wanaomwamini na kumpenda. Aidha, wakati vijana wawili waliotoka ughaibuni walifika, wakiwa na lengo la kutafuta wachumba, Kitete anamtayarisha bintiye Pendo kusudi aende akajaribu kuwapendeza vijana hao. Alimkanya Kalaa kwenda, hata kama Kalaa alikuwa pia amekomaa kiasi cha kuchumbiwa. Mwandishi anasema kuwa:

> … alimpamba Pendo akapambika kisha alimtaka Kalaa kubaki nyuma kama mlinzi wa nyumba (Kisovi, 2005:45).
>
> Kwa njia ya dharau na ubaguzi bayana, Kitete alimwambia Kalaa kuwa vijana hao walikuwa maridadi na hawangejaribu kumwangalia msichana ovyo kama yeye. Hata wageni walipowasili, Kalaa hakupewa hata angaa nafasi ya kuwasalimia. Kitete alimtaka aende kushughulikia kazi za asubuhi ili asiwakaribie (Kisovi, 2005:45).

Isitoshe, kila walipokuja vijana wakitaka mkonowe Kalaa katika ndoa, Kitete aliendelea kumuumbua na kuhujumu nafasi yake Kalaa kujipatia mchumba (Kisovi, 2005:47). Mwishowe inadhihirika kuwa Kitete alilichangamkia suala la Kalaa kujipatia mchumba, kijana aliyeonekana maskini. Aliuzidisha ushawishi wake kwa babake Kalaa akubali Kalaa kuolewa. Kitendo hiki ni cha unafiki mtupu.

Kitete anakubali Kalaa kuolewa na kijana huyu kwa sababu ni kijana aliyeonekana maskini hohehahe asiye na mbele wala nyuma. Tendo hili linaweza kutafsiriwa kuwa Kitete alitaka maisha ya Kalaa daima yawe ya hali ya chini. Alihakikisha kwamba Kalaa ameolewa na kijana maskini kinyume na vile alivyomtakia bintiye. Hata hivyo, kwa kuzingatia kuwa alikuwa amekataliwa na kubaguliwa na Kitete, Kalaa anamkubali kijana huyu aliyeonekana maskini hasa kwa kuzingatia mateso aliyokuwa akiyapata. Kinyume na maisha ya kukataliwa na kubaguliwa kama ilivyokuwa nyumbani kwao, kijana huyu alikuwa amempenda bila kujali hali yake Kalaa.

Hali inakuwa sawa na hii kwenye hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006). Mwanzoni mwa hadithi hii, Katiwa alizoea kuishi na shangazi yake lakini baadaye inavyoelezwa, shangazi yake anampeleka Masira kuishi na babu ambaye mwanzoni hakumchangamkia hata kidogo. Hali hii ilionekana kama njia moja ya kukataliwa au kutelekezwa kule Masira na babu yake. Katiwa aliwekwa katika mazingira yaliyokuwa na changamoto si haba. Alionekana kama mtoto asiyetakikana. Gelles (1973) anasema kuwa mtoto asiyetakikana huchukuliwa kama mzigo usiotakikana, mfadhaiko na chanzo cha usumbufu.

Babu hakutaka hata kumwangalia Katiwa alipokuwa akijitambulisha, hii ikiashiria kuwa babu hakumpenda hata kidogo na alikuwa kama mzigo kwake. Bila shaka, hii inaibua hisia za kukataliwa au hata kubaguliwa kwake Katiwa. Ni wajibu wa jamii kuwatunza watoto kama hawa. Kukataa kwa shangazi kuishi na Katiwa ni kinyume na maoni haya.

Yeye kama mwanamke anatarajiwa kujua kwamba mtoto wa umri huo anafaa kulelewa na mwanamke bali si mwanamume kama babu.

Hata ingawa Katiwa alikuwa na umri wa kupenda kucheza na wenzake, mwandishi anaeleza kuwa Katiwa hakuruhusiwa kutoka nje. Baada ya kumaliza kufanya kazi zake, alilazimika kukaa nyumbani hadi watoto wale wengine waliporudi. Akatamani kutoka nje na kucheza na watoto wa majirani au hata kuota jua na kucheza mwaficho lakini hakuwa na ruhusa. Mara nyingi aliishia kusimama dirishani na kuwaangalia watoto huko nje kama ndege aliyewekwa tunduni. Wakati watoto wa Mam' Peter walikuwa wakitazama televisheni, yeye hakuruhusiwa kuitazama pamoja na wenzake kama mwandishi anavyobainisha katika dondoo hili:

> Siku za Jumamosi na Jumapili, watoto walitazama vipindi vya vibonzo au katuni katika televisheni. Lakini Katiwa hakutazama televisheni! 'Hujui maana yake…' alikatazwa na kuambiwa hakujua bei ya televisheni…wakati wanaangalia televisheni yeye aliketi huko jikoni. Alitamani sana kuangalia televisheni lakini hakuruhusiwa. Alisikiliza tu akiwa mbali (Wamitila, 2006:53).

Kwa jumla, Katiwa anakataliwa kama vile anavyokataliwa na babu yake wakati shangazi anapompeleka kuishi na babu. Vile vile, anapoenda kuishi na Mam' Peter anajihisi kuwa Mam' Peter hakumpenda lakini anajipa moyo kuwa labda Mam' Peter atampenda baadaye. Hii ni hisia sawa na ile aliyokuwa nayo alipokutana na babu yake siku ya kwanza.

Hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) inamsawiri Johari kama mtoto yatima aliyekataliwa na kutengwa na jamaa yake. Mwanzo wa kutengwa kwake inakuwa pale

anapomwendea mamake wa kambo, Zebeli, na kumwarifu kuwa angependa kujaribu bahati yake kule mjini ili afaulu maishani. Zebeli alikataa kata kata wazo hilo. Alimzomea na kumtahadharisha kuwa hangemkubali hapo nyumbani tena iwapo angeufuata ushauri wa Mzee Magufuli. Ni wazi kwamba Zebeli alikuwa tayari kumtenga Johari na familia yake kama angeenda mjini. Utengano unadhihirika pia kupitia kwa majibu ya barua yake iliyoandikwa na Wakesho. Mwanzo, anamwita Johari Debora, jina hili la pili likiwa la mamake, badala ya Johari Kido. Aidha katika barua ambamo Wakesho anamsuta na kumwambia kuwa hataki 'vifedha vyake'. Zaidi ya hapo, barua iliendelea kwa kusema;

> Mama alinieleza nikufahamishe kuwa ulipoondoka nyumbani alimtupa jongoo na mti wake. Hana hamu ya kukuona, sisemi kuona hivyo vibarua vyako vya geresha. Koma kutudhihaki na vifedha vyako duni. Hatuna haja navyo! Pasahau hapa na usipaite nyumbani tena! Msiye na uhusiano tena,Wakesho Kido. (Ng'ang'a, 2006:46-47)

Inabainika kuwa mwisho wa barua hii 'Msiye na uhusiano tena Wakesho Kido' unadhihirisha kutengwa kwake Johari na familia hii. Dadake hataki uhusiano zaidi na yeye na kuwa hawamtambui kama mtoto wa baba yao. Wanamwita 'Johari' na kufuatisha jina la mamake, 'Debora', badala ya jina la babake, Kido. Hata Johari anapoendelea kuishi anaanza kuyatamani mandhari ya nyumbani lakini anakumbuka kuwa hana pa kwenda kwani nyumbani kwao ameshakataliwa. Uhalisia wa kukataliwa kwake unadhihirika pale ambapo anajitahidi na kufunga safari ya kwenda nyumbani kwao. Alikuwa ameandamana na Mzee Magufuli. Aliamini kuwa Mzee Magufuli angeleta upatanisho kati yake na familia yake. Mzee Magufuli aliandamana na Johari alipoenda

nyumbani kwa Zebeli kukutana na familia yake tena. Alikuwa tayari kumsaidia Johari kwa vyovyote vile.

Hali ya kutengwa kwa mayatima imetafitiwa mara kwa mara na watafiti mbalimbali, kama vile, Doodson & Davies (2014) wanasema kuwa mama wa kambo mara kwa mara huchukua muda mwingi kushughulikia watoto wake huku akiwatenga wale ambao si wake. Hata hivyo, wingi wa matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na hali hii iliyoko kwenye hadithi hizi tatu teule. Kwa mfano, kwa mujibu wa Nayak (2014), baadhi ya changamoto zinazowakumba watoto yatima ni pamoja na kutengwa na kubaguliwa watu katika jamii ambamo wao hawa huishi. Hii husababisha athari za kisaikolojia kwa watoto hawa yatima.

Lakini kinyume na hayo, inadhihirika kuwa Zebeli alishangaa kumwona kwani hakutegemea kuwa Johari alikuwa na lolote la kumhusisha na familia hiyo. Mazungumzo yaliyofuata yanaiweka wazi hali ya Johari kukataliwa na hata kutelekezwa kama mwandishi anavyoisawiri:

> Ni Johari?...Ebo, ni nini kimekuleta hapa.Hukuipokea barua? Hata mkaja hapa na Mzee Magufuli msimamo wangu hautabadilika! … mimi sikumkataa, yeye mwenyewe alijikataa. Aliondoka hapa bila kujali niliyomwambia… Nani ameomba usaidizi wake? Sisi hapa tulipo tunajiweza. Hatumhitaji tena hapa. Arudi huko alikofikiria ndiko nyumbani. Uhuni wa mjini asiulete hapa… Ondokeni na huyo mhuni wako. Mzee Magufuli…ukome kuingilia mambo ya nyumba hii. Koma kabisa! (Ng'ang'a, 2006:56).

Hii ndiyo ilikuwa dhoruba ya mwisho kumpiga Johari. Zaidi ya hapo, alikumbuka kuwa Zebeli alikuwa amewaarifu kuwa alishachoma vitu vyake vyote baada ya kuondoka

kwake. Hii inaashiria ‘kuondolewa kwa kivuli chake nyumbani kwao’ Ng’ang’a, (2006:57). Ukweli ni kwamba alikuwa ameshakataliwa kwao. Jambo la kuhuzunisha zaidi ni kwamba Zebeli alisisitiza kuwa hamhitaji Johari wala msaada wake, kisha akamuamuru aondoke kwake. Johari alianza kulia kwa kwikwi huku nduguze wa kambo wakimcheka. Ilikuwa siku ya huzuni na majonzi kwa Johari kukataliwa na familia yake; ilikuwa dhoruba kuu kwake.

**3.6 Kutumiwa kwa Mtoto Yatima kama Kitega Uchumi**

Mojawapo ya changamoto zinazowakumba watoto yatima ni jamii wanamoishi kuwatumia kama vitega uchumi. Mara kwa mara watoto hawa huwekewa miradi au kazi zozote zile wanazozifanya ili kuiletea familia inayodai kuwatunza faida. Katika hadithi hizi tatu teule, kunayo matukio kama haya ambapo yatima wamesawiriwa kama wanaotumiwa na familia wanamoishi kama vitega uchumi. Ajira ya watoto imekithiri kwa sababu ya waajiri ambao wanajinufaisha kwa kutumia watoto vibaya. Kwa mujibu wa Edmonds (2009), kazi hizi wanazozifanya watoto wa umri mdogo huwaathiri kijamii, kisaikolojia na vinginevyo. Watafiti wengi wameisawiri ajira ya watoto kama mojawapo wa njia za kuwanyanyasa watoto. Kwa mujibu wa nadharia ya vikale hali ya watoto kufanyishwa kazi ni kikale. Watoto wamekuwa wakinyanyaswa tangu zamani za kale hata kwenye fasihi simulizi. Isitoshe, kazi hii inajitokeza kama kazi ya sulubu ambayo ni kikale cha zamani cha utumwa.

Kwa kurejelea hadithi ya *Yatima,* Wamitila, (2006), Katiwa aliyekuwa yatima na mhusika mkuu anachukuliwa na shangazi yake kutoka kwa babu yake kwa kisingizio kuwa ameitwa huko mjini kupitia kwa barua fulani. Kisha baadaye shangazi yake anampeleka kwa Mam' Peter kama mfanyikazi wa nyumbani. Hata hivyo, Katiwa anashindwa kuelewa sababu ya kutopewa pesa zozote. Siku moja Katiwa alimwona Mam' Peter akimpa shangazi pesa fulani kisha akaondoka, (Wamitila, 2006:47) Katiwa hakuelewa maana ya kitendo hicho. Baadaye mwandishi anaonyesha kuwa Katiwa alikuwa akifanya kazi lakini hakuwa akipewa mshahara wake kwani shangazi yake ndiye aliyekuja kuuchukua mshahara kutoka kwa Mam' Peter kila mwisho wa mwezi. Ni wazi kuwa shangazi yake Katiwa alikuwa akimtumia Katiwa kama kitega uchumi. Alimtoa kwa babu yake kule Masira ili aje kumtumia kwa manufaa yake.

Hali haikuwa tofauti katika hadithi ya *Mateso ya Johari,* Ng'ang'a, (2006). Katika hadithi hii mwandishi anaeleza kuwa kando na mimea aliyokuwa akipanda na iliyonawiri vyema, Johari alianzisha bwawa la kuwazalishia samaki ambako wanakijiji walikuwa wakinunua samaki kwao. Hata hivyo, Zebeli alizichukua pesa zote zilizotokana na mauzo ya samaki hao. Johari kwa upande mwingine hakuambulia chochote. Jasho lake lilistarehesha wengine, Zebeli na wanawe, ambao hawakujua uchungu wa kulitumia jembe, Ng'ang'a, (2006:36).

Kwa upande mwingine, kuna haki ya kufaidika kutokana na jasho lao watoto yatima. Hii ni aina ya unyanyasaji wa watoto yatima ambayo inaenda kinyume na sheria ya watoto ya

Mwaka wa 2001. Pia katika Katiba ya Kenya (Republic of Kenya, 2010), sura ya sita, inayosisitiza kulindwa dhidi ya aina yoyote ya kunyanyaswa na kazi yoyote itakayohatarisha maisha yao.

### 3.7 Mtoto yatima kuishi katika mazingira magumu

Watoto walio na umri wa chini ya miaka kumi na nane wanalindwa na Mkataba wa Watoto (2001). Mkataba huu unawapa watoto haki ya kuishi katika mazingira yasiyohatarisha maisha yao. Kwa hivyo, kukingwa na hali zinazoyaweka maisha yao hatarini ni mojawapo ya haki ambazo watoto yatima hunyimwa. Watoto yatima huishi katika mazingira yaliyojaa changamoto. Hata ingawa baadhi ya changamoto hizi zimeshatajwa kwenye sehemu zilizotangulia, sehemu hii inaangazia anamoishi mtoto yatima kama alivyosawiriwa katika hadithi hizi teule.

Katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), hali ya Kitete kumfanyisha Kalaa kazi ngumu na kumpimia chakula ‘kama dawa’ inamfanya akonde ‘kama sindano’. Kutokana na hali hii, afya yake Kalaa inaathirika kwa sababu ya kukosa lishe bora. Hali hii inayoashiria ukosefu wa kinga dhidi ya hali za kumhatarishia Kalaa maisha yake. Watoto yatima hukabiliwa na shida ya waangalizi ambao wanahitaji kukidhi mahitaji yao. Kwa sababu ya kupuuzwa kwa mahitaji yao, yatima huteseka sana kwani wao hawana ajira yoyote ya kuwapa kipato ili waweze kujikimu. Mara nyingi, wao hulazimika kukaa njaa au kula chakula kisichofaa, hili likiashiria mazingira duni wanamoishi watoto yatima. Isitoshe, katika mateso haya yote, ni wazi kuwa Kalaa

hakuwa na wa kumlilia na kumpelekea kuishi maisha ya upweke kama anavyoeleza mwandishi:

> Kalaa alizidi kujiona mkiwa na mpweke baba yake alipokuwa mbali. Hakuwa na yeyote wa kumlilia (Kisovi, 2005:35).

Changamoto hizi za kunyimwa haki kwa watoto yatima zimekithiri sana katika tafiti nyingi ambazo zimefanywa barani Afrika. Kwa mfano, utafiti wa hivi majuzi uliofanywa na Abashula, Jibat na Ayele (2014) nchini Ethiopia umebaini kuwa watoto yatima hukumbana na changamoto kama vile kukosa chakula, mavazi, elimu na mahitaji mengine ya kimasomo, na kuwa kukosa mapenzi kutoka kwa wazazi huwasababishia watoto hawa msongo wa mawazo.

Katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), Katiwa anaonekana akiwa amezoea kuishi na shangazi yake kisha shangazi anampeleka kwa babu akaishi naye. Shangaziye Katiwa anamwacha katika mazingira ambayo hajayazoea. Aidha ni mazingira yaliyo na watu ambao hawajui wala kufahamiana. Mwandishi anaeleza kuwa Katiwa alipomwona babu alimwogopa kwa sababu babu alimwonyesha waziwazi kwamba hamtaki. Hali hii inadhihirika zaidi mwandishi anapoeleza kuwa Katiwa alipojaribu kujitambulisha kwa babuye, babu aliangalia upande mengine. Mwandishi anaeleza;

> Hakugeuka hata baada ya Katiwa kuyasema maneno hayo. Aliendelea kuangalia upande huo kwa muda. Mwishowe aligeuka na kumwangalia Katiwa kuanzia chini hadi kichwani. Bila kusema lolote alishika njia na kutokea mlango wa pili na kumwacha Katiwa amesimama pale pale (Wamitila, 2006:7).

Hii ni hali inayoonekana kuwa ngumu sana kwa maisha ya mtoto huyu aliye yatima na mhusika mkuu. Ama kwa kweli, ilikuwa vigumu sana Katiwa kuishi na babu yake ambaye ameonyesha waziwazi kwamba hampendi. Ni dhahiri kuwa badala ya babu kuonekana kama ambaye angemkinga Katiwa kutokana na hatari yoyote, yeye ndiye anayemsababishia Katiwa hisia za kuwa maisha yake yamo hatarini.

Baada ya kuanza maisha kama mfanyakazi wa nyumba kwake Mam' Peter, Katiwa alikumbana na hali ngumu. Mam' Peter alimsemesha kwa ukali na kumpiga mara kwa mara, (Wamitila, 2006:52). Huku haya yakitendeka, watoto wake Mam' Peter walimcheka na kumwimbia wimbo:

> Mtazame …mtazame… Katiwa mjinga
> Moja na moja hawezi kuunga,
> Anajua tu ugali kusonga anachekesha mjinga
> Mwangalie … mwangalie… Katiwa mchafu
> Mwili anatoa mbaya harufu
> Viguu vyake navyo vichafu
> Anachekesha mjinga…

Wimbo huu, mbali na kumsononesha Katiwa kila ulipoimbwa, unaashiria kuwa hamna yeyote katika mazingira haya anamoishi anayejali hisia zake au hata maisha yake kwa jumla. Hamna yeyote anayeweza kumkinga kutokana na hatari yoyote inayomkabili maishani mwake kama vile haki za watoto zinavyodhamiria. Zaidi ya hayo, Katiwa analazimisha kula chakula kilichomletea shida ya maumivu makali tumboni. Kwa sababu ya haya maumivu, anamwendea Mam' Peter anayemsuta kwa kumwambia kuwa:

> Huu si wakati wa kuumwa na matumbo. Huu ni wakati wa kulala. Usinisumbue tena. Kalale mara moja… (Wamitila, 2006:56).

Kitendo hiki kinazidi kudhihirisha kuwa Katiwa hapati haki ya kukingwa na hatari. Hatari zinazomkumba maishani mwake yeye kama mtoto, hususan yatima. Maneno haya yanadhihirisha kutojali kwa Mam' Peter. Kulingana na Ndungo (1998) wanajamii hutarajia mama yeyote amlee mtoto kama mamake mzazi. Mam' Peter anafanya kinyume cha haya na kumwachia Katiwa kazi nyingi za kufanya.

Johari anafanyishwa kazi nyingi bila kujali hisia zake. Kitete anakiuka hali inayothaminiwa sana katika jamii. Kama wanavyoeleza Bloom na Ottongy (1987) kuwa watoto huchukuliwa kama wanajamii wa ukoo mpana. Kulingana na kauli hiyo, watoto wana haki ya kutunzwa na kulindwa na aila zao. Dhana hii inafafanua kuwa wanajamii wana jukumu la kuwasaidia watoto ambao wana shida kama yatima.

Athari za haya yote zinaanza kuonekana pale inavyoelezwa kuwa Johari alianza kukonda huku nduguze wa kambo wakinenepa (Ng'ang'a, 2006:33). Aidha katika hadithi ya *Mama wa kambo, (*Kisovi, 2005), mhusika Pendo ambaye ni mtoto wa Zebeli alizidi kunona na kunenepa kama mbuni, huku Kalaa akiendelea kuteseka na kukonda kama sindano (Kisovi, 2005:29). Kwa hakika, hali hii inaweza kuyahatarisha maisha ya binadamu yeyote. Hata hivyo, kama walivyosawiriwa katika hadithi hizi teule, mayatima hawana kinga yoyote au yeyote wa kuwakinga kutokana na hatari hii. Hatari ya kunyimwa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na kadhalika.

Mwandishi katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), anaonyesha vile Katiwa anatolewa katika mazingira aliyoyazoea, kwa shangazi yake, na kupelekwa kuishi na babu yake ambaye mwanzo hakuonekana kumpenda Katiwa. Kwa sababu ya woga mwingi aliokuwa nao juu ya babu yake ambaye hakutaka hata kuzungumza naye, mwandishi anasema kuwa usiku huo wa kwanza, Katiwa alilala chini pamoja na mbuzi na kondoo. Asubuhi ilipofika, aliamshwa na sauti za mbuzi na kondoo hao (Wamitila, 2006:10). Kando na kazi nyingi na ngumu alizofanyishwa, mwandishi anaeleza kuwa Mam' Peter kwa upande mwingine, alikuwa akimsemesha kwa ukali. Mara kwa mara alimpiga huku watoto wake nao wakimcheka. Meier (1985) anaeleza kuwa baadhi ya walezi huishia kuwapiga watoto wao kama mojawapo ya njia za kusuluhisha mabishano bila kujali kama wakisemacho ni cha kweli au cha uwongo ili kuthibitisha uwezo wao juu ya watoto. Mam' Peter alimpiga Katiwa na kupuuza maelezo yake anapojitetea. Hata Peter anapoyamwaga maji kwenye kitanda cha Katiwa na kumsingizia Katiwa kuwa amekojoa kitandani, Katiwa anajaribu kujitetea lakini Mam' Peter anamgombeza na kumlazimisha kwenda kulianika godoro huko nje (Wamitila, 2006:52).

Katiwa aliishi katika mazingira kama ya mfungwa. Hakuruhusiwa kutoka nje wala kucheza na watoto wa majirani. Aliishia kusimama tu dirishani na kuwaangalia watoto huko nje kama ndege aliyekuwa tunduni (Wamitila, 2006:53). Zaidi ya hayo, baada ya kanisa, Mam' Peter angewanunulia watoto wake vibanzi kule madukani lakini Katiwa angerudi nyumbani pekee yake na kukaa huko kama mfungwa (Wamitila, 2006:53). Hata kama yeye ndiye aliyewatayarishia chakula, Katiwa alikula chakula tofauti na wale

wengine kwani yeye alikuwa akila makombo. Spinetta na Rigler (1972) wanasema kuwa huu ni mtindo hafifu wa kuwaadhibu watoto. Watoto wachanga kama hawa huhitaji kupewa chakula bora ili kudumisha afya yao. Mam' Peter alikuwa akimwadhibu Katiwa kwa kumnyima chakula bora kama alichokuwa akiwapa watoto wake. Huku wengine wakitazama televisheni, hususan kipindi walichofurahia sana cha vibonzo, yeye hakuruhusiwa kutazama pamoja nao bali aliketi tu huko jikoni (Wamitila, 2006:53). Chakula chake kinapoharibika na kuingiwa na vidudu vinavyoleta magonjwa, hakuruhusiwa kukitupa bali aliendelea kukila hadi kimalizike. Hali hizi zote zinafanya mazingira ya Katiwa kuwa magumu sana. Hii ni kinyume na maisha anayostahili mtoto yatima au hata mtoto yeyote yule.

Katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), mazingira anamoishi Kalaa ni yale yale. Yeye pia anaishi katika mazingira ya kufanyishwa kazi nyingi, ngumu na za lazima. Katika mazingira haya mwandishi anabainisha kuwa Kalaa aliteseka na kukonda kama sindano. Haya ni mazingira yaliyo na visa vya kusingiziwa na kuteswa. Kitete kwa upande mwingine anaufunika uovu huu ili babake Kalaa asiweze kujua vile mambo yanavyoendelea katika nyumba ile. Kwa njia nyingine, haya ni mazingira yanayomnyanyasa mtoto yatima bila matumaini ya kukombolewa. Hii ni kwa sababu kando na hali ya kuwa Kitete huufunika uovu wake huu. Tassoni (2002) akieleza kuhusu utunzaji wa watoto anaeleza kuwa watoto huwa na uhusiano bora zaidi wakiwa na wazazi wao halisi. Kalaa anakosa uhusiano bora na Kitete kwa sababu Konelia, ambaye ni mzazi wake halisi, hufanya kazi mbali. Yeye huja baada ya muda mrefu.

Haya ni mazingira ambamo yatima huyu hana uhuru wa kufanya jambo lolote kwa hiari. Hufanya tu lile aliloambiwa au kuruhusiwa kulifanya. Kwa mfano, Kalaa hana uhuru wa kuenda kuhudhuria sherehe zilizokuwa kwa mfalme. Pendo kwa upande mwingine alikubaliwa kuhudhuria hata bila kuomba ruhusa. Kalaa hana uhuru wa kujichagulia mchumba atakayemwoa ila mamake wa kambo ndiye anafanya uamuzi na kumshawishi babake Kalaa kumuunga mkono (Kisovi, 2005:47). Hata Kalaa anapomkubali kijana huyu aliyekuwa anamchumbia, alifanya hivyo tu kwa kuzingatia shida na mateso aliyokuwa akipitia na kuyapata kutoka kwa Kitete. Mazingira haya ni yale ambayo hakika yanamdhalilisha Kalaa kama mtoto yatima kwa kiasi kikubwa sana.

Katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), mtoto yatima ambaye ni Johari aliishi katika mazingira magumu sana kwani yeye pia alifanyishwa kazi nyingi na ngumu ambayo hakuifanya kwa hiari bali kwa kulazimishwa. Yeye pia hana uhuru wa kujifanyia mambo yake. Zebeli anamuamulia kuacha shule ili aendelee kufanya kazi shambani akizalisha chakula kitakachotumiwa na familia nzima. Hata anapoenda kushauriana naye Zebeli ili amruhusu kujaribu bahati yake mjini, Zebeli anamnyima ruhusa. Na wakati Johari anapofikia kufanya uamuzi wake na kufuata ushauri wake Mzee Magufuli, Zebeli anamkataa na kumfutilia mbali kama mmoja wa jamaa yake. Mazingira haya yanakuwa magumu kama mazingira ya jela na ambayo yanazibana haki za watoto, hasa watoto yatima. Zebeli anakiuka haki hii kulingana na maelezo yaliyotolewa na mwandishi kumhusu Johari.

Kulingana na nadharia ya vikale, Frye (2001), watoto yatima wamekuwa wakipitia shida mbalimbali tangu zamani. Mazingira magumu pia yamekuwepo tangu zamani. Haya mazingira magumu na shida ni vikale ambavyo vimekuwepo tangu zamani kwa mtoto yatima. Mazingira haya yanaonekana katika maisha ya Johari kabla ya kuokolewa na Mzee Magufuli.

Jambo linaloyafanya mazingira haya wanamoishi watoto yatima kuwa magumu zaidi ni kuwa hata wanapoteseka kwa hali mbalimbali ambazo zimeelezwa, watu walioko karibu na mazingira hayo hawajali. Kunao wale ambao hata wanaonekana kufurahia hali na mazingira kama hayo. Kwa mfano, katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005) mwandishi anaeleza kuwa:

> Kitete alizidisha uonevu na mateso kwa mwana huyu. Alisema vibaya kwa majirani akidai alikuwa akimwibia, lakini hakuwa na wa kumsikiliza (Kisovi, 2005:38).

Hapo awali mwandishi alieleza tofauti za kiafya zilizojitokeza kati ya Pendo na Kalaa. Ilidhihirika waziwazi kuwa Kalaa alikuwa ananyimwa lishe bora. Hata majirani walikuja kuzitambua tofauti hizi kwa mshangao.

Tassoni (2002) anasisitiza kuwa watoto wanapaswa kuwekwa katika mazingira yenye usalama ili wahisi kuwa wanatunzwa vilivyo. Jambo hili ni zaidi ya kutimizia haja zao za kila siku. Hali hii inapokuweko huchangia katika ukuaji wa mtoto. Hali hii inakosekana kwa Kalaa, na ukuaji wake unaathirika.

Hata hivyo, hakuna yeyote aliyedhubutu kuchukua hatua yoyote. Inatambulika kuwa ni wajibu wa kila mmoja wa jamii yoyote ile kuhakikisha kuwa maisha ya watoto yanatunzwa vilivyo. Aidha, jambo linaloshangaza wasomaji ni kwamba:

> Majirani walishangazwa na tofauti hizi lakini hakuna aliyetaka kuingilia boma la Konelia. walizungumza baina yao wakingojea Konelia ajigundulie yaliyokuwa yakiendelea (Kisovi, 2005:29).

Hali hii inaonyesha kuwa mazingira wanamoishi watoto yatima yamekumbwa na mikasa maradufu; kwanza, mkasa wa watoto kuishi maisha yaliyojaa mateso na pili, mkasa wa ukosefu wa uwajibikaji na jamii katika kuwatunza watoto yatima wanaoishi miongoni mwao.

Hali ni kama hii katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006). Mwandishi anasimulia kisa cha Katiwa kuchelewa kurudi kutoka dukani kwa sababu ya kile kilichompata njiani. Alikimbizwa na mtu asiyemjua hadi akaangusha na kupoteza pesa alizokuwa nazo. Pale Mam' Peter alimwangalia kwa macho makali na kumwambia kuwa anamdanganya, akamshika na kumpiga sana akimwita mwizi. Hata hivyo, mwandishi anaeleza kuwa:

> Katiwa alipigwa sana na Mam' Peter. Alishangaa kuwa watu walimwona akipigwa na hawakuja kumsaidia. Hata watoto wao walimpuuza. Jioni hiyo Peter na ndugu zake walishinda kumcheka Katiwa na kumwita mwizi (Wamitila, 2006:50).

Watoto huchukuliwa kama wanajamii, kwa hivyo wana haki ya kutunzwa na kulindwa na jamii husika. Dhana hii inafafanua kuwa wanajamii wana jukumu la kuwasaidia watoto ambao wana shida kama yatima. Katika hadithi ya *Mama wa Kambo* wanajamii hawachukui hatua yoyote kumsaidia Kalaa. Wanayaona yote anayofanyiwa na mamake wa kambo lakini wananyamaza tu. Isitoshe, katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006),

Katiwa anapopigwa na Mam' Peter hakuna yeyote anayejitokeza kumsaidia. Hii inaashiria kutowajibika kwa wanajamii.

Hata hivyo, kunazo chembe chembe za uwajibikaji hasa katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) hasa pale ambapo Bettina anaingilia maisha ya Katiwa. Bettina anazingatia msimamo wa kikundi chao cha kuhakikisha kuwa watoto wanapata haki zao. Huu ndio wakati pekee ambapo kuna juhudi za kijamii zinazolenga kuyaboresha mazingira wanamoishi yatima. Hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) ikirejelewa, hali ilikuwa tu sawia na mambo yalivyo katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), kwake Kalaa. Johari anajaribu kutetewa na jirani wakati ambapo Zebeli anamwachisha shule. Kulingana na vile mwandishi anavyoichora picha ya hali ilivyokuwa, inadhihirika kuwa majirani na wengine wote katika kijiji kile hawangefanya chochote kuonyesha uwajibikaji wao kuhusu maisha ya watoto yatima. Hata baadaye Mzee Magufuli anapomshauri Johari kujaribu maisha yake mjini, Johari anafanya hivyo. Lakini alijua kuwa angekumbana na upinzani mkali kutoka kwa Zebeli. Aidha, alijua fika kwamba hakuna ambaye angemuunga mkono katika juhudi hizi za kujaribu kuyaboresha mazingira ya maisha ya Johari.

Katika mada hii ya mazingira wanamoishi watoto yatima, jambo linalojitokeza waziwazi ni kuwa; mbali na kuwa mazingira haya yamekumbwa na mateso pamoja na ukiukaji wa haki za watoto. Mara nyingi watu katika jamii wanamoishi yatima hawaonekani wakichangamkia uwajibikaji wao kwa watoto yatima. Juhudi za makundi ya kijamii

kama lile ambalo Bettina anawakilisha zimetambuliwa, hata hivyo juhudi hizi zimesawiriwa kama zile zilizo nadra sana. Haziwafikii watoto wote wanaohitaji huduma za makundi kama haya katika jamii.

### 3.8 Hitimisho

Sura hii, imeziangazia na kuzijadili changamoto anazokumbana nazo mtoto yatima katika hadithi tatu teule. Changamoto hizi ziliangaziwa kwa kuzingatia jinsi mwandishi anavyosawiri visa na matukio mbalimbali katika mtiririko wa matukio katika hadithi. Kwa kufanya hivyo, changamoto hizo ziliweza kuainishwa katika makundi matano na zikashughulikiwa moja baada ya nyingine kwa kurejelea hadithi hizi tatu teule. Aidha, changamoto hizi zimejadiliwa kuzingatia mada kuu ya watoto kunyimwa haki zao. Nazo ni pamoja na kufanyishwa kazi nyingi na ngumu, yatima kunyimwa haki na uhuru wake, kutengwa, kubaguliwa na kutelekezwa na jamii, kutumiwa kwa mtoto yatima kama kitega uchumi na mtoto yatima kuishi katika mazingira magumu. Jambo linalojitokeza ni kuwa licha ya changamoto hizi, jamii haionekani ikiwajibika kama inavyotarajiwa. Juhudi zinazoonekana ni zile za kundi kama lile la Mama Rita ambalo pia halijaenea kote katika jamii.

# SURA YA NNE

# KUJIOPOA KWA MTOTO YATIMA KUTOKANA NA CHANGAMOTO ZINAZOMKUMBA

## 4.1 Utangulizi

Sura ya tatu ilishughulikia suala la changamoto anazokumbana nazo mtoto yatima katika hadithi tatu teule zinazoangaziwa katika utafiti huu. Changamoto hizi ziliangaziwa kwa kuzingatia jinsi mwandishi anavyovisawiri visa na matukio mbali mbali katika mtiririko wa matukio katika hadithi. Mada kuu ikiwa watoto kunyimwa haki zao. Kwa kufanya hivyo, changamoto hizo ziliweza kuainishwa katika makundi matano na kushughulikiwa moja baada ya nyingine kwa kurejelea hadithi hizi tatu teule. Sura hii imeliangazia suala la jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto anazokumbana nazo kwa kurejelea hadithi hizi tatu teule. Katika kuangazia kila hadithi, mhusika mkuu amezingatiwa jinsi ambavyo baada ya kuteswa na kukumbana na vizuizi mbalimbali katika safari yake, huweza kujiopoa kutoka kwa changamoto hizi. Katika uchanganuzi huu, kuhusiana na suala kuhusu jinsi ya kujiopoa kwa mtoto yatima, juhudi zinazotokana na ngazi mbili kuu zinazingatiwa. Ngazi zenyewe zikiwa, juhudi zinazotokana na mtoto yatima mwenyewe na ngazi ya jamii wanamoishi watoto yatima.

Jukumu kuu la mwandishi wa fasihi ya watoto ni kutoa matumaini kwa msomaji. Mpesha (1995), anaeleza kuwa mhusika mkuu katika fasihi ya watoto huwa mtoto ambaye matendo yake humpa msomaji matumaini. Isitoshe anakuwa na ujasiri katika kukabiliana

na hali ngumu zinazowakumba wakati wa kujiopoa. Kisia (1996), anasema kuwa idara za serikali, mashirika mbalimbali na hata watu binafsi huanzisha miradi ambayo hutoa huduma kwa watoto walio katika hali mbaya. Maelezeo haya humpa msomaji matumaini ya kwamba mtoto anayo nafasi ya kuopolewa. Carr & Captari (2013), wanasema kwamba ni muhimu makao ya watoto kuanzishwa ili watoto wawe na mazingira mazuri na mahitaji yao kutimizwa. Katika makao ya watoto, watoto hulindwa huku mipango ikifanywa ya kuwasaidia kuendeleza maisha kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano, katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) tunamwona Katiwa akiwa amekumbwa na matatizo mengi yanayotokana na hali yake ya kuwa yatima kufikia kiwango cha kuelekea kukosa matumaini maishani. Hata hivyo, kupitia kwa mhusika Betina, mwandishi anamrejeshea Katiwa matumaini katika maisha yake pale anapomchukua kutoka kwa mwajiri wake, Mam Peter, aliyekuwa anamtesa na kumrejesha kwa babu yake. Babu yake aliyeishi kijijini Masira alimchukua na kumpeleka shuleni kuendelea na masomo yake. Vile vile, katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) mwandishi anamrejeshea msomaji matumaini katika maisha ya Johari kupitia kwa mzee Magufuli. Mzee Magufuli alimwopoa Johari kutoka kwa mamake wa kambo aliyekuwa anamtesa. Alimpeleka mjini kwa mwanawe Ezekia alikojifunza kazi ya umakanika na kisha akaanza kujitegemea maishani.

Kulingana na nadharia ya vikale, Frye (2001) wahusika wanaoopoa yatima wana uwezo wa kuhisi jambo haraka. Wana sifa za maadili mema kama vile ukarimu na wako tayari kusaidia wakati wowote.

### 4.2 Kujiopoa kutokana na kazi nyingi na ngumu

Katika hadithi ya *Yatima* (Wamtilia, 2006), Katiwa ambaye ni mhusika mkuu anajiopoa kutokana na kazi ngumu kwa njia ya ujasiri. Mwandishi anasema kuwa:

> …ilikuwa vigumu kuamini kuwa Katiwa alikuwa na ushujaa wa kusimama pale usiku ule. (Wamitila, 2006: 63)

Ni kupitia kwa ujasiri wake ambapo anaopolewa. Ujasiri huu unadhihirika wakati ambapo Katiwa anastahimili baridi usiku kucha mle kibandani anamolala mlinzi wa lango kuu. Kulipokucha, mlinzi alipata nafasi ya kumpeleka kwa Bettina ambaye alimsaidia baadaye.

Kupitia kwa ujasiri, yatima anaweza kuepuka mateso au madhila ambayo hupitia. Ni vyema ieleweke kwamba kama yatima hawezi kujijasirisha yeye mwenyewe, hawezi kujiopoa. Ni juhudi zake mwenyewe ambazo zinaweza kumfungulia ukurasa mpya wa maisha.

Njia hii ya kujiopoa pia inaonekana kudokeza kwenye kisa kile cha nyanya, katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), alichowasimulia Katiwa na Mule, kisa cha wasichana na gogo. Kisa hiki kinaashiria visiki maishani. Visiki ni shida zilizo katika maisha. Ili kuepukana na shida hizi, ni muhimu kuwa na ujasiri na ushujaa. Katiwa anadhihirisha hili anapostahimili baridi ya usiku wote mle alimokesha kibandani mwa mlinzi. Kutokana na ujasiri huu, aliweza mwishowe kujiopoa kutoka kwa mateso ya Mam' Peter, aliyekuwa mwajiri wake.

Mwanzoni kabisa mwandishi anaeleza kuwa Katiwa alishindwa kuelewa ni kwa nini hakuenda shule kama watoto wengine. Hii inadhihirika kupita kwa dondoo hili:

> "Kwa nini mimi siendi shuleni?"(Wamitila, 2006 : 48)

Katiwa anamuuliza mwajiri wake Mam' Peter ambaye watoto wake walienda shule huku Katiwa akibaki nyumbani. Katiwa alikuwa anawazia kuhusu hali yake, ni kupitia kwa mawazo haya ndipo alipopata msukumo wa kujiopoa.

Katika *Mkataba wa Watoto* (2001), kila mtoto ana haki ya kupata elimu ya msingi ya bure. Katiwa amenyimwa haki hii. Baadhi ya wanajamii huwachukulia yatima kama viumbe tofauti na hivyo kuwanyima haki zao. Watoto yatima kama watoto wengine hawastahili kunyimwa haki na uhuru wa kufanya mambo kama wanajamii wengine.

Kisa cha Johari na Mzee Magufuli katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) kinaonyesha jinsi Johari alivyojiopoa kutokana na kazi ngumu shambani na nyumbani kwa Zebeli. Johari anaonyesha ujasiri kwa kuchukua hatua ya kuondoka nyumbani. Zebeli alikuwa amemtahadharisha kuwa hangemkubali hapo nyumbani tena kama angeufuata ushauri wa Mzee Magufuli. Mwandishi anaeleza kuwa:

> …kwa kuwa mamake wa kambo hangemruhusu Johari kuchukua chochote nyumbani, Mzee Magufuli alimpa pesa za kununulia nguo zingine… (Ng'ang'a, 2006 :40)

Dondoo hili linaonyesha vile Johari alikuwa jasiri katika kufanya uamuzi wake. Haikuwa rahisi kwake kuondoka baada ya kuambiwa kuwa hangekubalika tena nyumbani kwao. Isitoshe, alinyimwa nafasi ya kuchukua chochote pale nyumbani. Johari aliamua kuenda

hata baada ya kupewa masharti hayo yote. Alitumia uwezo wake mwenyewe kuwa jasiri na kuamua kuondoka.

Aidha, motifu ya safari ni kipengele muhimu sana katika maisha ya yatima. Kwa mujibu wa Melanie, (1999), ili yatima ajiopoe kutokana na changamoto anazokumbana nazo ni lazima aondoke mahali hapo penye shida ili aende kutafuta usalama. Judy (1999) anasema kuwa yatima huwa na msukumo ambao humhimiza kuondoka bila kujali vizuizi na kwenda kwingine ili apate kile ambacho kitamridhisha na kumfanya mkamilifu. Ni kweli kuwa kuondoka kwa Johari kulimfungulia ukurasa mpya katika maisha yake. La muhimu ni kujua kwamba ni yeye mwenyewe aliyefanya uamuzi baada ya kupewa ushauri na Mzee Magufuli.

Kwa hivyo, safari ni njia moja ya yatima kujiopoa kutokana na kazi ngumu na nyingi. Kulingana na nadharia ya vikale, Frye (2001), safari katika hadithi au kule kuondoka ni kikale. Yatima tangu zamani ni lazima angeondoka ili aende kutafuta usalama. Katika safari, yatima hukumbana na vikwazo lakini mwishowe hushinda. Mara nyingi baada ya safari, maisha ya yatima hubadilika. Kulingana na Melanie (1999), mhusika yatima hutengwa na kuteswa na walezi wake. Mateso haya humfanya kufunga safari ili kuondokea mateso. Yatima hupata utambuzi wa nafsi yake kutokana na kupambana na vizuizi katika safari hiyo na mwishowe anarudi mahali pa raha. Pengine pale pa asili au mahali pazuri zaidi.

Katika hadithi zilizoteuliwa, Kalaa anajiopoa kutokana na kazi nyingi na ngumu kwa kukubali kuondoka na kwenda na Baraka (Kisovi, 2005). Katiwa naye anajiopoa kwa kuondoka japo usiku wa manane bila kujua anapokwenda. Alistahimili baridi usiku kucha na hakuogopa giza hadi alipofanikiwa kupata usaidizi. Vikwazo njiani mwake havikumzuia kuendelea na safari yake, (Wamitila, 2006). Johari naye (Ng'ang'a, 2006), anafanya uamuzi mgumu wa kutoka kwao na kuacha familia yake. Safari ya kuenda kwa Ezekia mwanawe Mzee Magufuli kule mjini inamfanya ajiopoe kutokana na kazi nyingi na ngumu.

Katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), Kalaa anafuata ushauri wa mama yake wa hapo awali, anamwomba Mungu amsaidie kuepukana na madhila anayopitia. Mwandishi anadhihirisha kuwa;

> Kitete alianza kumfanyiza kazi nyingi. Alimtaka kuamka jogoo la kwanza kuandaa kiamsha kinywa na kuwapashia moto maji ya kuoga…'Kabla unywe chai ni lazima ufue nguo na kuzianika'. Alimfanya Kalaa kuwa mtumishi wake. (Kisovi, 2005)

Kalaa anajiopoa kutoka kwa kazi nyingi na ngumu kwa kufanya uamuzi dhabiti anapokutana na mwana wa mfalme wa Ughaibuni. Jina la kijana huyu lilikuwa Baraka. Ni kweli kwamba Baraka alileta baraka na nafuu kwa Kalaa. Mara nyingi katika jamii mayatima hufanikiwa kupata maisha mazuri baada ya mateso wanayopitia. Kalaa anapokubali kuolewa na Baraka, inakuwa njia moja ya kufungua ukurasa mpya maishani mwake. Maisha ya dhiki na majonzi yanafika kikomo.

Kwa ufupi, imebainika kupitia kwa uchanganuzi huu kuwa mtoto yatima anaweza kujiopoa kutokana na mateso anyopitia kwa kutumia sifa fulani za kibinafsi. Sifa hizi ni kama vile kuwa jasiri na kufanya uamuzi dhabiti. Hata hivyo, inavyojitokeza ni kwamba, mtoto yatima anayo nafasi finyu sana ya kujiopoa yeye mwenyewe pasipo na kusaidiwa na hali fulani au watu wengine walio karibu naye. Kufuatilia hili, sehemu itakayofuata itaangazia jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba kupitia kwa kusaidiwa. Ahmed (2012), anasema kuwa ni jukumu la jamii kuhakikisha kuwa watoto hawadhulumiwi. Jamii inafaa kuhakikisha kwamba watoto wanaenda shule ili wawe na maisha mema baadaye. Kwa njia nyingine, baada ya kuangazia jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kwa ngazi za kibinafsi, sehemu inayofuata itaangazia jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba kupitia juhudi za kijamii.

### 4.3 Kujiopoa kutokana na kunyimwa haki na uhuru

Kutokana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa haki za Kibinadamu (1948), pamoja na kipengele cha sheria ya watoto ya mwaka wa 2001, watoto wote wana haki zao. Haki hizi ni muhimu zizingatiwe. Kwanza kabisa tuna haki ya elimu. Aidha kuna haki ya kukingwa kutokana na hali zote zinazoweza kutisha hali yao ya maisha bora.

Matukio au visa mbali mbali vimeangaziwa katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006). Visa hivi vinaashiria kujiopoa kwa mtoto yatima kwa shida zinazotokana na jamii anamoishi. Katiwa ni mhusika mkuu na yatima katika hadithi hii. Ni dhahiri kwamba amepitia mateso mengi yakiwemo kunyimwa haki ya elimu, kuishi katika mazingira

magumu, kudhalilishwa, kutumikishwa, na mengine mengi. Hata hivyo, kuna watu walio karibu naye kama vile; watoto wa shangazi yake Kevin na Maria, watoto wa Mam' Peter na hata majirani hasa anapoishi na Mam' Peter. Watu hawa hawamsaidii kujiopoa kutokana na mateso haya.

Kwa mujibu wa nadharia ya vikale, Frye (2001) wasaidizi huwa ni watu wa karibu ambao hushuhudia madhila watoto yatima hupitia. Wasaidizi hawa hawachelewi kusaidia yatima kwa vyovyote vile. Huhakikisha kwamba mtoto yatima amefaidika kwa juhudi zake.

Katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), Mam' Peter anamsingizia Katiwa kuwa ni mwizi. Anampiga hadi kumtupia nguo zake kule nje. Kulikuwa na giza jingi lakini mlinzi wa pale langoni anamjia na kumsaidia kwa kumpa Katiwa mahali pa kulala katika kijumba chake kidogo. Mlinzi aidha anampa koti lake kubwa ili ajifunike. Mlinzi hakupendezwa na kitendo alichofanya Mam' Peter inavyobainishwa hapa:

> Hawa wanawake sijui ni nini shida yao. Wanatesa watoto wa watu kama wanyama… (Wamitila, 2006:64)

Mlinzi kama mwanajamii anayejali anamsaidia Katiwa. Ni jukumu la wanajamii kuwasaidia yatima hasa wale ambao wanadhalilishwa. Wanajamii wanastahili kuhakikisha kwamba watoto yatima wanapata mahitaji yao ya kimsingi. Ni muhimu wahakikishe kwamba watoto yatima hawanyimwi haki ya uhuru katika mazingira wanamoishi.

Aidha, jamii inastahili kuelewa kuwa watoto hawa pia ni wanajamii na vizazi vya siku za usoni. Ni jukumu la jamii pia kuhakikisha kuwa maisha ya watoto yatima yameshughulikiwa.

Mwandishi anaeleza kuwa Katiwa alipokuwa kule nje baada ya kufukuzwa na Mam' Peter, anakutana na Bettina kwa mara ya kwanza. Bettina anambembeleza na kumuuliza kama alikuwa anahisi njaa, Katiwa anapokubali mwandishi ameeleza kuwa:

> Aliutia mkono wake katika mfuko aliokuwa nao na kutoa maandazi mawili na kumkabidhi Katiwa. Katiwa alishukuru… (Wamitila, 2006:55)

Baadaye inaelezwa kuwa Bettina alimwambia Katiwa kuwa akiwa na shida yoyote, asione ugumu kumwendea na kumweleza. Bettina anakuwa mwanajamii wa kwanza kumwopoa Katiwa kutokana na shida ya njaa. Ni dhahiri kwamba kunao wanajamii ambao walifanya juhudi ya kumwokoa Katiwa kutokana na madhila yake.

Kupitia kwa Bettina, Katiwa anasaidiwa kutokana na hali ya kutojua kusoma na kuandika. Katiwa anasaidiwa na watoto wa Bettina kujifunza kusoma na hata kuhesabu. Hii inadhihirisha kuwa Katiwa alisaidiwa na Bettina pamoja na watoto wake katika kujiopoa kutokana na kunyimwa haki ya elimu. Aidha, kinyume na ilivyokuwa nyumbani mwa Mam' Peter, mwandishi anaeleza kuwa Katiwa alikuwa na uhuru wa kutazama televisheni na watoto wengine na hata kucheza nao (Wamitila, 2006:69).

Maelezo yanaonyesha kuwa Katiwa alipokuwa akiishi na Bettina alikuwa huru na hakuna chochote ambacho alinyimwa. Hivyo basi ni wazi kwamba Bettina na watoto wake ni baadhi ya wanajamii ambao wanasaidia watoto yatima katika kujiopoa kutokana na changamoto zinazowakumba.

Kupitia kwa ujuzi wake, Bettina anamsaidia Katiwa kwa kumshawishi msichana wa kazi kumuuliza shangazi kwa ujanja kilikokuwa kijiji cha Masira. Alifanya hivi ili ampeleke Katiwa kwa babu na nyanya yake. Hatimaye Bettina anafaulu kujua kiliko kijiji cha Masira na kumpeleka Katiwa huko kwa gharama yake. Wanapofika huko, kinyume na ilivyokuwa mara ya kwanza, mwandishi anaeleza kuwa:

> Babu alifurahi sana kumwona mjukuu wake. Alimsalimu kwa furaha kubwa… (Wamitila, 2006:72)

Kinyume na ilivyokuwa mara ya kwanza, Katiwa kwenda kuishi na babu yake, mara hii babu yake anamfurahia na kumkaribisha kwa uchangamfu. Mtazamo wake kwake Katiwa unaonekana kubadilika kabisa kiasi kwamba mara hii, anadhamiria kumkinga mjukuu wake na uovu wowote ambao amekuwa akiupitia. Inaelezwa kuwa:

> …babu alisema kwa sauti ya juu, 'Mimi sitamruhusu mjukuu wangu atoke huku tena!... Mjukuu wangu atasoma huku huku Masira. Mimi nina mbuzi, kondoo, na ardhi kubwa. Nitawauza mbuzi na kondoo au hata ardhi ili apate mahitaji ya shule! (Wamitila, 2006:73)

Maneno haya ni dhihirisho tosha kuwa babu sasa yuko tayari kumwopoa Katiwa kutokana na changamoto za kukosa masomo na kukosa malezi mazuri. Yamkini, kwa maneno ya babu yake Katiwa, 'haki ya mtu haipotei…' (Wamitila, 2006: 74), mwandishi anaendelea kueleza:

> Katiwa aliendelea kuishi na babu na nyanya na mwaka ulipoanza, aliingia shuleni pamoja na rafiki yake Mule. Babu naye aliwauza mbuzi na kondoo kadhaa wake kwa ajili ya kununua sare. (Wamitila, 2006: 82).

Katiwa na Mule walisoma kwa bidii sana na baada ya kipindi kifupi wakawa wanafunzi bora shuleni. Walisifiwa sana na walimu wao kwa kazi yao nzuri.

Kupitia kwa matukio haya yote kama yalivyosimuliwa, inaweza kuhitimishwa kuwa maisha ya Katiwa yalibadilishwa na Bettina na watoto wake, mlinzi na babu yake. Kama walivyosawiriwa katika hadithi hizi teule, wanajamii hawa wanachangia pakubwa sana katika kuopolewa kwa Katiwa kutokana na changamoto za kunyimwa haki na uhuru. Mlinzi anawakilisha ujirani mwema na uwajibikaji unaohitajika katika jamii ili kuwatunza watoto vyema. Bettina naye anawakilisha ujirani mwema pamoja na jukumu la mashirika ya kijamii yanayoshughulika kuhakikisha kuwa watoto, hasa yatima, wanapata haki yao bila kunyanyaswa wala kubaguliwa. Watoto wa Bettina nao wanawakilisha uwajibikaji, ukarimu na mapenzi yanayohitajika kwa yeyote anayeishi nao. Babu naye, hasa mara ya pili Katiwa anaporudi kuishi naye, amesawiriwa kudhihirisha uwajibikaji halisi wa jamaa walioachwa na watoto yatima na walio walezi wao.Watu hawa ni wana jamii ambao wamejitolea kumsaidia mtoto yatima kujiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba. Changamoto ambazo zimeangaziwa katika sehemu hii ni za kunyimwa haki na uhuru. Juhudi za wanajamii hawa zinadhihirisha uwajibikaji ambao unamsaidia mtoto yatima kuepuka na hali ngumu ya maisha.

Katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), jamii anamoishi yatima inaonyesha uwajibikaji halisi. Jamii iling'amua kuwa Johari alikosa uhuru akiwa kwa Zebeli, mama yake wa kambo. Aidha alikosa haki ya kupata elimu ambayo ilikuwa aali katika maisha yake. Akiwa amemtazama Johari kwa muda fulani, Mzee Magufuli, ambaye ni jirani yake, alitambua kuwa Johari alikuwa kijana mwenye bidii. Hivyo basi alianza kuwaza vile ambavyo angeweza kumwopoa Johari kutokana na changamoto zinazomkumba. Katika uzungumzi nafsia, anasema kuwa:

> Huyu ni kijana ambaye ana akili shupavu na hafai kuyapoteza maisha yake bure hapa shambani. Hapa hataweza kujiendeleza. Ataishia kuwalisha mamake wa kambo na wanawe bila yeye mwenyewe kunufaika… (Ng'ang'a, 2006: 37)

Usemi huu unaashiria azimio la Mzee Magufuli kumwopoa Johari. Kulingana na nadharia ya vikale, Northrop (2001), huyu mzee ni mhusika anayetokea wakati ambapo nguli yuko katika hali zisizokuwa na matumaini na za kukata tamaa. Ni mzee mwenye uwezo wa kuhisi jambo haraka. Ana sifa za maadili mema kama vile ukarimu na kila wakati yuko tayari kusaidia. Mzee Magufuli alihisi hali ya Johari haraka.

Huu ndio unakuwa mwanzo wa kujiopoa kwa Johari kupitia kwa jamaa au wale waliomo katika mazingira anamoishi. Mzee Magufuli kwa ukarimu wake anampokeza Johari kwa mwanawe Ezekia. Ezekia anatokea kuwa mwokozi wa pili wa Johari baada ya babake Mzee Magufuli. Ezekia anaonekana mwenye nia nzuri aliye tayari kabisa kumsaidia Johari. Hii inadhihirika anapomwambia Johari kuwa:

> Nataka utie bidii katika kujifunza kazi ya umakanika na pia udereva. Ukishajua kazi, wewe ndiwe utakayesimamia gereji. Sitaki ujisumbue kwa

> chochote. Kila utakachohitaji, usione ugumu kuniitisha mimi… (Ng'ang'a, 2006: 43)

Wanajamii hawa wawili wanamsaidia Johari kujiopoa kutokana na changamoto ya kunyimwa haki ya uhuru. Mzee Magufuli anampata Johari katika hali ya kutamatisha. Anampa ushauri ambao unamfaidi na hivyo, anaanzisha ukurasa mpya wa maisha yake. Magufuli na mwanawe Ezekia aidha wanamsaidia Johari kujiopoa kutokana na changamoto za kukosa pa kuenda, kufanyishwa kazi ngumu na kuachishwa na kunyimwa haki yake ya masomo. Wawili hawa wanamwopoa na kumwonyesha njia mbadala ya kujikimu kimaisha. Hata kama hakuenda shuleni tena, alipata mafunzo ya umakanika kupitia kwa Ezekia. Johari anatokea kufaulu katika taaluma ya umakanika na kurudi kuisaidia familia yake iliyomdhulumu hadi kumtelekeza. Mbali na mzee magufuli na mwanawe, juhudi za wanajamii kusaidia yatima zinaonekana pia kupitia kwa mama jirani. Mama huyu anamwambia Zebeli kuwa:

> "Mama Wakesho, mwache Johari asome. Siku hizi hakuna urithi ulio aali kama elimu…" (Ng'ang'a, 2006: 35).

Dondoo hili linadhibitisha kuwa Johari ana changamoto ya elimu na uhuru wa kufanya vile inavyompendeza. Mwandishi anaendelea kueleza kuwa:

> Johari alijaribu kumsihi mamake wa kambo amwache aendelee na masomo lakini maombi yake yaliambulia patupu (Ng'ang'a, 2006: 35)

Ni dhahiri kwamba Johari alikuwa amenyimwa haki ya masomo. Jambo ambalo lilimhuzunisha sana kwa sababu aliyapenda masomo. Mama jirani anajaribu kumsaidia Johari ili apate haki yake ya masomo lakini mamake wa kambo anakataa katakata. Johari mwenyewe pia kama mwanajamii anaelewa umuhimu wa masomo. Anamsihi mamake wa kambo amwachilie aendelee na masomo lakini anakataa kubadilisha msimamo wake.

Kupitia kwa matukio yaliyojadiliwa yote ni wazi kuwa maisha ya Johari yalibadilishwa na Mzee Magufuli na mwanawe Ezekia. Wanajamii hawa wanawakilisha ujirani mwema na ukarimu unaohitajika katika jamii. Mzee Magufuli anatoa ushauri mwafaka ambao Johari anafuata na kujiopoa kutokana na changamoto zilizomkumba. Ezekia kwa upande mwingine anakuwa mkarimu sana kwa Johari, anakuwa mwalimu wake na mshauri mkuu. Kupitia kwa wanajamii hawa Johari anapata kujiopoa kutokana na changamoto ya kunyimwa haki na uhuru. Mbali na hawa wawili, kuna jirani mmoja ambaye alimshauri Zebeli kumwacha Johari aendelee na masomo. Hii inadhihirisha kwamba jamii inaelewa umuhimu was masomo kwa mtoto yeyote yule. Kwa hivyo mtoto anapopatikana kwamba hapati haki hii au amenyimwa haki hii, jamii inaingilia kati mara moja ili suluhu ipatikane. Jirani huyu alionyesha kuyajali maslahi ya mtoto yatima katika jamii. Aidha watoto wa Ezekia; Mishele na Yohana walimpenda sana Johari na kumheshimu wakati aliishi nao. Hii ni njia moja ya kumsaidia yatima kuishi katika mazingira ambamo anakubalika na huru.

### 4.4 Kujiopoa kutokana na Kutengwa na Kubaguliwa

Katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005) Kalaa ambaye ni mhusika mkuu na yatima anakumbuka mambo aliyoambiwa na mama yake akiwa na umri mdogo. Alimwambia kuwa kumcha Mungu ndicho kingekuwa chanzo cha maarifa. Kwa maneno halisi ya marehemu mamake:

> ‘Aliyeongolewa na Mungu hapotoki’ (Kisovi, 2005: 35)

Inadhihirika kwamba chanzo cha kujiopoa kwa Kalaa ni kuwa alifuata ushauri wa mamake na hivyo inaelezwa kuwa:

> 'Alimwomba Mungu amsaidie na kumpa chakula cha kila siku…'
> (Kisovi, 2005: 35).

Hapa ndipo Kalaa anaanza safari yake ya kujiopoa kutokana na changamoto ya kutengwa na kubaguliwa. Kalaa alipimiwa chakula kama dawa na Kitete aliye mamake wa kambo, na hata wakati mwingine ananyimwa kabisa. Siku moja Kalaa alisikia sauti ikimshauri kuimba wimbo fulani kila alipohisi njaa.

> 'Na pale angeona meza ikitokea ikiwa imeandaliwa kila aina ya chakula;
> (Kisovi, 2005: 36)

Chakula kilitokea kiajabu na kwa njia hii, Kalaa anajiopoa kutokana na shida ya njaa, Matokeo yake yakawa kama mwandishi anavyoeleza:

> Mara mabadiliko yalianza kutokea katika maumbile yake. Alianza kuongeza uzito na ngozi yake ikaanza kung'aa kwa shibe. (Kisovi, 2005: 36).

Kalaa anabaguliwa kwa kunyimwa chakula ilhali Pendo, dadake wa kambo, anapewa chakula na Kitete ambaye ni mama yake mzazi. Lakini Kalaa kulingana na kauli iliyotolewa, ameshajiopoa kutokana na minyororo ya kunyimwa lishe kwa njia ya kimuujiza. Hali hii ya kujiopoa kimiujiza inaibua mihimili ya vikale ambapo mtoto aliye katika mateso huweza kuopolewa kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Kitete anajaribu juu chini kumdhalilisha Kalaa lakini juhudi zake zinaambulia patupu. Kwa mara nyingine, kupitia kwa njia hii, Kalaa anajiopoa kutokana na kutengwa na kubaguliwa ambapo chanzo chake ni wivu na ubinafsi wa Kitete. Kalaa, anabaguliwa wakati Kitete alianza kumtenga na Pendo. Mara nyingi alimwambia Kalaa kuwa:

"Sitaki ucheze na Pendo. Utamchafua!" (Kisovi, 2005:28)

Kauli hii inaweza kumwathiri Kalaa vibaya sana kwani hakuwa na mtoto mwingine ambaye alikuwa ndugu wake wa kambo. Utengano huu ulimvisha Kalaa upweke hata akatamani kama mamake angekuwa hai kwani angemwepusha na mateso haya.

Aidha wakati ambapo Kitete anabishana na Konelia, babake Kalaa, kauli ya Konelia inaonyesha Kalaa kuwa alikuwa amebaguliwa.

> KONELIA: Sikujua kwamba unaweza kuwabagua wana. Kalaa angali mtoto kumbuka… (Kisovi, 2005: 32).

Mwandishi anaeleza kuwa:

> Kalaa alipiga magoti na kumlilia Mungu, mara tu alijipata amezungukwa na mapambo ya aina nyingi. Anavalia na kupendeza ajabu. (Kisovi, 2005: 42)
>
> Urembo wa Kalaa unamvutia hata mfalme ambaye anakiri kuwa hakuwa ameuona urembo kiasi kile (Kisovi, 2005: 44).

Mtoto yatima katika jamii mbali na kuopolewa na wanajamii, anaweza kuopolewa kupitia kwa miujiza na maombi, hizi mbili zikiwa njia zinazoambatana na mihimili ya nadharia ya vikale. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, ni dhahiri kwamba Kalaa anaopolewa kutokana na kutengwa na kubaguliwa kupitia kwa miujiza. Nguvu za ajabu zinamsaidia Kalaa kujiopoa kutokana na mateso anayoyapitia. Kuopolewa kwa njia hii ni kikale ambacho kimekuwako tangu zamani katika jamii. Kupitia kwa njia hii ya kuopolewa, mambo ambayo hutokea huwa ni matukio ya kihalisi ambayo yamevamiwa na jambo ambalo ni la ajabu mno na ni vigumu kuaminika. Wanajamii hawawezi kuyazuia matukio haya wala kuelewa vile yanavyotokea. Matukio haya humfaidi yatima kama

ilivyoonyeshwa katika maelezo. Mara nyingi yatima anapokosa mtu wa kumsaidia katika jamii, huokolewa kwa njia hii ya miujiza.

Kalaa anaopolewa kutokana na kutengwa na kubaguliwa kwa njia hii. Mamake wa kambo anajaribu kuchunguza ili apate kuelewa kinachoendelea lakini hafaulu kwa sababu anayemsaidia Kalaa ana uwezo kumshinda.

Hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) mhusika mkuu Katiwa ametengwa na kubaguliwa na familia ya Mam' Peter. Katiwa hakuruhusiwa hata kutoka nje inavyoonyeshwa katika kifungu hiki:

> Alitamani kutoka nje na kucheza na watoto wa majirani au hata kuota jua na kucheza mwaficho lakini hakupewa ruhusa. Mara nyingi aliishia kusimama dirishani na kuwaangalia watoto huko nje kama ndege aliyekuwa tunduni (Wamitila, 2006: 53).

Maelezo haya yanabainisha kuwa Katiwa alikuwa ametengwa na mambo mengi ambayo msichana wa umri wake angefurahia kufanya. Kutengwa huku kunamwathiri sana Katiwa kwani msichana wa rika lake angefurahia kutoka nje, acheze, aote jua na hata kutambiana hadithi. Isitoshe, Katiwa hakuruhusiwa kula pamoja na wengine kwenye meza; alikuwa akila chakula chake ambacho kilikuwa tofauti na cha wengine jikoni. Aidha Katiwa hakuruhusiwa kujumuika na watoto wa Mam' Peter kutazama vipindi vya vibonzo au katuni katika televisheni. Siku moja Mam' Peter alimwambia:

> "Wewe huna ruhusa ya kutazama televisheni! Hujui maana yake!" (Wamitila, 2006:53)

Yatima anapotengwa hujihisi pweke na huathirika kisaikolojia. Yatima kama watoto wengine anaweza kuwa na talanta ambayo inaweza kutambulika kama anajumuika na watoto wengine au wanajamii wengine. Anapotengwa, talanta yake haiwezi kukuzwa kwa hivyo inapotea. Talanta ambayo ingekuwa ya manufaa kwa jamii na taifa kwa jumla inaishia kupotea na kutomsaidia yeyote.

Katiwa anajiopoa kutokana na kutengwa na kubaguliwa kupitia kwa matumaini aliyokuwa nayo. Matumaini kwamba mambo yanaweza kubadilika. Baada ya shida hizi zote, Katiwa, katika chumba chake usiku, alipata ndoto ya ajabu. Aliona mwangaza mkubwa ukitokezea dirishani. Akamwona nyanyake kama amevalia mavazi meupe na kuota mabawa meupe pia. Katiwa alipomwangalia alimwita kwa mkono.

Kwa mujibu wa nadharia ya vikale, Northrop (2001), mwanga huashiria hali ya matumaini, nuru na kufanya upya. Ndoto hii inaonyesha kwamba Katiwa anatarajia kupata nuru na matumaini mapya. Shida anazozipitia za kubaguliwa na kutengwa zinastahili kuisha ili aanze maisha mapya yasiyokuwa ya ukiwa. Ndoto hii ilikuwa mwanzo wa kujiopoa kwake. Siku iliyofuata baada ya ndoto hii, Katiwa alisingiziwa wizi na kufukuzwa usiku. Katiwa aliishia mikononi mwa Bettina ambaye alijaribu kwa vyovyoye vile hadi akapata kijiji wanakoishi babu na nyanya yake Katiwa.

Nadharia ya uhalisia inasisitiza usanii wa matukio katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Matukio haya huwasilisha kweli kama ulivyo katika mazingira. Jamii

haikosi watu wenye huruma kama Bettina. Kujitolea kwake katika kumshughulikia Katiwa ni tukio la kawaida na halisi katika jamii. Jamii haikosi watu ambao huchukua hatua wakiona mambo yakienda vibaya. Bettina anaelewa kuwa tabia ya kuwatenga na kuwabagua watoto yatima ni kinyume na maadili ya jamii. Hivyo basi, anamchukua Katiwa na kumpeleka kwake nyumbani ambako anajumuika na watoto wake ambao wanamwonyesha mapenzi ya dhati. Ni wazi kuwa watoto wa Bettina wanaelewa kuwa mtoto yeyote, awe yatima au asiwe ana mchango wake katika maendeleo ya jamii, na kamwe hastahili kutengwa wala kubaguliwa. Ndiposa wanakuwa kati ya wale wanaompa Katiwa matumaini. Kwa hivyo wanamsaidia katika kujiopoa kutokana na dhiki yake.

Johari katika hadithi ya *Mateso Ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) ametengwa na kubaguliwa na Zebeli mamake wa kambo. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Johari angepewa kazi ya kujaza pipa zima la maji jioni baada ya kutoka shuleni. Wakati huo watoto wa Zebeli wangekuwa wakicheza. Johari alipimiwa chakula kama dawa. Nao wanawe Zebeli walilishwa mapochopocho…Mara nyingi, wanawe Zebeli wangelishwa mayai na kunywa maziwa huku Johari akila chakula cha maharagwe yenye viwavi. (Ng'ang'a, 2006: 32).

Dondoo hili linadhihirisha ukweli kwamba Johari alikuwa amebaguliwa na familia ya Zebeli. Ni muhimu kufahamu kuwa Johari hata kama hakuwa amepata mtu wa kumwokoa wakati huu, inaelezwa kwamba alimwomba Mungu sana kila siku kabla ya kulala. Maombi haya yalikuwa njia moja ya kutaka kujiopoa kutokana na dhiki iliyomwandama kila siku. Utengano unazidi kubainika baina ya Wakesho, dadake wa kambo, anapomwambia Johari:

> 'Pasahau hapa na usipaite nyumbani tena!' (Ng'ang'a, 2006: 29)

Maelezo haya yanaonyesha kwamba Johari ametengwa na nyumbani kwao. Isitoshe, mwanzo wa barua unaonyesha ubaguzi; dadake ameanza barua kwa, 'Johari Debora' – anamwita kwa jina la marehemu mamake wala si la babake. Hii inadhihirisha kwamba hawataki kuwa na uhusiano naye. Zebeli katika dondoo hili anadhihirisha kutengwa kwa Johari:

> "…hatumhitaji tena hapa. Arudi huko huko alikofikiria ndiko nyumbani. Ajue kuwa hapa hapana chochote chake.Mararu yake niliyachoma yote moto…" (Ng'ang'a, 2006: 56).

Tukio hili linatokea wakati ambapo Johari anarudi nyumbani mara ya kwanza baada ya kuenda mjini. Alikataliwa na familia yake, akafukuzwa na hata akaitwa mhuni. Ezekia, mwanawe Magufuli, ndiye anayemwopoa kutokana na changamoto hii ya kubaguliwa na kutengwa. Anamkaribisha kama mmoja wa familia yake jinsi inavyodhihirika hapa:

> Johari usijali, nataka kuanzia leo ujihisi kuwa mmoja wetu katika familia hii. Kazi ya mshahara hutafanya tena. Nataka tufanye kazi kama yetu… (Ng'ang'a, 2006: 58).

Maelezo haya yanaonyesha kuwa Ezekia amemkaribisha Johari kuwa kama mmoja wa familia yake. Johari anaanza maisha mapya na familia ya Ezekia. Maombi ambayo alikuwa anaomba kila siku yanajibiwa kwa kuopolewa na hapo basi kudhihirisha mojawapo wa mihimili ya nadharia ya vikale .

Jamii tunamoishi mna watu ambao ni wakarimu, watu walio tayari kusaidia bila kulipwa chochote. Ezekia ni mfano mzuri wa watu hawa. Anatoa ukarimu huu kwa babake mzazi, Mzee Magufuli, ambaye ni kielelezo chema kwake. Ni wajibu wa jamii kuhakikisha kwamba kila mtoto analindwa na kupata mahitaji yake ya kimsingi. Hii ni kwa sababu

jamii ina uhusiano wa karibu sana na yatima, huwa inashuhudia changamoto anazopitia. Aidha jamii huweza kutambua uwezo wa yatima na hivyo kupata njia ya kumwopoa kwa urahisi. Ezekia baada ya kuwa na uhusiano wa karibu na Johari, aliweza kugundua kuwa ni kijana mwenye bidii na anao uwezo wa kufanya kazi vizuri na hata kuwavutia wateja. Mwishowe alimfanya mmoja wa familia yake na hivyo wakafanya kazi pamoja.

Johari anajiopoa kutokana na changamoto zake kupitia kwa bidii yake ambayo ilimpendeza Ezekia na hivyo akachukua hatua ya kumsaidia. Kulingana na nadharia ya vikale, yapasa nguli atoke nyumbani, asafiri hadi eneo asilofahamu, avumulie hali ngumu, akifikie alichokuwa akitafuta, apate ujuzi mpya na arudi nyumbani na ujuzi huo ili awasaidie wengine katika jamii yake. Haya yote yanadhihirika katika maisha ya Johari. Anajiopoa kutokana na kutengwa na kubaguliwa baada ya kuondoka akaenda mjini, akapata ujuzi kisha akasaidia familia yake na jamii kwa jumla.

### 4.5 Kujiopoa kutokana na Kutumiwa kama Kitega Uchumi

Katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006) Katiwa anatumiwa na shangazi yake, Juliana, kama kitega uchumi. Shangazi Juliana anamtoa kwa babu yake Masira na kumpeleka kwa Mam’ Peter kama kijakazi. Katiwa alikuwa anafanya kazi zote za nyumbani lakini hakuna hata siku moja ambayo alipewa mshahara. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Katiwa alimwona Mam’ Peter akimpa shangazi pesa fulani kisha akaondoka…” Kwa nini mimi sipewi pesa zozote?” Alijiuliza (Wamitila, 2006: 47)

Dondoo hili linadhibitisha kwamba Katiwa alikuwa anatumiwa na shangazi yake kama kitega uchumi. Yeye ndiye aliyepewa mshahara wa Katiwa.

Mashirika mbali mbali, jamii na hata serikali inatakikana kuweka sheria za kutumiwa kuhakikisha kwamba watoto yatima hawatumiwi kama vitega uchumi. Sheria hizi zitahakikisha kwamba mtoto yatima amelindwa na kuepushwa kutokana na kutumikishwa. Kuna visa vingi katika jamii ambapo walezi wa watoto yatima hufanyishwa kazi nyingi na ngumu. Kazi hizi zinapofanywa, yatima halipwi chochote bali malipo huenda kwa mlezi wake.

Senefield (2011) anaeleza kuwa baadhi ya mashirika husaidia yatima katika kuwatunza kiafya, kuwapa lishe bora, huwasaidia kisaikolojia, kiuchumi na hata kielimu. Ratiba hii huwasaidia yatima kupata mahitaji ya kimsingi na pia kuwatayarisha ili wajitegemee. Hii ni njia moja ya jamii kuopoa mtoto yatima kutokana na changamoto zinazomkumba.

Katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006) mhusika mkuu Johari ambaye ni yatima anaachishwa shule baada ya kifo cha Mtemi Kido aliyekuwa babake. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Alianzisha bwawa la kuzalishia samaki. Wanakijiji walikuwa wakinunua samaki kutoka kwao. Hata hivyo Zebeli alizichukua pesa zote zilizotokana na mauzo, Johari hakuambulia chochote. (Ng'ang'a, 2006:36).

Maelezo haya yanaashiria kuwa Johari alikuwa anatumiwa na mamake wa kambo, Zebeli, kama kitega uchumi. Alikuwa anafanya kazi nyingi shambani lakini hakupata chochote. Kazi yake yote ilimfaidi mamake wa kambo na binti zake. Johari aliweza

kupata mkulima jirani ambaye alimwokoa kwa kumpa ushauri kuhusu maisha yake nje ya mle shambani. Bidii yake Johari ilimvutia mzee huyu hadi akaamua kumwokoa. Ni wazi kwamba Johari anajiopoa kupitia kwa bidii yake. Safari anayofunga baada ya kufuata ushauri wa Mzee Magufuli inakuwa ndiyo mwanzo wa maisha yake mapya na mwisho was kutumiwa kama kitega uchumi na mamake wa kambo. Mzee Magufuli na Ezekia wanamwopoa na kumwonyesha njia mbadala ya kujikimu kimaisha. Johari anatokea kufaulu katika taaluma ya umakanika na kurudi kuwasaidia jamaa/familia yale iliyomdhulumu hadi kumtelekeza.

Mbali na kujiopoa mwenyewe ni muhimu kuelewa kuwa mashirika ya kibinafsi yanastahili kuanzisha miradi mbali mbali yenye nia ya kusaidia yatima kujiopoa na changamoto zinazowakumba. Miradi hii inaweza kusaidia yatima kuepukana na changamoto za kukosa elimu na kukosa siha njema. Aidha mashirika haya yanaweza kuanzisha miradi ya kiuchumi ambayo inaweza kumfanya yatima aweze kujikimu maishani. Watoto yatima pia wanaweza kuopolewa kama kuna njia bora ya kuwalea watoto hawa ili wapate kuishi na watu ambao watawapa maisha mazuri bila kunyimwa haki, kubaguliwa, kutengwa na hata kutumiwa kama vitega uchumi. Hii itapelekea watoto hawa kukua katika mazingira bora. Pia, ni vyema kuwe na makao mazuri ya watoto yatima ambamo watoto hawa wataishi na kutimiziwa mahitaji yao ipasavyo. Njia hizi zitamsaidia mtoto yatima kujiopoa na kuepukana na changamoto zinazomkumba. (*Carr & Captari, 2013*).

### 4.6 Hitimisho

Sura hii imeangazia njia ambazo yatima anatumia kujiopoa kutokana na changamoto zinazomzingira katika maisha yake. Kutokana na uchanganuzi ambao umefanywa kuhusu suala hili, njia hizi ni pamoja na: njia anazozitumia mtoto yatima mwenyewe kutokana na uwezo wake na njia zilizoko katika ngazi za jamii. Njia zinazojitokeza katika ngazi za mtoto yatima mwenyewe ni pamoja na; kujiweka Imani na kufanya maombi kuhusu hali yake, ujasiri wa mtoto yatima na kufanya bidii katika maisha yake. Hizi ni sifa za kibinafsi. Katika ngazi za kijamii, watoto yatima wanajiopoa kupitia kwa; kusaidiwa na majirani wema kama vile Bettina, mlinzi wa lango kuu na babu yake Katiwa katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila,2006) pamoja na Mzee Magufuli na mwanawe Ezekia. Katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), hawa wawili wanamwopoa Johari kwa kulenga kumstawisha kiuchumi ili aweze kuyakidhi mahitaji yake. Mahitaji ambayo aliyakosa kutosheleza kutokana na hali yake ya uyatima.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulilenga kuchunguza masuala yanayohusiana na maisha ya watoto yatima, yakiwemo; chanzo cha watoto kuwa yatima, changamoto zinazowakumba watoto yatima na jinsi mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto hizo. Utafiti huu umetimiza malengo haya kwa kuzingatia vitabu vitatu teule vikiwemo *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), *Yatima* (Wamitila, 2006) na *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006). Malengo makuu katika utafiti huu yalikuwa; kwanza, kubainisha hali ambazo zinachangia mtoto kuwa yatima katika kazi hizi tatu teule. Hadithi zilizozingatiwa hapa ni baadhi ya kazi za Sanaa zinazojumlishwa kama fasihi ya watoto. Lengo la pili lilikuwa kujadili changamoto zinazowakumba watoto yatima katika jamii na mwisho kuangazia namna mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia changamano zikiwemo nadharia ya vikale (Frye, 1954) na na nadharia ya uhalisia (Larkin, 1977). Nadharia ya vikale hushikilia mihimili kuwa misingi ya miundo ya fasihi inanyambuliwa kwa vikale ambavyo huchukulia fasihi kwa lengo la upana wake. Nayo nadharia ya uhalisia, kwa upande mwingine, ni nadharia inayosisitiza kuwa usanii ni lazima uzingatie maisha yanavyoonekana kupitia kwa hali za maisha ya kila siku. Utafiti huu umetumia nadharia mbili kwa sababu nadharia ya kikale inatekeleza jukumu la kufafanua matini kwa kuchunguza kiini cha visasili vinavyorudiwarudiwa katika hadithi. Visasili hivi ni kama; yatima, kifo, mizozo,wivu,

safari na kadhalika. Nayo nadharia ya uhalisia, inatekeleza jukumu la kuchanganua ujumbe jinsi ulivyo katika ilimwengu halisi au kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira.

Sura ya kwanza ya utafiti huu imeeleza kuhusu mada ya utafiti, malengo ya utafiti pamoja na sababu za kuchagua mada ya utafiti. Hali kadhalika sura hii imeangazia upeo na mipaka ya utafiti huu. Pia, misingi ya nadharia changamano zilizotumika kuongoza utafiti huu zimeangaziwa katika sura hii. Sura hii inaishia kwa kueleza mihimili inayotumiwa kuchanganua data pamoja na kufafanua mbinu zilizotumiwa kuendeleza utafiti huu.

Sura ya pili imechunguza hali zinazochangia watoto kuwa yatima. Baadhi ya hali ambazo zimejadiliwa ni pamoja na mizozo katika familia, tabia za wivu na tamaa, magonjwa na mikasa. Hali hizi zimejitokeza hasa ikizingatiwa jinsi ambavyo waandishi wa kazi hizi tatu teule wamezisawiri hoja kuu katika kazi zao.

Sura ya tatu imeangazia changamoto zinazowakumba watoto yatima. Baadhi ya masuala ibuka ambayo yanajitokeza katika uchanganuzi na tafakari zilizofanywa katika sura hii ni pamoja na kufanyishwa kazi nyingi na ngumu, mtoto yatima kunyimwa haki na uhuru wake; kutengwa, kubaguliwa na kutelekezwa na jamii; kutumiwa kwa mtoto yatima kama kitega uchumi na mtoto yatima kuishi katika mazingira magumu.

Sura ya nne nayo imeziangazia njia na mbinu anazozitumia mtoto yatima kujiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba. Njia na mbinu hizi zimegawanywa katika makundi mawili yakiwemo; njia zinazotumika katika ngazi za mtoto yatima mwenyewe na zile zilizoko katika ngazi za jamii. Njia zinazojitokeza katika ngazi za mtoto yatima mwenyewe ni pamoja na kujiweka imani na kufanya maombi kuhusu hali yake, ujasiri wa mtoto yatima mwenyewe na kufanya bidii katika maisha yake.

Kwenye ngazi za kijamii, mbinu wanazozitumia watoto yatima kujiopoa kutokana na changamoto zao ni pamoja na kusaidiwa na majirani. Majirani hawa wema ni pamoja na Bettina, mlinzi wa lango kuu na babu yake Katiwa. Jirani wengine, hasa katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), ni kama Mzee Magufuli pamoja na mwanawe Ezekia wanaomwopoa Johari kwa kulenga kumstawisha kiuchumi ili aweze kujiendeleza. Hata hivyo, katika hadithi hizi tatu, hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), ndiyo inayokiuka mihimili ya nadharia ya uhalisia kama inavyoongoza utafiti huu. Njia na mbinu anazotumia Kalaa kujiopoa si njia ambazo zinaambatana moja kwa moja na hali inavyokuwa katika maisha ya jamii. Kwa mfano, hata kama kufanya maombi ni jambo la kawaida, si kawaida kupata majibu papo kwa hapo kwa njia ya kimiujiza kama vile mambo yanavyomtendekea Kalaa. Hata kama utafiti umewahi kuzishughulikia hali hizi ngumu zinazowakumba watoto yatima, kunao uhaba wa tafiti zinazolishughulikia suala hili kifasihi. Kwa hivyo, mchango mkuu wa kazi hii ni kutoa mtazamo wa kifasihi kuhusiana na suala hili la hali ya watoto yatima na kuangazia vile ambavyo uchanganuzi umebaini namna mtazamo huu unatofautiana au kufanana na mitazamo mingine.

## 5.2 Hitimisho

Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa kuna masuala ambayo yameibuka hasa kuhusiana na hali ya watoto yatima. Masuala haya ni pamoja na hali zinazochangia watoto kuwa yatima yakiwemo mambo kama magonjwa, kukosa kuelewana katika familia, tabia kama hasira na hata mikasa. Pia, kumekuwa na masuala kuhusiana na changamoto zinazomkumba mtoto yatima. Hali kadhalika jinsi ambavyo mtoto yatima anajiopoa kutokana na changamoto hizi.

Katika utafiti huu, imebainika kuwa wasanii wa vitabu hivi vitatu teule wameyasawiri masuala haya kwa kutumia na kuongozwa na dhana zinazoyaweka katika hali inayoambatana na uhalisia wa mambo kama inavyokuwa katika maisha ya kawaida. Kwa mfano, katika hadithi ya *Mama wa Kambo* (Kisovi, 2005), mwandishi amesawiri hali inayomfanya Kalaa kuwa yatima na pia changamoto anazokutana nazo katika maisha kwa hali inayofanana na vile ambavyo maisha ya kawaida yalivyo. Hali ya uhusiano kati ya Kalaa na Kitete ni ya utata kama vile ambavyo imeweza kushuhudiwa katika jamii hata ya sasa. Hali ni hiyo hiyo katika hadithi ya *Mateso ya Johari* (Ng'ang'a, 2006), ambamo Zebeli anatokea kumwachisha Johari shule kisha kumfanyisha kazi ngumu na nyingi pia. Katiwa naye anahangaishwa na Mam' Perter katika hadithi ya *Yatima* (Wamitila, 2006), ikiwemo kunyimwa lishe bora, masomo, haki za aina mbalimbali na hata kuwa katika mazingira magumu.

Kwa hivyo, katika kuchunguza masuala ya maisha ya watoto kwa vigezo vinavyoashiriwa na malengo ya utafiti huu, imebainika kuwa waandishi wameweza kufaulu kuwasilisha hoja na mitazamo yao kwa kuzikita kazi zao za sanaa katika misingi ya mihimili ya nadharia ya uhalisia. Kwa kutumia nadharia hii katika kusawiri maisha ya watoto hawa yatima, waandishi wameweza, sio tu kuwasilisha ujumbe wao kwa urahisi, bali kuvutia msomaji wa fasihi ya watoto wakiwemo wasomi wenye umri mdogo ambao ni watoto pia.

Katika kusimulia hadithi hizi zinazoangazia masuala ya maisha ya watoto yatima, ni vizuri kusisitiza kuwa waandishi hawa wote wameweza kutumia mandhari inayoaminika na wala sio kufikirika tu. Mifano ya mandhari ambayo imetumika katika hadithi hizi tatu ni pamoja na maisha ya kijijini, mjini, maisha ndani ya familia kwa kutaja tu. Kwa kufanya hivyo, waandishi hawa wameweza kuleta uhalisia mwafaka katika kazi hizo na pia kuweza kukubalika na pia kufahamika na watoto.

### 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umeangazia hasa usawiri wa mtoto yatima, changamoto zinazomkumba mtoto yatima na jinsi ambavyo mtoto yatima anavyojiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba. Utafiti ulihusisha vitabu vitatu vya hadithi katika fasihi ya watoto. Hata hivyo, masuala haya ya usawiri wa mtoto yatima, changamoto zinazowakumba na jinsi watoto hao wanavyojiopoa kutokana na changamoto hizi yamejadiliwa kuzingatia mipaka na peo za hadithi hizi tatu. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kuzingatia na

kurejelea aina zingine za fasihi kama vile mashairi, hadithi fupi, tamthilia na hata vitabu vya lugha vilivyo kwenye mtaala ambavyo vimependekezwa na taasisi ya kukuza mitaala na vilivyo na sehemu zinazozungumzia masuala ya watoto yatima. Kwa upande mwingine, utafiti huu uliegemea sana kazi na habari zilizohifadhiwa maktabani. Kwa hivyo, inapendekezwa kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu masuala ibuka kule nyanjani. Kwa kufanya hivyo, mwelekeo huu utatoa nafasi ya kuwahusisha washika dau wengine wanaohusiana na masuala ya watoto yatima kwa uhalisia. Washika dau hawa ni kama vile walezi, walimu, viongozi wa serikali katika mitaa, maafisa wa watoto, waandishi, wakuza mitaala na kadhalika.

## MAREJELEO


Abashula, G., Ayele, T., & Jibat, N. (2014). "The Situation of Orphans and Vulnerable Children in Selected Woredas and Towns in Jimma Zone". In *International Journal of Sociology and Anthropology,* 6(9), 246-256.

Ahmed, H. (2012). The Impact of Public School Enrolment on Child Labour in Punjab, Pakistan. *The Lahore Journal of Economic*, 17 (2), 1-35.

Arbuthnot, H. na Sutherland, Z. (1972). *Children Literature.* U.S.A. Scotty California.

Ayieko, M. A. (1997). *From Single Parents to Child-headed-Households: The Case of Children Orphaned by AIDS in Kisumu and Siaya Districts.* UNDP, New York.

Benedicts, T., Jafle S.J. (2006). Child Abuse*:* Types and Symptoms.*Mental Health Issues.* Internet Publication. Pp. 23.

Bloom, L. & Ottony, J (1987). *Changing Africa: An Introduction to Sociology*. London: Macmillan Publishers.

Bolby, J. (1969). *Attachment and loss vol.1.* New York: Basic Books.

Campbell, J. (2004). The Hero with a Thousand Faces. Princeton UP.

Canary, H., Canary, D. (2013). *Family Conflict: Managing the Unexpected*. New York: John Wiley & Sons.

Carr, J. & Captari, L. (2013). *Orphan Justice: How to care for Orphans Beyond Adopting.* Nashville: B&H publishing group.

Constantino, C., Ganga, E. (2013). The Effect of HIV and AIDs on the Academic Performance of Orphaned and Vulnerable Children from Child Headed Families. *International Journal of Learning & Development.* 62-69.

Daemmrich, H.S. (1985). Themes and Motifs in Literature: Approaches: Trends: Definition German katika Quartely, 566-575.

David, K. (2009). *Challenges facing AIDS orphans in Nairobi Kibera Slums,* unpublished Bachelor's Thesis, Turnun Ammattikorkeakoulu Turku University of Applied Science.

Davies, R. (2017). Kenya – Deadly Floods in Mombasa After 235mm of Rain, Thousands Displaced in Taveta, Daily Nation Newspaper, 10 May, 2017, Online Edition. Available at: http://floodlist.com/africa/kenya-mombasa-may-2017.

Doodson, L. J, & Davies, A. P. (2014). "Different Challenges, Different Well-being: A Comparison of Psychological Well-Being across Step Mothers and Biological Mothers and across four Categories of Stepmothers". *Journal of Divorce and Remarriage,* Pp, 49-63.

Edmonds, E (2009). Defining child labor: A Review of Definitions of Child Labour in Policy Research. Geneva: International Labour Organisations. Pp.35.

Esterhammer, A. (2005). "Blake's Treatment of the Archetype." *Northrop Frye on Milton and Blake.* Toronto: University of Toronto Press. 190–206.

Gelles, R. J. (1973). Child Abuse as Psychopathology. *A Social Critique and Reformation,* 623- 628.

Guerin, W. L. et al. (2005). "Mythological and Archetypal Approaches." *A Handbook of Critical Approaches to Literature.* New York: Oxford UP. 182-221.

Hollingsworth, J.M. (2013). *The Social Problems of Children in Sub-saharan Africa*. Newcastel: Cambridge Scholars Publishing.

Huck, C. (1976). *Children's Literature in Elementary Schools*. 3rd Edition. New York: Holt Rhinehart.

Hugborg, A. S. (2010). *Family Relations in Harry Portter:* From Jungs Viewpoint. Reykjavik. University Press.

Judy, L.L. (1999). *Individualism and the orphan Archetype.* A Phenomological Study Proquest. LLC Michigan.

Kahenya, P. W. (1992). Children's Literature: An analytical Study of the content value of Tin Tin Comic. M.A. Thesis, University of Nairobi. (Haijachapishwa)

Karanja, D. W. (2008). Usawiri wa Masuala-ibukizi katika hadithi za watoto. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kavuria, P. N. (2000). Dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kell, A.J. (1983). *Treating Child-Abusive Families.* New York: Plenum Press.

Kisia, A. (1996). *Watoto wa Mitaani.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Kisovi, C. N. (2005). *Mama wa Kambo.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Larkin, M. (1977). *Man and Society in the Nineteenth Century Realism.* London: Macmillan Press.

Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism.* A sociological survey of writings of Balzac, Stredhal, Zola, Tolistoy, Gorki na wengine. London: Marlin Press.

Lukens, R. (1990). *A critical Handbook of Children's Literature.* 4th Ed. New York: Harper Collins.

Lynch-Brown, C. & Tomlison C. M. (2008), "Realistic Fiction." In *Essentials of Children's Literature*. Boston: Pearson/Allyn & Bacon, 150-67.

Mc Mahon, J. W. na wengine (1990) *Psychology and You.* New York: Los Angeles, San Francisco: West Publishing Company.

Meier, J. (1985). *Assault Against Children.* San Diego California. College Hill Press.

Melanie, A.K. (1999). *From Folktales to Fiction: Orphan Characters in Children Literature.* Library Trends.

Mpesha, N. (1995). Children's Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its growth and Development. Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Munawar, A. (2015, June 4). *11 Countries with the Highest Rates of Orphans in the World.* Retrieved August 17, 2017, from Insider Monkey: https://www.insidermonkey.com/blog/11-countries-with-the-highest-rates-of-in-the-world-351524/

Nairobian Writer (2016). *Bungoma barmaid in court for stabbing and killing co-wife - SDE,* The Nairobian Newspaper, 31 October, 2016. Online Edition. Available at: https://www.sde.co.ke/thenairobian/article/2000124779/bungoma-barmaid-in-court-for-stabbing-and-killing-co-wife.

Nayak, B. K. (2014). Orphans Problems and Community Concerns in Ethiopia. *International Journal of Management and Social Sciences Research.* 3(1), 8-15.

Ndungo, C. M. (1998). "Images of Women in Gikuyu and Literature*: A Case of Gikuyu And Swahili Proverbs."* Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Ng'ang'a, S. (2006). *Mateso ya Johari.* Nairobi: Moran (E.A) Publishers Limited.

Nikolajeva, M. (2002). *The Rhetoric of Character in Children's Literature.* Lanham-Maryland. U.S.A.: The Scarecrew Press.

Norton, D. E. and Norton, S. E. (2011),"Contemporary Realistic Fiction." In *Through the Eyes of a Child: An Introduction to Children's Literature*. Boston: Pearson, 356-94.

Northrop, F. (1957). *Anatomy of Criticism: Four Essays.* United States of America. Princeton University Press, Princeton, New Jersey.

Northrop, F. (2001). *The Archetypes of Literature. The Norton of Anthropology Theory and Criticism.* New York. Ed. Vincent B. Leitch.

Nyambedha, E. O. na wengine (2003). "Retirement Lost" – The new role of the elderly as caretakers for orphans in Western Kenya. Katika *Journal of Cross-Cultural Gerontology* 18:35-52: U.S.A. Kluwez Academic Publishers.

Nsagha, D. S., Bissek, A. Z., Nsagha, S. M., Assob, J. N., Kamga, H. F., Njamnshi, D., Njamnsi, A. K. (2012). The Burden of Orphans and Vulnerable Children due to HIV/AIDS in Cameroon. *The Open AIDS Journal,* 6(1), 245-258.

Odhiambo, T. (2004). "From Fairyland to lived life Narrative transitions in David Maillu's Fiction." Katika *Journal of African Children's and Youth Literature.* The Free Library.

Oyedele V, Chikwature, W. & Manyanga, P. (2016), *Challenges facing orphaned student and the effects on academic performance in 0-level commerce at Samaringa Cluster Secondary school* International Jouranal of Academic Research and Reflection Vol. 4 No 3, pp.20.

Plaks, A.H. (1976). *Archetype and Allegory in the Dream of the Red Chamber;* Princeton and Guildford, Survey: Princeton University Press.

Raptim Humanitarian Travel (2016, October 17). *Focus on NGOs: 42 Organisation that Help Children in Need.* Retrieved August 18, 2017, from https://www.raptim.org/focus-on-ngos-42-organizations-that-help-children-in-

need/

Republic of Kenya (2001), *Children Act*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya (2001). Children Rights. Nairobi. Government Printer.

Republic of Kenya (2010). The Constitution of Kenya. Nairobi. Government Printer.

Russell, D. L. (2012), Realistic Fiction: The Days of Our Lives." In *Literature for Children: A Short Introduction'*. Boston: Pearson, 222-50.

Russell, F. (2000). "Jung and Frye." Northrop Frye on Myth. New York: Routledge. 116-22.

Senefeld, S. Strasser, S. & Campbell, J. (2009). *Orphans and Vulnerable Children Wellbeing Tool: User's Guide.* Nairobi: Catholic Relief Services.

Sengendo, J. na Nambi, J. (1997). The Psychological effect of Orphanhood. Katika *Health Transition Review,* Supplement to Volume 7. 105-124.

Snicket, L. (1999). *The Bad Beginning.* Herpes Collins (US).

SOS Children's Villages. (2016, April). *Worldwide Children's Statistics.* Retrieved August 17, 2017, from http://www.sos-usa.org/our-impact/childrens-statistics.

Spinetta, J. & Rigler, D. (1972). The Child Abusing Parent. *A Psychological Review.* 296-304.

Tadele, G., & Kloos, H. (2013). *Vulnerabilities, Impacts and Responses to HIV/AIDs in Sub-Saharan Africa.* Berlin: Springer.

Tassoni, P. (2002). *Certificate in Child Care and Education.* (third edition). Halley Court: Heinman Educational Publishers.

Tomison, A.M. (1996). *Child Maltreatment and Substance Abuse.* Discussion Paper Number 2. Spring 1996. Australian Institute of Family Studies.

Tucker, N. (1981). *The Child and the Book: A Psychological and Literary Exploration.* Cambridge University Press.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. East Africa: Oxford University Press.

Voigt, K., & Brown, S. (2013, September 17). *International Adoptions in Decline as Number of Orphans Grows.* Retrieved August 17, 2017, from CNN Home:

http://edition.cnn.com/2013/09/16/world/international-adoption-main-story-decline/index.html.

Wafula, R. M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wainaina J. (2018). *Juja man who killed himself, wife and 3 kids had money problems*, THE STAR Newspaper, 17, January 2018. Online Edition, available at: https://www.the-star.co.ke/news/2018/01/17/juja-man-who-killed-himself-wife-and-3-kids-had-money-problems_c1699078

Walker, S. F. (2002). Jung and the Jungians on Myth: An Introduction. New York: Routledge.

Wamuswa N. (2016). Voices from Budalangi on the never ending floods Standardmedia, August 31st 2016. Available at: https://www.standardmedia.co.ke/lifestyle/article/2000214025/voices-from-budalangi-on-the-never-ending-floods


Wamitila, K. W. (2006). *Yatima.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Winding, T. (2007). Lost and Found: The Orphaned Hero in Myths, Folklore and Fantasy Journal of Mythic Arts.

Zaman, S., Martin, S. & Kibria, A. M. (2014). A study on Present Scenario of Child Labour in Bangladesh. *Journal of Business and Management*, 16(6), 25-36.

**VIAMBATISHO**





**KIAMBATISHO 1**

Picha inayoonyesha Johari akienda shambani badala ya shule kama wengine (Mateso ya Johari, Ng'ang'a 2006: Jalada).



**KIAMBATISHO 2**

Picha inayoonyesha Johari Shambani (Ng'ang'a 2006: 32).




**KIAMBATISHO 3**

Picha inayoonyesha Katiwa akifukuzwa na babu yake (Wamitila, 2006: 9).



**KIAMBATISHO 4**

Mam’ Peter akimpiga mtoto yatima (Wamitila, 2006: 51).



**KIAMBATISHO 5**

Mwilu akizikwa hai na mamake wa kambo (Wamitila, 2006: 23).




**KIAMBATISHO 6**

Picha inayoonyesha mtoto yatima akisokotwa na tumbo (Wamitila 2006: 26).




**KIAMBATISHO 7**

Kalaa akivalia matambara huku Pendo akionekana nadhifu (Kisovi, 2005: 29).




**KIAMBATISHO 8**

Mtoto yatima anajaribu kujiopoa kutokana na changamoto zinazomkumba (Wamitila 2006: Jalada).



**KIAMBATISHO 9**

Mtoto Yatima ameopolewa hatimaye, na sasa anaenda shuleni (Wamitila 2006: 82).